Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

EQUIPPING CHURCH LEADERS
• EAST AFRICA •

UKRISTO NA UISLAMU:
Mambo Muhimu—Sehemu ya Pili

Mwandishi

Jonathan M. Menn

B.A., University of Wisconsin-Madison, 1974
J.D., CornellLawSchool, 1977
M.Div., Trinity Evangelical
Divinity School, 2007

Equipping Church Leaders-East Africa
3701 N. Gillett St., Appleton, WI54914
(920) 731-5523
jonathanmenn@yahoo.com
www.eclea.net

2015; kimepitiwa Machi 2016; marekebisho Juni-Novemba 2016, Julai 2018; kimepitiwa Aprili 2019; marekebisho Mei 2019

Haya ni mafafanuzi ya Uislamu kutokana na mtazamo wa Kikristo na malinganisho ya mafundisho ya Kikristo na Kiislamu. Sehemu ya pili inajumuisha majadiliano ya Yesu kama yanavyopatikana kwenye Korani na kuangalia tabia za Mohamedi. Inajadili pia dhambi na wokovu kulingana na Ukristo na Uislamu na kiasi kikubwa cha tofauti ya matokeo ambacho kila moja inayo.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

2. YESU NA MOHAMEDI

VIII. Korani yenyewe inamweka Yesu juu kuliko mtu mwingine awaye yote (ikiwa ni pamoja na Mohamedi) na kwa umuhimu kumpa yeye hadhi ya Kiungu ….2
A. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyeanza kutenda miujiza*……...2
B. *Yesu, siyoMohamedi, ni "Neno" la Mungu*……...5
C. *Yesu, siyo Mohamedi, ni "Roho" toka kwa Mungu*……...6
D. *Yesu, siyo Mohamedi, ni "Masihi"*……...6
E. *Yesu, siyo Mohamedi, asiye na waa, mtakatifu, na asiye na dhambi wala kosa toka alipozaliwa*……7
F. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyelindwa kutokana na ushawishi wa Shetani*……...9
G. *Yesu, siyo Mohamedi, mwenye baraka za kipekee na heshima kwa Allah kwenye ulimwengu huu na ujao*.....10
H. *Yesu, siyo Mohamedi, ni "Ishara" kwa watu wote wa duniani.*.....11
I. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyetenda ishara na miujiza*……...11
J. *Yesu, siyo Mohamedi, mwenye ujuzi usiokuwa wa kawaida*……..……12
K. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyefundisha kwa mamlaka ya Kiungu*……...13
L. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyepandishwa mbinguni akiwa hai ambako bado akingali hai*……..…….....13
M. *Yesu, siyo Mohamedi, atakayekuja tena ulimwenguni kuhukumu na kutawala*.....14
N. *Hitimisho*…….....14

IX. Tabia za Mohamedi……..……14
A. *Mohamedi na pesa*…….....15
B. *Mohamedi na wanawake*…….....16
C. *Mohamedi na nguvu*……...18
D. *Mohamedi na mauaji*……..19
E. *Hitimisho*……20

3. DHAMBI NA WOKOVU

I. Utangulizi……21

II. Dhambi na Wokovu Kulingana na Ukristo……..……..22
A. *Maana ya dhambi*……...22
B. *Asili ya dhambi na madhara yake kwa watu*……23
C. *Kutokuwezekana kwa mtu kujiokoa mwenyewe kwa matendo yake mema*……..23
D. *Wokovu kulingana na Ukristo: kile Kristo alichokikamilisha pale msalabani*.....25
E. *Matokeo ya dhambi na wokovu kulingana na Ukristo*……...……...27

III. Dhambi na Wokovu Kulingana na Uislamu……..……..……..28
A. *Asili ya ubinadamu na mahusiano ya dhambi kulingana na Uislamu*……29
B. *Wazo la uadilifu kwenye Uislamu*……..29
C. *Wazo la dhambi kwenye Uislamu*……...30
D. *Tofauti na mafundisho yake rasmi, Uislamu kwa kweli unakubali kuwa mwanadamu anayo dhambi ya asili*….32
E. *Wokovu kulingana na Uislamu*……..……35
F. *Matokeo ya dhambi na wokovu kulingana na Uislamu*……..……...38

IV. Dhambi na Wokovu: Hitimisho……...46

ORODHA YA VYANZO……..……47

MWANDISHI……..……..….47

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

VIII. Korani yenyewe inamweka Yesu juu kuliko mtu mwingine awaye yote (ikiwa ni pamoja na Mohamedi) na kwa umuhimu kumpa yeye hadhi ya Kiungu

Mohamedi alisema, "Mimi ninafanana sana na Yesu Kristo miongoni mwa wanadamu wote" (Muslim: 2365b; angalia 2365a, c; al-Bukhari: 3442, 3443). Korani yenyewe imejaa maandiko mengi ambayo, moja kwa moja au vinginevyo, yana mlinganisha Yesu na Mohamedi. Siyo tu Kwamba Yesu ametajwa kwa jina kwenye Korani mara tano Zaidi ya kutajwa kwa Mohamedi (Deedat 2002: 4), lakini mtihani wa usawa wa maelezo ya Yesu kwenye Korani yanatuongoza kwenye hitimisho kwamba Korani inamweka Yesu juu kuliko kila mmoja (ikiwa ni pamoja na Mohamedi) na kwa umuhimu kumpa Yeye hadhi ya Kimungu ingawa kimsingi mafundisho ya Kiislamu yanakataa hilo. Kwa suala hilo hivyo inaweza kufanyika kwamba watetezi wa Kiislamu wa kisasa wanamshusha na kumwelezea isivyo Yesu, *kama alivyoonyeshwa kwenye Korani,* kwa sababu Waislamu waliojifunza maisha ya Yesu na kumlinganisha na Mohamedi watamwendea Yesu na kumwacha Mohamedi mbali. Hayo maelezo ya Korani ni pamoja na haya yafuatayo:

A. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyeanza kutenda miujiza*

Muislamu wa Awali Abd al-Masih alisema, "Kama kwa Kristo, Korani imesema mara kadhaa kwamba hakuzaliwa kwa njia ya kawaida, kama sisi tulivyo. Baba yake hakuwa mwanadamu. Alitungwa mimba kwa bikira Mariamu [**Q. 19:20-22**] bila mwingiliano wa baba mwanadamu, kwa kuwa Allah alimpulizia pumzi yake kwa Mariamu. Hili linamfanya Kristo—kwa uhakika—kuwa yeye pekee kwenye Ulimwengu wote ambaye alizaliwa kwa neno la Mungu na Roho wake." (al-Masih 1993: 8)[1]

---

[1] Tafsiri ya Hilali-Khan inajaribu kufifisha suala hilo kwa kusema kwamba ni malaika Gabriel, siyo Roho wa Allah, "aliyemvuvia" Mariamu. Tafsiri yao ya **Q. 21:91** inasema *"Tulivuvia kwenye (vazi) la Mariamu (shati au nguo) [kupitia malaika wetu Gabrieli]."* Tafsiri yao **Q. 66:12**: *"Tulivuvia kwenye (vazi la shati au nguo za Mariamu)kupitia malaika wetu Gabrieli]."*Dirks anasimulia **Q. 2:97** inayosema kuwa Gabrieli alileta ufunuo kwa Mohamedi na **Q. 16:102** inayosema kwamba Roho mtakatifu alileta ufunuo kwa Mohamedi na kuhitimisha kwamba "Gabrieli siyo Zaidi ya Roho mtakatifu . . . malaika wa Allah apelekaye ujumbe kwake kwa wanadamu" (Dirks 2008: 197).

Kwa kiasi kidogo kama alivyohusika na kutungwa mimba ya Yesu, kumtafsiri Roho mtakatifu kama Gabriel haitakuwa sahihi. Kwanza, **Q. 21:91** na **66:12** zote ziansema *"Tulimvuvia ndani yake (Mariamu Roho wetu,"* siyo "malaika Gabrieli alimvuvia." Haleem anasema Korani mara nyingi hutumia neno "'sisi', mtu wa kwanza kwa wingi wa ukuu wake, kumwakilisha yeye mwenyewe [Allah]" (Haleem 2005: xx). Pili, Kiarabu ni *rūhinā* (kutoka *rūh,* "roho"), ambalo hakika lina tafsiri ya*"Roho wetu."* Watafsiri wengi (Ali, Pickthall, Sarwar, Arberry, Haleem) hutafsiri kwa njia hii. Mawdudi anasema kwamba "kuzaliwa kwa Nabii Yesu (Amani iwe juu yake) hakukuwa tofauti na kuzaliwa kwa Nabii Adamu, maneno ya Kiarabu kwenye matukio haya mawili [linganisha **Q. 21:91;66:12** (Yesu) na **15:29; 32:9; 38:72** (Adam)] ni kama yanafanana" (A'la Mawdudi n.d.: Q. 21:91n.89). Hakuna mahali kwenye Korani panaposema kwamba Gabrieli alimvuvia Adamu.

Kuhusiana na Adamu, Mawdudi anaelezea, "'Na alivuvia ndani yake Roho Wangu [*rūhī*]' inamaanisha wakati nilipomwekea tabia yangu ya kiungu ndani yake. Hii inatuonyesha kwamba nafsi ya mtu hubeba uhai, maarifa, nguvu, utashi, uchaguzi na tabia nyingine za mwanadamu kwenye ujumla wake." (Ibid.: Q. 15:29n.19) Ali hali kadhalika anakuita kule kupuliziwa pumzi "Roho yangu" kwenye **Q. 15:29**, "kitengo cha ujuzi wa kufanana na Mungu" kinalisema hili kama upande wa juu wa mwanadamu, kitengo kilifikishwa hapo na Roho wa Allah" (Ali 2006: Q. 15:29n.1968). Kwa hilo **Q. 32:9** Mawdudi anaongeza, "Allah analiita hili 'Roho' Yake mwenyewe labda kwa sababu ni mali yake mwenyewe, na iliwekwa kwake Mwenyewe ni kama kitu kinachowekwa kwa Bwana wake, au kwa sababu ya asili ya ujuzi, wazo, nafsi, utashi, hukumu, uchaguzi, nk. Ambavyo mwanadamu amewezeshwa kuwa navyo ni taswira ya tabia ya Allah" (A'la Mawdudi n.d.: Q. 32:9n.16). Wavuti ya Kiislamu *IslamAnswering.com* inahitimisha kwa kufanana, "Alimuumba mwanadamu kwa kumpulizia Roho yake mwenyewe ndani (Qur'an, 15:29; 32:9; 66:12). Kwa kuwa kwa uhakika Mungu ni mwema siku zote na Roho wake wakati wote hana waa; kwa kuwa mwanadamu, kupitia uumbaji, aliipokea Roho ya Mungu, basi mwanadamu amefungwa kupokea angalau sehemu ya Roho hiyo njema ya Muumba." ("Wazo" 2009: n.p.) Kwa hiyo, "Roho" kwenye **Q. 21:91; 15:29; 32:9** na **66:12** haimzungumzii malaika Gabrieli.

Q. 2:87, 253, na **5:110** zote zinasema kwamba Allah "*alimtia yeye[Yesu]kwa Roho mtakatifu* [Ruh Al-Qudus]." Neno wakati wote limetafsiriwa "Roho mtakatifu" (Ali, Pickthall, Shakir, Sarwar, Arberry, Haleem; angalia pia **Q. 16:102**). Reynolds anaonyesha, "Aya hizi [**Q. 2:87, 253; 5:110**] anawaza kwamba kwa 'Roho mtakatifu' Korani haimaanishi malaika, na kwamba Korani inatumia maelezo hayo sawasawa na maana iliyopo kwenye Biblia . . . kumaanisha nguvu ya Kiungu. Wazo hili linafanana na jinsi Korani inavyozungumza juu ya "Roho" wa Mungu,' aliyekuwa mtendaji kwenye uumbaji (Q 15:29; 32:9; 38:72) na ufunuo (Q 16:102; 26:192-93) kwenye amri za Mungu (Q 17:85)." (Reynolds 2018: 427) Hata hivyo, Hilali-Khan anamleta tena malaika Gabriel kwenye aya kitheolojia na siyo kwa sababu za maneno kwa kusema *"alisaidiwa na Ruh-ul-Qudus [Jibrael (Gabriel)]."* Wakati huo wachambuzi wengine wakisema kwamba walimaanisha ni Gabrieli (e.g., Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 2:87, maoni; Jalal 2013: Q. 2:87, maoni), siyo kwa kila alichokifanya. Ali anaeleza kwamba **Q. 2:87** inamaanisha kwamba Allah "kwa neno lake alimpa yeye [Yesu] nguvu za kiroho—'akamtia nguvu kwa Roho mtakatifu'" (Ali 2006: Q. 3:32n.401; angalia pia A'la Mawdudi n.d.: Q. 2:87n.93 ["inakumbusha pia kwamba Roho mtakatifu wa Yesu, Roho ambaye Mungu alimtoa kwa tabia ya kimalaika"]).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Kulingana na muujiza na nguvu zisizo za kawaida za kutungwa mimba kwa Yesu, islamu wengi wanasisitiza **Q. 2:117; 3:47, 59; 19:21, 35** kwamba ili kuwepo na matokeo ni Allah pekee mwenye uwezo wa kusema "Iwe!" na chochote anachokitaka (pamoja na Yesu) kikaumbika (angalia pia **Q. 16:40; 36:82; 40:68**). Walikusudia pia kuushusha upekee wa Yesu kwa kumlinganisha na Adamu, i.e., "Kama inasemekana kwamba alizaliwa bila Baba mwanadamu, Adamu pia alizaliwa hivyo. Kwa hakika Adamu alizaliwa bila kuwa na Baba wala Mama mwanadamu." (Ali 2006: Q. 3:59n.398; angalia pia A'la Mawdudi n.d.: Q. 3:59n.53; Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 3:59, maoni; Deedat 2002: 25-26) Hata hivyo, Adamu na Yesu wanatofautiana kimsingi kwa angalau sababu mbili:

- Kwanza, Adamu aliumbwa kwa vitu vilivyokuwepo—vumbi la ardhi (**Mwanzo 2:7; Q. 3:59; 7:12; 32:7; 38:76**). Wanadamu wengine wote wameumbwa kwa kizazi cha wanadamu (kwa muunganiko wa mbegu na yai). Kwa suala la Yesu, "Kuzaliwa kwa Yesu – na upekee wake kwa wanaume na wanawake wote kwenye historia ya mwanadamu – haikuwa nguvu isiyokuwa ya kawaida tu lakini *kinyume na maana ya asili*. Adamu na Hawa waliumbwa – Yesu *alizalishwa* kwa njia isiyokuwa ya kawaida kabisa ambayo ilivamia na kusumbua maana nzima ya kawaida ambayo mtoto huletwa kwayo Ulimwenguni. Ni lazima kuwe na sababu maalum kwa kuzaliwa huku kwa kipekee." (Gilchrist 2015: 64, fafafnuzi imeongezwa) Biblia inatuambia kwamba kulikuwa na "sababu maalum sana kwa kuzaliwa huku kwa njia ya kipekee: **Luka 1:35** inasema kwamba Yesu atakuwa mwana wa Mungu; **Math 1:21** inasema, *"Atawaokoa watu wake na dhambi zao."* Hivyo, "maisha yake yalianza kwa njia isiyokuwa ya kawaida kwa sababu alikuwa na *tabia ya kipekee* aliyekuja dauniani akiwa na *jukumu la kipekee*, kuleta wokovu na uzima wa milele kwa wale wote watakaomkubali yeye kama Bwana na mwokozi wa Maisha yao" (Ibid.: 67, fafanuzi imeongezwa).
- Pili, Adamu na Yesu wako *tofauti* sana. Kwa wanadamu wote wengine, akiwapo Adamu, "*Pumzi ya Mungu ndani yao"* ndiyo iwapayo wanadamu uhai; humfanya mwanadamu kuwa Zaidi ya mnyama (Ali 2006: Q.32:7-9, nn.3637-40; angalia **Mwanzo 2:7; Q. 15:29; 32:9**). Hata hivyo, kwenye suala la Yesu, Allah alimpulizia Roho *kwa Mariamu*, siyo kwa Yesu, ili Yesu kuuvaa mwili moja kwa moja na kwa njia isiyoingiliwa (**Q. 21:91; 66:12**). "Adamu *aliumbwa* kwenye hali ya mtu mzima jambo ambalo halingewezekana kwa kuzaliwa na wazazi mwanadamu. Mtu alipaswa aumbwe kwanza. Lakini Yesu *alizaliwa* na mwanamke mwenyewe wakati ambao agizo la Mungu la uumbaji wa asili lilikuwa limeshatekelezwa kwa karne zilizopita. Ni wazi kwamba kwanini Adamu hakuwa na Baba wala Mama.

Q. 58:22 inasema kwamba Allah *"aliwatia nguvu [waamini wa kweli] kwa Roho kutoka kwake mwenyewe."* Ali anaelezea: "Allah alimtia nguvu Nabii Yesu kwa Roho mtakatifu. Hapa tunajifunza kwamba kila mtu mwema na mwenye haki hutiwa nguvu na Allah kwa Roho mtakatifu. Kama kitu chochote, msemo unachokisema hapa kina nguvu, 'Roho kutoka kwake mwenyewe'. Popote pale mtu yeyote atakapojitoa kwa moyo wake na imani na usafi kwa Allah, Allah atakikubali, huangalia imani iliyoko kwenye moyo wa yule anayemtafuta, na zaidi humjalia yeye Roho wa kiungu, ambaye hatuwezi kumwelezea kwa utoshelevu Zaidi ya kumwelezea kwa lugha ya kibinadamu kwa asili na sifa za Allah." (Ali 2006: Q. 58:22n.5365) Sam Shamoun anaelezea, "Ili huyu Roho aweze kumwezesha kila mwamini halisi kwa wakati huo huo ni lazima awepo yeye mwenyewe na wao popote pale walipo na ni lazima awe na nguvu ya Kimungu kuwalinda na kuwahifadhi wao wote" (Shamoun, "Quran" n.d.: n.p.) Hivyo, "Roho" hawezi kuwa Gabrieli ambaye ana ukomo wa kuwa mahali pamoja kwa wakati mmoja na haijawahi kusemekana kwamba aliwatokea waamini wote kwa wakati mmoja.

Mohamedi alithibitisha kwamba "Roho" aliyewasiliana na Yesu siyo Gabriel. Alisema, "Yeye aliyesema: 'Hakuna mungu isipokuwa Allah, Yu pekee wala hana mshirika naye, kwamba Mohamedi ni mtumishi na mjumbe wake, kwamba Kristo ni mwana wa binti- mtumwa wake na yeye (Kristo) Neno lake ambalo aliwasiliana nalo na Mariamu *na ni Roho wake*, kwamba Paradiso ni kweli ipo na kuzimu kweli ipo,' Allah atamfanya yeye (atakayethibitisha kweli hizi) kuingia Paradiso kupitia milangoni, mlango mmojawapo wa milango yake nane atakaopenda" (Muslim: 28a; angalia pia al-Bukhari: 3435; at-Tirmidhi: vol. 1, book 46, no. 3616, fafanuzi imeongezwa). Kwakuwa Kristo "ndiye Roho wake," "Roho" hawezi kutajwa na Gabriel, kwa sababu Kristo siyo malaika Gabriel.

Korani inamtaja malaika Gabriel kwa jina kwenye tukio (angalia **Q. 2:97**). **Q. 16:2; 70:4; 78:38** anatofautisha *"Roho na Malaika."* "Malaika," kwa vyovyote, angeishia na Gabriel. **Q. 17:85** (Hilali-Khan) anatolea taarifa, *"Na watakuuliza (Ee Mohamedi SAW) kulingana na Ruh (Roho); sema: "Roho [Ruh]: ni mmoja wa vitu, ujuzi wa mmoja pekee ambaye ni Bwana wangu. Na kwa ujuzi, wewe (mwanadamu) umepewa kidogo tu."* Kumbuka kwamba Mohamedi *hakumtaja* Roho kama Gabrieli; Badala yake, aliukiri ujinga ulioambatana naye na kuonyesha kwamba Roho ni wa kipekee ndani ya ujuzi wa Bwana. Hicho hufanya Kwamba Roho ni wa Uungu (i.e., Mungu mwenyewe) kwa kuwa ukuu wa Mungu (Allah) hauchunguziki na mwanadamu lakini na Mungu mwenyewe (e.g., **Q. 6:103:** *"Yuko juu ya mafikira yote"*; **Q. 42:11:** *"hakuna chochote mahali popote pale kama Kwake"*). Kwa hiyo, kwa wachambuzi na watafsiri wa Kiislamu kushikilia kwamba Korani inaposema Yesu alipokea "Roho mtakatifu" au "Roho yetu" malaika Gabriel anahusishwa kwa cha kiwango cha yote mawili "maombi maalum" (i.e., ni ubishi wa kijinga ambao unahusisha madai, yasiyo na uthibitisho, kukubaliana kwa ujumla na sheria na kanuni) na "kuomba swali" (i.e., wakiwa na madhanio ya awali kwamba ni kipi ambacho ni lazima kikubalike).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Lakini kulikuwa na sababu zipi zilizomfanya Mungu aingilie mfumo wa asili wa kuzaliwa ili Yesu azaliwe na Mama pekee?" (Gilchrist 2010: 10-11) Sababu pekee ya kuelezeka ni ile iliyotolewa kwenye Biblia ambayo kimsingi *inamtofautisha* Adamu na Yesu: Adamu alitokana na Ardhi, lakini Yesu ni kutoka Mbinguni (**1 Wakor 15:47**); Adamu alikuwa mtu wa kawaida tu, lakini Yesu ni Roho atoaye uzima (**1 Wakor 15:45**); kwa Adamu wote wanakufa, lakini kwa Yesu wote wanahuishwa (**1 Wakor 15:22**). Mungu hakutakiwa kumpulizia pumzi kwa Yesu ili kumpa nafsi "kwa sababu Yesu alikuwa anaishi kwenye ulimwengu wa Kiungu kabla ya kuzaliwa duniani" (Gilchrist 2015: 67). Kwa sababu Yesu alikuwa na umilele ndani yake, "alipaswa kuzaliwa na bikira Mariamu. Hakutakiwa kuumbwa tena kupitia wawili Baba na Mama kama mtu mpya kabisa, kumtofautisha kabisa na wazazi wake, bila kujali vinasaba na DNA" (Ibid.).

Hatimaye, Korani haituambii kwamba Allah alisema "Iwe!" na Yesu aliumbwa. Ni jambo maalum sana kuhusiana na nguvu isiyo ya kawaida iliyowezesha kutunga mimba ya Yesu. **Q. 21:91** inasema*, "Na (kumbuka) yeye [Mariamu] ambaye alikuwa akiulinda ubikira wake: tulimpulizia ndani yake Roho yetu, na kumfanya yeye na mwanae kuwa ishara kwa watu wote."* **Q. 66:12** anaongeza, "*Mariamu binti yake na 'Amramu, aliyeulinda ubikira wake; na tulimpulizia ndani yake (mwilini mwake) Roho yetu; na alishuhudia kwa ukweli wa maneno ya Bwana wake na kwa Ufu wake, na alikuwa miongoni mwa watumishi waaminifu)."*[2] Kulingana na aya hii, Mawdudi anaeleza, "Hili ni kwamba, hakuwahi kuwa na mahusiano na mwanaume yeyote, Allah alipulizia pumzi ndani ya tumbo lake Roho kutoka kwake mwenyewe (A'la Mawdudi n.d.: Q. 66:12n.28).

Kinyume na upekee na nguvu isiyo ya kawaida ya kuwepo kwa Yesu, "Ni uelewa wa kawaida kwamba baba yake na Mohamedi alikuwa Abdallah; na mama yake alikuwa Amina. . . . Alizaliwa kwa njia ya asili kama ambavyo sote tulizaliwa, kutoka kwa Baba na Mama wote wanadamu." (al-Masih 1993: 8) Hata hapa, Korani

---

[2] Matamshi ya Kiarabu ya Korani **Q. 21:91** na **66:12** yapo wazi. Inaonyesha muunganiko wa mahusiano ya *hali ya juu* sana baina ya Allah na Mariamu kuliko hata wengi wa Uislamu wanavyotambua. Hilali-Khan anajaribu kulishusha [kutokulipa uzito]jambo kwa kutafsiri **Q. 21:91** kama, *"Na (kumbuka) ambaye aliyekuwa akiulinda ubikira wake [Bikira Mariamu (Mary)], Tulimpulizia ndani yake (kwenye upindo wa nguo yake)Yeye[mwanamke] (shati au nguo yake). . ."*Walitafsiri **Q. 66:12:***"Na Mariamu (Mary),binti yake na Amramu ambaye alikuwa akiulinda ubikira wake;na Tulimpulizia pumzi ndani yake (upindo wa vazi au nguo yake). . ."* Mumim Salih, Muislamu wa awali, analijadili hili hivi: "Tafsiri ya hapo juu ni uongo mtupu. Neno 'ubikira wake' liko linatumika kama tafsiri ya neno la Kiarabu 'farjaha', ambalo liko mbali sana na ukweli .Kimsingi neno la Kiarabu ni 'farj' linamaanisha viungo vya mwanamke (uke kwa kueleweka zaidi). . . . Waarabu wanamsemea mwanamke mwenye ubikira kwa maneno kama vile 'afifa' au 'sharifa', bila kuwa na sababu kabisa ya kuvitaja viungo vyake vya uke. Tafsiri ya uongo iko wazi pia kwa ushahidi wa matumizi ya neno'kumpulizia pumzi ndani' kama tafsiri ya kiarabu ya neno 'nafakhna feeha', linalomaanisha 'tulileta upepo juu yake (mwanamke)…'. Korani inamaanisha kusema 'kwenye viungo vyake vya uke/uke', lakini mtafsiri anazungumzia kuhusu nguo na shati! Ninafikiri kama tungewauliza watafsiri kwanini wanaleta suala la nguo hapa, majibu yao yangekuwa kwamba mchakato wa kupuliza hufanyika tofauti bila kuwa na cha kumfunua! . . . Korani inazungumzia jambo hilo hilo kwenye surat Al Tahreem (66:12), lakini inatumia neno la kiarabu 'nafakhna feehy' badala ya nafakhna feeha, bila kuacha nafasi yoyote ya kubadilisha maana. Nafakhna feehy linamaanisha 'tulipulizia kwenye viungo vyake (uke)' kuthibitisha mahali ambapo mchakato wa kupulizia ulipofanyikia. Neno sahihi kwa Q.66:12 lilitakiwa kuwa: 'Na Mariamu, binti wa Amramu aliyeulinda uke wake; na tuliupulizia kwa Roho wetu'. Pamoja na ufafanuzi huo,mtafsiri [Hilali-Khan] anasisitiza kwa kuleta suala lisilowazi na dhaifu la vazi, shati na nguo kwenye aya." (Salih 2007: Kumpulizia ndani ya Mariamu!)

Ali na Dirks wanajaribu kuyadhoofisha maelezo ya Biblia juu ya uzazi wa bikira kwa kulilinganisha hili na simulizi ya Kigiriki ya miungu waliomtunga mimba mtu mwanamke. Ali anasema kwamba maelezo ya Korani "haipaswi kuchukulia kwamba Allah alikuwa Baba wa Yesu kwa kile simulizi za kigiriki zinavyomfanya Zeus kuwa baba wa Apollo kwa Latona au kwa Minos kwa Europa. Na bado ndilo fundisho linaloongoza ambalo kwalo mawazo ya Wakristo wanalo juu ya 'mwana mzaliwa pekee wa Mungu." (Ali 2006: Q. 66:12n.5552; angalia pia Dirks 2008: 68 [Wazo la "mwana pekee" . . . ndiyo matokeo ya wale wanaoamini kwenye miungu wengi, e.g., historia ya kuzaliwa kwa Hercules"]) Ali na Dirks, kama Hilali-Khan, wametokea kuwa wapotoshaji waliokusudia. Kwenye maelezo ya Biblia, Gabrieli alieleza kwa Mariamu, *"Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu."* (**Luka 1:35;** angalia pia **Math 1:18-23**). "Hakuna kwenye [maelezo ya Biblia] panapoeleza kwamba kulikuwa na mwingiliano (wa kimapenzi) baina ya Mungu na Mariamu. Maneno *atakujilia juu yako* na *zitakufunika* kwenye mstari wa 35 halihusishi mahusiano ya kujamiiana, na Luka hapa anaelezea kwa neema iliyo kuu tukio ambalo ni Zaidi ya ufahamu wetu." (Schreiner 1989: 806) Kwa namna nyingine, kwenye maelezo ya Korani, Allah hakusema tu kirahisi kwamba "Iwe!" kumwuumba Yesu. Badala yake, Allah alijihusisha moja kwa moja yeye mwenyewe kwenye kumwuumba Yesu na kwa wazi alifanya jukumu la Ubaba. Alipulizia pumzi yake *ndani ya Mariamu* (kwenye uke wake) kwa kusudi la kumzaa Yesu. Hili ni Zaidi sana wazi na la kujamiiana Zaidi ya maelezo ya Biblia. Hili linapunguza maswali ya msingi kwenye **Q. 6:101**, *"Ni jinsi gani Yeye [Allah] atakuwa na mwana wakati hana mwenza?"* kimsingi halina maana. Maelezo ya Korani kweli "yanaeleza kwamba Allah alikuwa Baba wa Yesu." Kama Mungu siyo Baba yake na Yesu, basi yeye ni nani? Kwa kuwa Mungu ni Baba yake na Yesu, hili linamfanya Yesu kuwa "Mwana wa Mungu" kwa njia ambayo ni tofauti sana na wanadamu wengine.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

inamtofautisha Yesu na Mohamedi kwa jinsi walivyowatofautisha Mama zao. Mariamu ametajwa mara 34 kwenye Korani; aliitwa *"mwanamke wa kweli"* (**Q. 5:75**) na *"ishara ya watu wote"* (**Q. 21:91**; angalia pia **23:50**). **Q. 3:42** inaeleza, "*Ee Mariamu! Allah amekuchagua wewe na kukutakasa wewe-alikuchagua wewe juu ya wanawake wote wa mataifa yote.*" Tofauti na Mariamu, Mama yake na Mohamedi hakutajwa hata mara moja kwenye Korani.

B. *Yesu, siyo Mohamedi, ni "Neno" la Mungu*

Q. 3:45 inasema, *"Tazama! Malaika alisema: 'Ee Mariamu! Allah amekupa wewe habari ya furaha ya neno kutoka kwake: jina lake litakuwa Kristo Yesu, mwana wa Mariamu, kuwekwa kwenye heshima ulimwenguni humu na Baadaye kuwa (kufuatana na) na wale wa karibu na Allah'"* (angalia pia **Q. 3:39; 4:171**). Masih anaeleza, "Manabii wote walisikie neno la Mungu na kulielezea kwa ukunjufu. Kama kwa Kristo, Hakulisikia tu neno la kusisimua, Yeye mwenyewe alikuwa mzaliwa wa neno la kiungu." (al-Masih 1993: 10) matamshi ya Kiarabu yanathibitisha hili: "Suala la msingi hapa ni kwamba *Yesu mwenyewe* aliitwa Neno toka kwa Allah – *kalimatim-minhu* – Neno toka *kwake*, na *kalimatuhu* – Neno *lake*. Ni kihusishi *hu* (yeye) kinachotupa cheo na fafanuzi maalum. Neno halikuja kwa Yesu kama yale yaliyokuja kwa manabii kabla yake, *yeye mwenyewe* ni neno lile lililotoka kwa *Allah mwenyewe.*" (Gilchrist 2015: 140-41) Mwanazuoni Muislamu Professor Ayoub anakubali: "Yeye [Yesu] anawakilisha uumbaji maalum; yeye ni neno la Mungu lililoletungwa ndani ya mwanadamu ili liweze kuishi" (Ayoub 1980: 93).[3]

Mohamedi hakuitwa neno lililohai kwenye Korani. D. A. Carson anaelezea kifupi, "Yesu hawakilishwi tu kama mtu aliyeubeba ujumbe wa Baba yake, kama ambavyo Mohamedi anavyowakilishwa kwa Uislamu kama nabii wa mwisho aliyebeba ujumbe wa Allah; badala yake, kwa njia iliyo muhimu, Yesu *ni* ujumbe

[3] Wakati Yesu aliitwa "Neno" la Mungu, baadhi ya Uislamu huongeza neno kwenye **Q. 3:47, 59** na kudai kwamba aliitwa "Neno" kwa sababu, kama uumbaji wa Adamu, Allah alimuumba Yesu kwa neno lake—"Iwe!" (angali Q. 3:45, Hilali-Khan; Ali 2006: Q. 3:59n.398; Q. 4:171n.676; Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 4:171, maoni). Haya siyo sahihi kwa angalau sababu nne:

- Kwanza, "Kama wafafanuzi wangedai kwamba "neno"linamaanisha nini ni kihusishi 'iwe' (*kun*) au msemo kwenye maneno mengine hakuna namna wangeweza kudai maana hiyo kwa suala hilo. Maneno, 'Neno kutoka kwake ambaye jina lake ni Masihi linaonyesha kwamba neno hapa ni mtu na siyo tamko wala amri kama itakavyokuwa wazi kwenye kiashiria rahisi. Ni kama vile kusema, 'Mtu kutoka kwake.' Kumbuka kwamba matamshi ya Kiarabu *ismihi* ('ambaye jina lake') linaashiria mwanaume kwa *kalima* (Neno) likimaanisha mwanamke kwa kiarabu lakini likiwakilisha mwanaume kwenye maana; vinginevyo, kilugha lisingeruhusiwa kutumika." (Ghabril 2003: 31) Hadithi inathibitisha hili. Kwenye *Sahih al-Bukhari* (vol. 6, book 60, no. 236) Yesu aliitwa "Neno lake [Allah's] lililotumwa kwa Mariamu." Rick Brown analiweka kwa njia hii, "Matumizi kwenye Korani yapo wazi kwamba ni Mungu kwenye mwili, na Yohana mbatizaji aliitwa kupeleka ushahidi kwa Yesu kama neno (3:39, 45; 4:171). Kumbuka kwamba ingawa *kalima* 'neno' ni mwanamke kwa Kiarabu, limewekwa kwenye aya hii kama mwanaume, hata kabla ya kuasisiwa, kama 'neno toka kwa Mungu, jina lake ni Yesu.'" (Brown 2002: 27n.2)
- Pili, Makosa ya majadiliano ya Uislamu yanasababisha matokeo. Ghabril anaelezea, "Kama Mungu alimuumba Isa, yaani Kristo, kwa neno la amri (*kun*, kwa kiarabu) kama wanavyodai, asingeitwa (*kalima*) neno, kwa sababu siyo neno lakini ni matokeo ya neno (amri). Kama nikiandika kitabu kwa mawazo yangu, kitabu hicho hakiitwi mawazo (au mawazo yangu) Makala ya mawazo. Vinginevyo, ukweli utachanganywa na makosa, na mambo muhimu yatachanganywa na mambo ya dharura." (Ghabril 2003: 31) "Neno" wazi ni Yesu, i.e., kitu kilichohamishwa kwenda kwa mpokeaji, kwa sababu **Q. 4:171** inasema kwamba neno *"lilipokelewa kwa Mariamu"* (Ali; Hilali-Khan) au *"lilipelekwa kwa Mariamu"* (Sarwar; Pickthall [*"lilipelekwa ndani"*]).
- Tatu, Sundiata anaonyesha, "Neno la Mungu au la mtu mwingine yeyote, lililonenwa, andikwa, au kuelezewa kwa ishara fulani, ni maelezo ya mawazo. Kwa kuwa ni Yesu pekee aliyeitwa 'Neno la Mungu' kwenye Korani, inafuatia kwamba Korani inamheshimu Yesu pekee kama Maelekezo ya Kimungu, ambacho ndicho hasa Mtume Paulo alichokieleza kwa Wakolosai kwenye Biblia (Wakol. 2:9)." (Sundiata 2006: 204)
- Nne, ingawa Adamu aliumbwa kutoka kwenye mavumbi hana mzazi wa kimwili, Korani kamwe haikuwahi kumwita yeye "Neno" la Allah kama ilivyomwita Yesu. Kwa hiyo, kumwita Yesu "Neno" la Mungu, lakini siyo sawa na kumwita Adamu "Neno," haitakuwa njia rahisi kuelezea nguvu isiyo ya kawaida kwenye hali ya kutungwa iliyomleta Yesu, lakini kwa kweli, ni njia ya *kumtofautisha* Yesu na Adamu bila kujali namna walivyozaliwa au kuja duniani.

Kwa sababu Korani yenyewe haielezei au kufafanua *maana* ya Yesu kama "Neno,"maana hiyo yaweza kutokana na Biblia pekee ambayo awali ilimwelezea Yesu kama"Neno." Yesu hapo mwanzo alielezewa kama "Neno" kwenye **Yohana 1:1, 14**: *"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. . . . Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli"* (angalia pia **Ufu 19:13**). Kuipa historia hii, maana pekee yenye sababu ya Yesu kama"Neno" kwenye Korani ni kwamba Yesu ni mzaliwa wa neno la Kiungu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wenyewe, Yeye *ni* Neno, kama vile anavyolibeba" (Carson 2008: 53).

C. *Yesu, siyo Mohamedi, ni "Roho" toka kwa Mungu*

Q. 4:171 Inamwita Yesu "*Roho atokaye Kwake [i.e., Allah].*" Gilchrist anakumbusha, "Yesu siyo tu Neno *kutoka* kwa Allah, pia ni Roho *atokaye* kwa Allah. Maneno hayo hayo ya Kiarabu yametumika – *min-hu* – 'kutoka kwake'. Hakuna Nabii mwingine aliyepewa cheo hicho kwenye Korani au aliyeambiwa *ametoka* kwa Allah. . . . Wengine wanasema Korani inazungumza kuhusiana na Roho ya uzima aliyopuliziwa Yesu wakati wa alipozaliwa na bikira mwanamke. . . . Sura 4.171, hata hivyo, inasema kwamba Yesu mwenyewe ni Roho kutoka kwa Allah, siyo kwamba alipokea Rohokutoka kwake. Kuna mfanano wa milele kati yao wawili." (Gilchrist 2015: 144, 145)

Kwenye Hadithi, Mohamedi mwenyewe alisema moja ya kweli ambazo mtu apaswa kuzijua ili aingie Paradiso ni kwamba Krisyo ni "*Neno lake* ambalo lilinenwa kwa Mariamu *na Roho wake*" (Muslim: 28a; angalia pia al-Bukhari: 3435; at-Tirmidhi: vol. 1, book 46, no. 3616, fafanuzi imeongezwa). Hakuna madai kama haya kwenye Korani yaliyodaiwa kwa Mohamedi.

D. *Yesu, siyo Mohamedi, ni "Masihi"*

Kwenye matukio mbalimbali, Korani inamtaja Yesu kama "Masihi" (**Q. 3:45; 4:157, 171-72; 5:72, 75; 9:30**; Kiarabu ni "al-Masih"). Memsuah Mansoor anaeleza, "Neno la Kiarabu, 'masih' limetofautiana na 'mamsuah' na kwamba 'mamsuah' kifupi inamaanisha 'mpakwa mafuta' na likimaanisha kupakwa mafuta kidogo. 'Masih' hata hivyo, ina msingi wa umbo la kisarufi inayoeleza ukweli wa kupakwa mafuta kunakomilikiwa na mtu Fulani au kitu fulani. Ni kwenye 'umbo la kumaanisha' ambapo mara nyingi inaashiria 'kiwango cha hali ya juu cha ubora ambao una umiliki wake au tendo ambalo hufanyika mfululizo ... kwa mfumo wake.'" (Mansoor n.d.: n.p.)

Al-Masih "ni kiambishi cheo kwa jina la kila nabii kwenye Korani. . . . [Hili linaashiria] kwamba kulikuwa na kitu cha kipekee kumhusu Yesu, kwamba alikuwa ameinuliwa Zaidi ya manabii wote wa Allah." (Gilchrist 2015: 121, 123) Ingawa Yesu alipewa cheo cha "al-Masih," maana ya neno hili au umaalum wa 'kupakwa kwake mafuta' halijafafanuliwa wala kuelezewa. Maelezo ya Yesu kama "Masihi" (al-Masih), wazi wazi linatokana na Biblia, kwakuwa "Kristo" (Kigiriki = *Christos*) ni kigiriki sawa na Kiebrania"Masihi" (Danker 2000: *Christos,* 1091), na "Kikorani *al-Masihu 'Isa* kifupi tafsiri ya Kiarabu kwa jina na cheo hicho hicho, likimaanisha kwa usahihi 'Kristo Yesu' au kwa uhalisia zaidi 'Yesu Masihi.' Hili linaeleza ni kwa sababu gani Korani haijaribu kuelezea cheo – kinatumika pamoja na jina Yesu ni la kawaida sana miongoni mwa Wakristo na kiufupi linakubalika na kulikiri." (Gilchrist 2015: 124)

Muislamu Professor Abdul-Mohsin anakiri kwamba "Wayahudi walikuwa wanamtarajia Masihi kuja moja kwa moja kati ya makundi haya matatu: 1. Mfalme [nukuliwa kwenye **Yer 23:5-6; Zab 110:1-2**]. 2. Kuhani [nukuliwa kwenye **Zek 6:12-13; Zab 110:3-4**]. 3. Nabii [nukuliwa kwenye **Kumb 18:18-19**]." (Abdul-Mohsin 2006: 95-97) Kiumuhimu, Masihi asingeweza kuwa "mfalme tu" lakini alikuwa awe "Mfalme"— Mfalme wa *mwisho* wa Ulimwengu. Louis Jacobs aliandika kwenye *Maktaba maalum ya Wayahudi* akasema, "Kwenye mawazo ya kiualimu, Masihi ni mfalme atakayewaokoa na kuwatawala Israel kwenye kilele cha historia ya mwanadamu na vyombo ambavyo Ufalme wa Mungu utaanzisha. Wakati Biblia inasisitiza asili ya wakati ikiuita 'mwisho wa siku,' waalimu wanaliangalia kama ushauri wao, ambao walitoa umri wa Umasihi (*yemot ha-mashi'aḥ*) na kuutaja." (Jacobs 2008: Masihi kwenye mawazo ya kiualimu) Mistari mingi ya Agano la kale inaashiria kwamba Masihi atakuwa mwanadamu (e.g., **Mwanzo 3:15; Isa 11: 1-5; 42:1-6; 59:20; Yer 30:18-22; 33:14-15**); hata hivyo, mistari mingine inasisitiza kwamba Masihi atakuwa wa Kiungu (e.g., **Zab 2:6-12; 110:1-7; Isa 9:6; Yer 23:5-6; Mika 5:2; Zek 14:9**).

Agano Jipya kwa uwazi linaonyesha kwambaYesu Kristo alitimiza tarajio la Waisraeli la Mfalme na Mwokozi aliyetumwa na Mungu (angalia e.g., **Math 2:4-11; 16:16, 20; 22:42-45; 26:63-64; Marko 8:29; 12:35-37; 14:61-62; Luka 4:41; 20:41-44; 22:67-70; 23:2-3, 39; 24:26, 46; Yohana 4:25-26; 11:25-27; 20:30-31; Matendo 2:30-36; 9:22; 17:3; 18:5, 28; 1 Yohana 2:22; 5:1**). Yesu alikuwa Mfalme aliyetabiriwa. Hili lilitambulika wakati wa mwanzo wa huduma yake (**Yohana 1:49,***" Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli"*) na wakati Yesu alipoingia Yerusalemu wakati wa mwisho, ambapo Injili zote nne zinatafsiri kama ujio wa kinabii wa ufalme wa Daudi (**Math 21:1-11; Marko 11:1-11; Luka 19:28-40; Yohana 12:12-16**). Yesu pia ni Kuhani mkuu mkamilifu kwenye hekalu la kweli (**Waeb 2:17; 4:14-5:10; 7:1-8:6; 10:11-22**). Hatimaye Yesu anakamilisha unabii wa Musa kwamba Mungu atamwinua nabii mwingine kama yeye (angalia **Kumb 18:15, 18-19; Yohana 1:45; 6:14; Matendo 3:20-23**).

Kwa sababu Yesu ndiye "Masihi," na Masihi ni wa mwisho, nabii wa nyakati za mwisho, Kuhani, na Mfalme, Mohamedi asingeweza kuwa nabii wa"mwisho", kwa kuwa jukumu hilo la kipekee lilikamilishwa na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Masihi, i.e., Yesu.[4] Kwa kuwa hata Korani inatambua kwamba Yesu ni "Masihi," maana ya neno hili yaweza kuwa maana ile ambayo *Yesu mwenyewe aliyoimaanisha.* Maana hiyo yaweza kupatikana tu kwenye Agano Jipya, kwa sababu Agano Jipya pekee limeandika kwa kina kile Yesu alichokisema na kukifanya kutuongoza kwenye (yasiyotarajiwa) hitimisho ambalo kwamba kwa hakika alikuwa, Masihi. Kwa sababu Korani inatumia msamiati wa Kibiblia ("Masihi") na kusema kwa urahisi kuthibitisha ufunuo wa awali (**Q. 2:41, 89, 97; 3:3; 4:47; 5:15, 48; 6:90, 92; 10:37; 12:111; 35:31; 46:9, 12,** 30), kwa sababu inasema kwamba *"Tunaamini katika kile . . . alichopewa Musa, 'Yesu na manabii kutoka kwa Bwana wao"* (**Q. 2:136**, Hilali-Khan), ni Lazima kwa hilo kuukubali ufunuo wa Biblia wa *kile* "Masihi" anachomaanisha na *kwanini* Yesu ni Masihi—na kwamba inajumuisha kwamba Yesu ni Mungu, kwa kuwa sehemu ya maelezo ya Masihi kwenye Biblia ni kwamba Yeye ni Mungu.

Kunao ukweli mwingine Zaidi wa Korani kumwita Yesu "the" Masihi (al-Masih): "Kiarabu, neno "*al* " wakati wote lina maana sawa na neno la kiingereza '*the*' na linahusishwa kwenye jina ambalo linamtaja Mungu pekee yake. Hii ndiyo sababu majina yote 99 ya Allah yanaanza na neno *Al au The*. Hata hivyo ikumbukwe kwamba, neno *The* siyo sehemu ya jina. Ni kihusishi kinachotumika kuashiria kwamba neno hilo ni la kipekee kwa Mungu—Mungu pekee ndiye apewaye daraja hilo. Kwa mfano, hatuwezi kumtaja Mohamedi kwa kuanza na kihusishi, 'The Mohamedi,' kwa sababu Mohamedi ni jina tu la mtu fulani. Ni jambo la kufurahisha kugundua kwamba Masihi kwenye Korani anaitwa Al-Maseeh. Likimaanisha kwamba Yeye pekee ndiye Masihi duniani kote. Ndiye mtu pekee kwenye Korani ambaye kihusishi cha *Al* au *The* kimefungamanishwa na jina lake." (Prince 2011: 5; angalia pia Mansoor n.d.: n.p.)[5] Korani haikumtaja Mohamedi wala nabii mwingine yeyote kama "masih," awe pekee "al-Masih."

E. ***Yesu, siyo Mohamedi, asiye na waa, mtakatifu, na asiye na dhambi wala kosa toka alipozaliwa***

Korani inatuambia kwamba Adamu hakumheshimu Mungu (**Q. 20:116-21**); Musa alimwua Mmisri (**Q. 28:15-16**); Daudi alifanya hukumu ya haraka au alitaka Mume wa Bethsheba auawe ili yeye amwoe Bethsheba (**Q. 38:21-24**);[6] Wengi wa manabii waliomba msamaha kwa ajili ya dhambi zao: Nuhu (**Q. 11:47; 71:28**), Ibrahimu (**Q. 14:41; 26:82**), Sulemani (**38:30-35**); Mohamedi mwenyewe alikemewa na Allah na kuhitajika kuomba msamaha kwa dhambi zake wakati uliopita na ujao (**Q. 8:67-68; 9:43; 40:55; 47:19; 48:1-2**; angalia Abdul-Mohsin 2006: 69-75; Ghabril 2003: 13-20; na angalia hapo chini kuhusiana na Mohamedi). Maneno yaliyotumika kwenye mtiririko huu ni maneno ya kawaida ya Kiarabu "ambayo kwenye Korani yametumika kote kwa maana ya kuomba msamaha zilizofanywa kinyume na Mungu [siyo "makosa" yasiyo ya msingi' au 'makosa kwenye kutoa hukumu']" (Gilchrist 2015: 72-75).

Yesu pekee alikuwa tofauti. Ingawa Korani imeorodhesha dhambi za manabii wengine ikiwa ni pamoja na Mohamedi, Hakuna dhambi iliyoorodheshwa ya Yesu kwa sababu hakutenda. Abbas Sundiata anaangalia matokeo haya muhimu: "Hata pale tunapokuwa hatujatenda dhambi, tunabaki kuwa wenye dhambi—ni urithi

[4] Mohamedi alisema, "Kati ya watu wasiostahili mbele za macho ya Allah Siku ile ya Ufufuo na mtu mbaya ambaye ni mlengwa wa hasira yake atakuwa mtu yule aliyeitwa (Malik al-Amlak) Mfalme wa Wafalme kwa kuwa hakuna Mfalme isipokuwa Allah" (Muslim: 2143a; angalia pia al-Bukhari: 6205, 6206; at-Tirmidhi: vol. 5, book 41, no. 2837). Kwa maneno mengine, msemo "Mfalme wa Wafalme" linamaanisha kwamba mtu huyo ni Mungu mwenyewe. Hata hivyo, kwenye Biblia Yesu anaitwa *"Mfalme wa Wafalme"* (**1 Tim 6:15; Ufu 17:14**). Zaidi, kwa kuunganishwa na ujio wa pili wa Yesu hapa ulimwenguni, **Ufu 19:16** inaarifu kwamba *"Naye ana jina limeandikwa kwenye vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME, NA Bwana WA MABwana."* Kwa kuwa "hakuna Mfalme mwingine isipokuwa Allah," na Allah anasema "Mimi ni Mfalme" na kuwadhihaki hao wanaojiita wenyewe "wafalme" (al-Bukhari: vol. 6, book 60, no. 336; angalia pia al-Bukhari: 6519, 7382), Kwahiyo basi, Yesu ni lazima *awe* Mungu na Mfalme kwa sababu aliitwa "Mfalme wa Wafalme" na kwenye vazi lake na paja *alijiita mwenyewe* "Mfalme wa Wafalime"; bado, kulingana na Uislamu, Yesu *siyo* mlengwa wa hasira ya Allah lakini yuko hai na yupo mbinguni!

[5] Kwenye kujaribu kumdidimiza Yesu kuwa kama manabii wengine, Deedat anasema kwamba neno la Kigiriki *christos* linamaanisha "mpakwa mafuta" na kwamba watu wengi kwenye Biblia wanasemekana kuwa wapakwa mafuta (Deedat 2002: 13-14). Wakati huo huo ni ukweli kama ambavyo inaendelea, Deedat ameondoa ukweli uliodhahiri: "Cheo alichopewa Yesu kwenye Biblia ni Kweli (kwenye asili ya kigiriki) *ho Christos*, kwamba ni, ('the Christ') Kristo. Matumizi ya kweli ya Makala yanakizungumzia cheo hicho kwenye hali inayofunua kwamba kwa kweli Yesu alikuwa *Masihi (the Messiah*), Mpakwa mafuta wa Mungu, kwa njia ambayo hakuna nabii mwingine aliyekuwa." (Gilchrist 2010: 8)

[6] Baadhi ya Wachambuzi wa Kiislamu hukataa kwamba tukio hili linahusiana na Bathsheba na Uriah, lakini hudai kwamba Daudi alitoa hukumu ambayo msingi wake uliegemea kusikia toka kwenye simulizi ya mlalamikaji mmoja tu (angalia Ali 2006: Q. 38:24n.4176-A, Q. 38:26n.4178). Wengine, inaonekana wakijumuishwa na wachambuzi wa awali, huhusisha hili na maelezo ya Kibiblia ya Daudi, Bathsheba, na Uriah. Hata hivyo, wanakataa kwamba Daudi hakuzini pamoja na Bathsheba lakini husema kwamba Daudi alimwona tu, akahisi kumpenda, na kuhakikisha kwamba Uriah anauawa vitani ili kwamba aweze kumuoa. (angalia maoni ya Asad 1980: Q. 38:21n.22; Jalal 2017: Q. 38: 22, 24)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

wetu kama wanadamu. Tofauti na sisi, Mungu hana hisia hizo. Kwa hiyo, kama Mungu aliishi kati ya wanadamu kama mwanadamu, kitu kimoja ambacho kitavutia hisia zetu kwake na kumtofautisha Yeye na wengine ni maisha yake makamilifu ambayo atayaishi, kwa sababu Mungu hatatenda dhambi." (Sundiata 2006: 201) **Q. 19:19** anasema malaika walimtangazia Mariamu kwamba, ingawa alikuwa bikira, atapewa "*mwana mtakatifu*" (Ali), "*mwana mtakatifu sana*" (Pickthall), "*mwana mwenye haki*" (Hilali-Khan), "*kijana asiye na waa*" (Arberry; angalia pia Sahih, Shakir, Sarwar, Haleem). "Malaika walikuwa wawazi kumwambia kwamba atapata mimba kwa njia *maalum* sana kwa sababu tu kuna kitu *maalum sana* kwa mtoto atakayemzaa" (Gilchrist 2015: 46). Abd al-Masih anaeleza, "Mwanazuoni wa Kiislamu al-Tabari, al-Baidawi, na al-Zamakhshari alikubali kwamba maelezo 'mtakatifu sana' inamaanisha asiyelaumika, asiyeshtakiwa na dhamira na asiyetenda dhambi. Kabla Kristo hajazaliwa, Uvuvio wa Kimungu ulitangaza kwamba huyo atakayekuja kuzaliwa, atazaliwa kwa Roho wa Mungu na wakati wote ataishi akiwa mkamilifu, bila dhambi kabisa. Hakuna hitaji la kuutakasa moyo wake, kwa kuwa alikuwa mtakatifu yeye mwenyewe. Mwana wa Mariamu hakulisikia neno la Mungu pekee yake; Alikuwa hilo neno. Hapakuwa na tofauti kati ya Matendo yake na Maneno yake. Alibaki kuwa asiyelaumiwa na asiye na dhambi." (al-Masih 1993: 13) Mawdudi anahitimisha, "Mungu alimzawadia Yesu Nafsi iliyo safi na isiyo na hatia. Kwa hiyo alivikwa mwili wa kweli, uhakika , haki, na ubora." (A'la Mawdudi n.d.: Q. 4:171n.213) Upekee wa Yesu umeelezewa na Mwanazuoni Muislamu Professor Mahmoud Ayoub: "Kwa hiyo Yesu hakuwa na waa la uovu uwao wowote wala hakujichafua. . . . Usafi huu, ambao Adamu alikuwa nao hadi hapo alipoguswa na kidole cha shetani na hivyo akaupoteza, sasa umebaki kudhihirishwa na Yesu pekee." (Ayoub 1980: 93)

Tofauti na Yesu, "Nabii [Mohamedi] mara chache amekuwa hata akihukumiwa kwenye Korani" (Haleem 2005: xv). In **Q. 8:67-68** Mohamedi alikemewa kwa kupokea sadaka toka kwa wafungwa waliochukuliwa kwenye vita vya Badr mwaka 624 CE. In **Q. 9:43** Mohamedi alishtakiwa kwa kuwaruhusu baadhi ya wapiganaji wake kubaki kabla ya vita vya Tabuk mwaka 631 CE. In **Q. 66:1** (Sarwar) Mohamedi alikemewa kwa *"kuviharamisha vile ambavyo Mungu aliviruhusu vitumike."* Mara mbili kwenye Korani, **Q. 40:55** na **47:19**, Mohamedi aliagizwa "*kuomba msamaha kwa kosa lake"* (angalia pia **Q. 110:3**).Tafsiri ya Arberry, Shahih, Pickthall, Sarwar, na Haleem **Q. 40:55** kama "*kwa dhambi zako.*" John Gilchrist anaonyesha kwamba kwenye aya ya **47:19** neno la Kiarabu kwa *omba msamaha kwa dhambi zako"* ni *wastaghfir lithanbik* "ambalo ni sawasawa kwa uhakika kama neno lililotumika wakati Zulaykah (Jina la kiislamu la mke wa Potifa) alipoamriwa kutubu kwa tamaa yake ya kutaka (kumpotosha) kumtongoza Yusufu[kwenye **Q. 12:29**]" (Gilchrist 2002: 48). **Q. 48:1-2** inathibitisha kwamba Mohamedi alitenda dhambi (au "makosa") kabla na baada ya kuitwa kama nabii.

Mohamedi mwenyewe alikiri kutenda dhambi na kumwomba msamaha kwa Allah kwa dhambi zake. Mwisho wa moja ya maombi yake alisema, "Ee Allah, kwako nauelekeza moyo wangu, kwako mashaka yangu, na mbele zako naleta hoja zangu, hivyo *nisamehe dhambi za awali na zile za baadaye, za dhambi za siri na zile zilizo wazi*" (Abi Dawud: 771, fafanuzi imeongezwa; angalia pia Abi Dawud: 760, 761). Hadithi nyingine imeandika, "Wakati nabii akihitimisha maombi yake, alikuwa akitumia maneno haya: 'Ee Allah, nisamehe mimi dhambi zangu za awali na za baadaye, nilizozifanya kwa siri na zile nilizozifanya wazi wazi, na zile nilizozifanya kwenye starehe zangu; na zile uzijuazo vema kuliko mimi.'" (Abi Dawud: 1509) Alikiri pia makosa, ujinga, upotovu, kumaanisha na dhambi zile nilizofanya kwa kukusudia (Muslim: 2719a). Kwa kweli, Hadithi zingine zinaandika kwamba Mohamedi alikiri kwamba alikuwa anatubu *mara mia moja kwa siku!* "Mjumbe wa Allah (saas) alisema: 'Ninatafuta msamaha kwa Allah na kutubu kwake mara mia moja kwa kila siku'" (Ibn Majah: 3815; angalia pia al-Bukhari: 6307; Ibn Majah: 3814; at-Tirmidhi: 3434; Muslim: 2702a, 2702b; Abi Dawud: 1516). Kweli, neno la mwisho mke wake Aisha alilolisikia kabla ya Mohamedi kufa alimsikia akimwomba Allah msamaha: "Wakati Nabii alipokuwa mgonjwa kwa ugonjwa ambao ulikuwa ndo mwisho wake, Nilichukuwa mkono wake nikaufuta mwili wake kurudia maneno haya. Aliuondoa mkono wake kutoka kwangu nakusema: '*Ee Allah, nisamehe mimi* na uniruhusu kukutana na kundi la wale watakaoinuliwa (i.e., wale ambao watamiliki nafasi za juu kule Paradiso).' Hayo ndiyo maneno yake ya mwisho niliyoyasikia." (Ibn Majah: vol. 1, book 6, no. 1619, fafanuzi imeongezwa)

Kwa kweli, Mohamedi hakuwa na hakika kama Allah angemsamehe. Kulingana na **Q. 33:56** (Sarwar; angalia pia Hilali-Khan), *"malaika walimwombea msamaha,"* na waumini hali kadhalika wanatakiwa *"kumwombea Nabii."* Kwamba malaika wanamwombea msamaha na waumini nao wanapaswa kumwombea hii yawezekana kumaanisha kwamba, hata ilivyo kwa sasa, Mohamedi *bado* hajasamehewa. Hakika, kwenye **Q. 46:9** Mohamedi mwenyewe alikiri kwamba hakuwa na uhakika wa wokovu, "*Hata mimi sijui kitakachofanyika kwangu au kitakachofanyika kwenu.*" Hadithi inalithibitisha. Mohamedi alisema, "Kwa Allah, ingawa Mimi ni mjumbe wake, Mimi wala sijui kitakachofanyika kwangu, wala kwenu" (al-Bukhari: 7018; angalia pia 1243, 3929).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Kunayo matokeo muhimu ya ukweli kwamba hata Korani inatambua kwamba ni Yesu pekee asiye na dhambi wala makosa: "Kama Yesu Kristo ni mwanadamu wa kawaida na bado ni mkamilifu, inaonyesha kwamba Mungu kwa kusudi kamili alimpa Yesu nguvu ya kushinda dhambi na uovu lakini akatuacha sisi wengine wote kugaagaa dhambini. Lakini kwanini Mungu alimpa Yesu pekee nguvu ya kushinda dhambi na uovu? Hataki wanadamu wengine wote waishi bila dhambi, au Yeye hana nguvu za kutosha kutufanya sote kuishi kama Yesu alivyofanya? Kama Mungu anataka sisi tuishi kama Yesu, basi itakuwepo sababu ya msingi kwanini wote waliotokea kama wanadamu, Yesu pekee alikuwa na nguvu ya kuishi bila kulaumiwa. Hivyo, pia Mungu alimpa Yesu, mwanadamu wa kawaida nguvu maalum ya kushinda dhambi na kwa makusudi akatuacha sisi wengine wote kugaagaa dhambini, au Yesu Kristo hakuwa na dhambi na mkamilifu mahali pa kwanza kwa sababu kimsingi ni tofauti na wanadamu wengine wote. Ukamilifu wa Yesu ulikuwa ni matokeo ya asili yake ya Uungu badala ya kwamba ni matokeo ya jinsi ambavyo Mungu alimtendea kwa uadilifu." (Sundiata 2006: 201-02)

Ukweli kwamba Yesu alikuwa safi na asiye na dhambi wakati ambao Mohamedi alikuwa mwenye dhambi za lazima pia inamaanisha kwamba "mfano wa Yesu, ulioelezwa kwenye Korani, ni mkamilifu na bora kuliko mfano wa Mohamedi. Kwa namna nyingine hili linaibua mambo mengine mawili, ambayo yanastahili kuangaliwa. La kwanza, Yesu kama kielelezo kikamilifu kamwe hatamshauri mtu kufuata kielelezo kisicho kamili. Pili, Yesu kamwe hatakubali huduma yake iliyokamilifu kufuatiwa na huduma isiyo sawasawa, hasa pale inapokuwa haieleweki kuhusiana na wokovu. Kwa hiyo, madai ya Mohamedi kwamba yeye mwenyewe ndiye muhuri manabii (Nabii wa mwisho) ni kinyume na sifa za hali ya juu ambazo Korani imemsifia Yesu miongoni mwa manabii wengine wote, ikiwa ni pamoja na Mohamedi mwenyewe." (Shayesteh 2004: 191-92)

F. ***Yesu, siyo Mohamedi, aliyelindwa kutokana na ushawishi wa Shetani***

Q. 3:36 inataarifu kwamba, baada ya kujifungua, Mama yake na Mariamu alimwambia Allah, *"Nimemwita Mariamu, na ninamnenea mema yeye na uzao wake kwa ulinzi wako kutokana na yule mwovu,aliyekataliwa."* Mohamedi mwenyewe alithibitisha kwamba Yesu hakuguswa na Shetani, tofauti na mtu mwingine yeyote (ikiwa ni pamoja na Mohamedi mwenyewe). Kulingana na Hadithi. "Nabii alisema, 'Wakati mwanadamu yeyote anapozaliwa, Shetani humgusa pande zote za mwili wake kwa vidole vyake viwili, isipokuwa Yesu, Mwana wa Mariamu, ambaye Shetani alijaribu kumgusa lakini alishindwa, kwakuwa aligusa kondo la nyuma badala yake.'" (al-Bukhari: 3286; angalia pia 3431; Muslim: 2366a, c)

Hakuna mahali popote kwenye Korani au kwenye hadithi panaposema kwamba Allah alimlinda Mohamedi na kutokana na ushawishi wa shetani. Kwa kweli, hadithi zinasimulia kwamba Shetani alimwingia Mohamedi: "Anas b. Malik anataarifu kwamba Gabriel alikuja kwa Mjumbe wa Allah wakati akicheza na wachezaji wenzake. Alimtazama na akamlaza kwa mgongo ardhini alifungua kifua chake na akautoa moyo wake na baadaye aliondoa mabaki ya damu moyoni na kusema: Hii ni sehemu ya Shetani ndani yako. Na akauosha kwa maji ya Zamzam kwenye beseni la dhahabu na kisha akauunganisha tena na kuurudisha mahali pake." (Muslim: 162c, 163; angalia pia al-Tabari 1999: 275-82)

- Aya za Kishetani. Kuoshwa kwa maji ya Zamzam hakukuuhitimisha ushawishi wa Shetani kwa Mohamedi. *Tafsir al-Jalalayn* anaarifu kwamba Shetani alizungumza na Mohamedi na kumsababisha kuisifu miungu mitatu iliyokuwa ikiabudiwa na kabila la Quraysh: "Wakati yeye [Mohamedi] aliposimulia [maandiko] Shetani alimtupia kwenye simulizi zake, kile ambacho hakikuwa kwenyewe Korani, lakini ambayo kwa wale ambao yeye [nabii] atawatuma watapata upendeleo kwa watu. Nabii (Ma) wakati wa kusanyiko la watu wa Quraysh, baada ya kusimulia [aya zifuatazo kutoka sūrat al-Najm, Ulishaangalia Lāt na 'Uzzā? Na Manāt, watatu huyo? iliongezwa, kama matokeo ya Shetani kulitupia neno hilo ulimini pasipo nabii kulijua neno hilo, [maneno yafuatayo]: 'hayo ni magurudumu yarukayo juu (al-gharānīq al-'ulā) na kweli maombi yao ni ya kutegemewa', na hivyo wao [wanaume wa Quraysh] kwa hilo walifurahishwa." (Jalal 2017: Q. 22:52, maoni) Zile ziitwazo "Aya za Shetani" (**Q. 53:19-23**). Ibn Ishaq (c. 704-767), mmoja wa waandishi wa kwanza wa Mohamedi, alitaarifu kwamba baada ya Mohamedi kuisifu miungu mitatu, aliwasababisha watu wengine kuisujudia: "Wakati alipolifikia lile neno lake 'Uliwahi kufikiri kuhusual-Lat na al-'Uzza na Manat watatu, wengine', Shetani, wakati akitafakari juu ya hilo, na kutamani kukileta (*sc.* kwenye usuluhisho) kwa watu wake, aliweka kwenye ulimi wake 'wameinuliwa hawa Gharaniq ambao maombi yao yalikubaliwa.' Wakati WaQuraysh walivyosikia hayo, walifurahi sana kwa jinsi ambavyo alivyoisifu miungu yao na wakamsikiliza; wakati waumini wakiamini kwamba kile ambacho nabii wao aliwaletea kutoka kwa Bwana wao ni cha kweli, bila kuchunguza makosa au tamaa za mtu binafsi, na mwisho walipohitimisha walisujudu na mwisho wa sura ambapo alisujudu mwenyewe Waislamu husujudu wenyewe wakati nabii wao anaposujudu kuthibitisha kile alichowaletea na kutii maamrisho yake, na wale waabuduo miungu wengi WaQuraysh na wengine waliokuwepo msikitini

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

walisujudu wakati waliposikia miungu yao ikitajwa, hivyo wote waliokuwa msikitini waamini na wasioamini walisujudu." (Ibn Ishaq 1955: 165-66; angalia pia al-Bukhari: 1070, 3972, vol. 6, book 60, no. 385; Muslim: 576 kuhusiana na Mohamedi na wapagani wote wanasujudu wenyewe) kwa maneno mengine, Mohamedi hawezi kueleza tofauti baina ya maneno ya Allah na yale ya Shetani.

Ipo maana ya muhimu sana kwa kweli zilizo hapo juu. **Q. 15:42-43** inasema, *"Huna mamlaka juu ya watumishi Wangu wewe [Iblisi; Shetani], isipokuwa wale watakaojiweka wenyewe kwenye makosa na kukufuata wewe.Na hakika, Kuzimu imeahidiwa kuwa nyumba yao wote!"* (angalia pia **Q. 16:98-100; 22:53; 38:82-83**) Inatupa ukweli kwamba Mohamedi hawezi kutueleza tofauti iliyopo kati ya maneno ya Shetani na yale ya Allah, Mohamedi hawezi kuwa mtumishi mwadilifu aliyetakaswa kwa neema ya Mungu au kuwa Nabii wa kweli wa Mungu.

- Mohamedi alikiri kuwa alilaaniwa. Mke wa Mohamedi mwenyewe Aisha alielezea kwamba Mohamedi hakuwa na ulinzi juu ya nguvu za Shetani. Aisha alisimulia, "Wakati nabii alipologwa alianza kuona kuwa anafanya vitu ambavyo kwa kweli hakupaswa kuvifanya" (al-Bukhari: 3175; angalia pia 3268, 6391). Kwa kweli, Mohamedi alikuwa chini ya laana ya Shetani, au uchawi, au kwenye hali ya kukosa fahamu, au ukichaa, ilikuwa ni ngumu kiasi kwamba angeweza kuona amelala na wake zake kumbe wala haukuwa nao! Aisha alishuhudia tena, "Kipindi hicho kiliendelea sana akiona kwamba amelala na wake zake (akijamiiana nao), na kwakweli hakufanya hivyo" (al-Bukhari: 6063). Kwenye hadithi hiyo, mashuhuda wawili walihitimisha kwamba Mohamedi alikuwa "chini ya madhara ya kichawi" (hali ya kichawi "ngozi na mbelewele za mti dume ukiwa na chanuo na nywele zilizoshikamana nalo, zikiwa zimewekwa chini ya jiwe kwenye kisima cha Dharwan"); Mohamedi mwenyewe alihitimisha, "Allah amenilaani mimi" (Ibid.). Mpagani aliyeona na kumsikia, alihitimisha kwa kusema kwamba Mohamedi alikuwa kichaa au aliyepagawa na mapepo (**Q. 23:70; 25:8; 37:36; 44:14; 68:51**).
- Asili ya kifo cha Mohamedi. **Q. 69:44-47** (Hilali-Khan) anasema, *"Na kama yeye (Mohamedi SAW) alitukaririsha misemo ya uongo (Allah swt), Kwa kweli tutamkamata mkono wake wa kuume (au kwa nguvu na uweza), na basi kwa hakika tutakata mishipa ya uhai wake (Aorta), na hakuna mtu atakayetuzuia sisi kumwadhibu yeye"* Hadithi inaeleza, "Wakati Khaibar ilipomilikishwa, kondoo (aliyepikwa) aliyetiliwa sumu, alitolewa kama zawadi kwa Mtume wa Allah" (al-Bukhari: 4249; angalia pia 2617; Muslim: 2190a; Abi Dawud: 4509). Hadithi nyingine inaelezea, "Aisha anasimulia: Nabii kwenye hali ya ugonjwa uliopelekea kifo chake, alisema, 'Ee Aisha! Bado ninasikia maumivu yaliyosababishwa na chakula nilichokula kule Khaibar, na kwa wakati huu, Nasikia kama vile *mishipa ya uhai wangu itakatwa* kutokana na ile sumu" (al-Bukhari: 4428, fafanuzi imeongezwa). Ukweli kwamba **Q. 69:44-47** imetaja hali ya kifo chake (kukatwa mishipa ya uhai wake) hili lingetokea kwa Mohamedi ikiwa angekuwa nabii wa uongo (i.e.,kuzungumza uongo kumhusu Allah), na baadaye Mohamedi alikufa vilevile kama neno lilivyosema **Q. 69:46**, haikuwa kwa bahati mbaya lakini kuthibitisha kwamba kifo chake ni utimilifu wa maneno ya Aya hizo.

G. *Yesu, siyo Mohamedi, mwenye baraka za kipekee na heshima kwa Allah kwenye ulimwengu huu na ujao*

Q. 3:45 inasema, *"Tazama! Malaika alisema: 'Ee Mariamu! Allah amekupa wewe habari ya furaha ya neno kutoka Kwake: Jina lake litakuwa Kristo Yesu, mwana wa Mariamu, amepewa heshima kwenye ulimwengu huu na ule Ujao ikiwa ni pamoja na (ushirika wa wale) walio karibu na Allah.'"*Ghabril anatolea maoni kwenye Aya hii kwa kusema "kutokana na kusoma Korani najifunza kwamba hakuna mwingine ambaye ameandikiwa kuwa amejulikana ulimwenguni humu na ule ujao Zaidi ya Kristo (Isa), na hakuna mwingine kati ya manabii na mitume atakayefurahia heshima hii isipokuwa Yeye" (Ghabril 2003: 35). Heshima hii ya kipekee ya Kristo imethibitishwa kwenye **Q. 19:31** pale Yesu aliponukuliwa akisema kwamba Allah "*amenifanya mbarikiwa popote nitakapokuwa*." Lester Fleenor anaelezea, "Sura 19:31 imeeleza kwamba Kristo alikuwa amebarikiwa popote alipokuwa, kumaanisha kwamba Mungu alilikubali kila tendo na neno, kwa kila hatua kwenye maisha yake. Mungu hatambariki yeyote kwenye mazingira yote isipokuwa maisha yake *yote* yalikuwa safi na yasiyo na dhambi." (Fleenor 2005: 61) **Q. 19:33** inamnukuu Yesu kama alivyosema, "*Amani ilikuwa juu yangu siku niliyozaliwa, siku nitakayokufa, na siku ambayo kwamba Nitainuliwa juu (tena) kwenye uzima.*" Mtetezi Muislamu Ahmed Deedat anakiri kwamba "hapakuonekana hata alama moja yenye doa/waa kwenye Korani nzima iliyomhusu Yesu (Deedat 2002: 5).

Kwa maana nyingine kama ambavyo imeonyeshwa hapo juu, Mohamedi alionekana kuwa na hatia kwa Allah kwenye Korani. Zaidi, tofauti na Allah kumhakikishia Yesu kwamba atakuwa kwenye heshima baada ya hapa, Mohamedi hakuwa na hakika kwamba hata ataiona Paradiso (**Q. 46:9**; al-Bukhari: 7018; angalia pia 1243, 3929).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

H. ***Yesu, siyo Mohamedi, ni "Ishara" kwa watu wote duniani***

Korani inamwelezea Yesu pekee kama "ishara" kwa watu wote wa ulimwengu: *"Alisema: 'Hivyo (itakuwa):Bwana wako anasema, "hili ni rahisi kwangu: na (Tunakutakia) kumteua yeye kama Ishara kwa watu na Rehema toka Kwetu"'"* (**Q. 19:21**). **Q. 43:61** anaongeza, *"Na (Yesu) atakuwa Ishara (ya kuja kwa) Wakati (wa hukumu)."* (angalia pia **Q. 21:91; 23:50**). Kwa uwazi, **Q. 7:36** inaeleza, *"Lakini <u>wale watakao zikataa ishara zetu</u> na kuzitenda kwa jeuri- <u>washirika wao watakuwa pamoja na moto kukaa huko milele</u>"* (angalia pia **Q. 3:4**). Kwa maana nyingine, Mohamedi hajaelezwa kama Ishara; badala yake, kwa kurudia rudia ilimwelezea yeye kama mjumbe au mhubiri pekee (e.g., **Q. 3:144; 7:188; 11:2, 12; 17:93, 105; 22:49; 24:54; 25:56; 27:92; 29:50; 34:28; 42:7; 46:9; 79:45; 88:21**).

I. ***Yesu, siyo Mohamedi, aliyetenda ishara na miujiza***

Korani inaeleza kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kutenda miujiza, ikiwepo kuongea kama mtoto mchanga (**Q. 19:29-34; 5:110**), kuumba uhai (**Q. 3:49; 5:110**), kuwaponya watu (**Q. 3:49; 5:110**), na kuwafufua wafu (**Q. 3:49; 5:110**); angalia pia **Q. 2:253; 3:45-49; 43:63; 61:6**. Korani inaonyesha kwamba ni Allah pekee mwenye uwezo wa kuumba uhai (**Q. 7:158; 9:116; 10:34, 56; 15:23; 22:73; 23:80; 67:2**). Ingawa Ali alitafsiri **Q. 5:110** kama Yesu "aliumba" ndege kutoka kwenye udongo (Hilali-Khan anasema "alibuni"), neno ni *"akhluqu"* linalomaanisha "kuumba" (kama Sarwar na Arberry walivyotafsiri kwa usahihi **Q. 3:49**). Mahali pengine pote kwenye Korani neno na popote lilipoasisiwa lina tafsiriwa kama"kuumba," pamoja na hasa wakati Allah "alipoumba" kitu (e.g., **Q. 2:29; 3:47; 5:17; 7:19; 14:32; 16:17, 48; 17:99; 22:73; 24:45; 28:68; 30:54; 51:56**). Hata Yesu*"alipulizia"* (ndege wa udongo aliowaumba) pumzi ya uhai (**Q. 3:49; 5:110**). Hicho ndicho hasa Allah alichokifanya kutoa uhai (**Q. 15:29; 21:91; 32:9; 38:72; 66:12**).

Q. 10:34 inasema, *"Mwambie: 'Mwenzi wako,"anaweza kuuasisi uumbaji wa asili na kuurudia?' Sema: 'Ni Allah aliyeasisi uumbaji na kuurudia: ni jinsi gani basi unaupotosha mbali (kutoka kwenye kweli)?'"* Kuhusiana na Aya hii Ali anasema, "Miungu wa uongo hawawezi kuumba chochote kutoka kwenye kitu ambacho hakipo wala kuendeleza nguvu ya uumbaji inayoushikilia ulimwengu" (Ali 2006: Q. 10:34n.1428). Kwa kuwa Yesu *aliumba* uhai, ni lazima asiwe mungu wa uongo lakini lazima yeye mwenyewe ni Mungu. Hili pia linamaanisha, kulingana na **Q. 10:34**, kwamba Yesu *siyo* "mwenza" na Mungu (Kama Uislamu wanavyodai Wakristo humfanya), lakini ni Mungu mwenyewe.[7]

---

[7] Watetezi wa Uislamu huharakisha kuonyesha, "Angalia ni jinsi gani neno 'kwa kuondoka kwangu' lilivyorudiwa kwa kila muujiza kusisitiza ukweli kwamba walifufuka, siyo kwa nguvu au kwa mapenzi ya Yesu, lakini kwa kuondoka na mapenzi na nguvu ya Allah, ambaye ni mkuu kwa Yesu kama alivyo kwa wanadamu wote" (Ali 2006: Q. 5:110n.820). Yapo majibu mawili kwa hili. La kwanza limetamkwa na Muislmu wa awali Daniel Shayesteh: "Pumzi ambayo aliipulizia Yesu kwenye ndege wa udongo ilikuwa na nguvu na tabia ileile kama pumzi aliyoipulizia Mungu kwenye uumbaji. Kama Yesu siyo Mungu, ni jinsi gani pumzi yake yaweza kufanya sawa sawa na ile pumzi ya Mungu? Pumzi hii ilitoka ndani ya Yesu? Ni kwa sababu Mungu alikaa ndani ya Yesu? Pumzi ya uumbaji siyo mali ya Mungu mwenyewe? . . . Ndege ambao wangekuwa ushuhuda kwa kupewa uhai kwa pumzi iliyotoka kwa Yesu. Kwa sababu ya aya hii na nyingine nyingi, ukweli kwamba Korani inaukataa Uungu wa Yesu ni jambo ambalo linaipelekea theolojia ya Korani nzima kutiliwa shaka." (Shayesteh 2004: 141)

Jibu la pili ni kwamba Uislamu wanaweka msingi wa kutokuzielewa maana za Kibiblia zinazomwonyesha Yesu Kristo. Kwa uhakika, Yesu alikuwa mwanadamu kamili.Lakini kimsingi alikuwa Zaidi ya mwanadamu wa kawaida: pia alikuwa Mwana wa Mungu. R. C. Sproul anafupisha kwamba "Kwenye utatu wahusika wote (Baba, Mwana na Roho Mtakatifu) wana asili ya kufanana, kwa heshima, na kwa utukufu. Wote watatu ni wa umilele, wanaojitegemea; wanaushiriki wa vipengele vyote na sifa za Uungu. Kwenye mpango wa Mungu wa Ukombozi, hata hivyo, Mwana kwa hiyari yake mwenyewe alichukuwa jukumu la kumsaidia Baba [angalia **Wafil 2:5-11**]. . . Kwa kujinynyekesha mwenyewe kwenye mapenzi matakatifu ya Baba yake, Yesu alitutendea yale ambayo sisi wenyewe tusingeweza kujifanyia. Alizitii sheria za Mungu kikamilifu. . . . Kwa kuzitii sheria kikamilifu, Yesu aliyakamilisha mambo muhimu makuu mawili. Kwa maneno mengine alipata sifa za kuwa mwokozi wetu, mwanakondoo asiye na waa. Yesu angetenda dhambi, Asingeweza kujilipia kwa dhambi zake mwenyewe, na Mwenyewe kwa dhambi zetu. Pili, Kwa utii wake mkamilifu aliipokea tuzo ambayo Mungu aliwaahidia wote watakaolishika agano lake. Aliistahili tuzo ya mbinguni ambayo alitupa sisi. Kama msaidizi mmoja, Aliwaokowa watu ambao hawakuwa na uwezo wa kujisaidia wenyewe." (Sproul 1992: 79-80)

Huku kujitoa mwenyewe au kujivua mwenyewe cheo na nafasi yake kama Mungu na kuwa mwanadamu kunajulikana kama Kristo's *kenōsis* (**Wafil 2:7**; Zodhiates 1992: *kenoō,* 857-58). Vivyo hivyo, "*kama mwanadamu*, alifanya miujiza yake, siyo kwa umuhimu wa Uungu wake, ambao alikwisha kurithishwa ndani yake, lakini kwa umuhimu wa Imani iliyokamili kwa nguvu za Baba yake, kupitia utele wa "Roho Mtakatifu" (Bickersteth 1957: 99n.*, fafanuzi ya asili). Hiki ni kifungu ambacho Kristo kwa kurudiarudia alisema kwamba hakutenda lolote kwa matakwa yake mwenyewe lakini alitenda kile tu ambacho Baba alimwagiza kutenda (**Yohana 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Kwa maneno mengine, upo umoja mkamilifu, mawasiliano, na maelewano kati ya Baba na Mwana. Hili siyo kinyume cha fundisho la Utatu bali linalithibitisha fundisho. Kwa kweli, kwa ujumla ni utambulisho wa Yesu na Baba kwamba kwenye maneno

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Tofauti na Yesu, Korani inaeleza kwamba Mohamedi alipewa changamoto ya kutenda miujiza lakini alijibu kwamba hana uwezo huo, mwenye uwezo wa kufanya ishara ni Mungu pekee (**Q. 2:118-19; 3:183-84; 6:37, 109; 10:20; 13:7, 27; 17:59, 90-93; 20:133; 21:5; 28:48; 29:50; 30:58; 34:28; 43:40**). Kwa kweli, kulingana na Korani, "ishara" pekee Mohamedi aliyopewa ilikuwa ni *Korani yenyewe* (**Q. 2:118-19; 20:133**).[8]

J. *Yesu, siyo Mohamedi, mwenye ujuzi usiokuwa wa kawaida*

Korani inasema, *"Wewe pekee [Allah] ndiwe unayejua yote kwa yale yote yaliyositirika (au yasiyoonekana, etc.)"* (**Q. 5:109**, Hilali-Khan) na "*kwake [Allah] kunazo funguo za yasiyoonekana,hazina ambayo hakuna aijuaye isipokuwa Yeye*" (**Q. 6:59**; angalia pia **34:2-3**). Mwanazuoni Muislamu na mwandishi Sayyid Saeed Akhtar Rizvi anasema, "*Al-Ghayb* maana yake 'yasiyoonekana' au 'vitu vilivyositirika'. *Ilmu 'l ghayb* maana yake ujuzi wa vitu vilivyositirika kwa sasa, kama matukio yajayo. Ujuzi huo ni haki pekee ya Allah. Hakuna atakayeielewa *ghayb* isipokuwa Allah." (Rizvi 1992: 37) Mwishoni mwa **Q. 3:49** Yesu alinukuliwa akisema, "*Ninawatangazieni ninyi chochote mnachokula, na kile mnachokihifadhi kwenye nyumba zenu. Hakika ni ishara kwenu kama mnaamini.*" *Tafsir al-Jalalayn* anatoa maoni yake juu ya hili, "Nitawajulisha ninyi pia vitu mnavyokula, na vile mnavyohifadhi, kwenye nyumba zenu, na vile ambavyo sikuwahi kuviona, na atawaeleza watu walikula nini na watakula nini" (Jalal 2017: Q. 3:49, maoni; angalia pia Ibn Kathir, *Stories,* n.d.: 178 [Hata kama vile kijana Yesu "angewaambia marafiki zake ni aina gani ya chakula cha jioni walikuwa wakikisubiria nyumbani na nini walichokificha na wapi walikokificha"]). Kwa maneno mengine, Yesu alikuwa na nguvu isiyokuwa ya kawaida au ujuzi wa unabii wa vitu au matukio ambayo alikuwa bado hajayaona. Qushairi anaeleza, "Hizi ni ishara za nje za Yesu na za kushangaza, ambazo ni Zaidi ya uthibitisho: kuwarejeshea wafu uhai, kuwaponya vipofu na wenye ukoma, *kuwaeleza kile walichokitenda kwa*

---

hayo hayo ambayo alisema *"Kwa sababu mimi sikunena kwa nafsi yangu tu; bali Baba aliyenipeleka, yeye mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema"* (**Yohana 12:49**), Yesu pia alisema, *"Yeye aniaminiye mimi, haniamini mimi bali yeye aliyenipeleka.. Naye anitazamaye mimi amtazama yeye aliyenipeleka"* (**Yohana 12:44-45**). Kama al-Masih alivyoelezea kwa kifupi kuhusiana na **Q. 5:110**, "Korani inashuhudia kwa kurudia ukamilifu wa muunganiko miongoni mwa Allah, Kristo na Roho Mtakatifu. Watatu hawa hufanya kwa umoja uliokamilika, hufanya miujiza ya Kristo pamoja. Wakristo pia, wanaamini kwenye matendo ya ushirika wa Utatu Mtakatifu." (al-Masih 1993: 22) Hii ni picha halisi ya Umoja wa Yesu na ushirika mkamilifu wake na Baba ulioelezwa kwenye Biblia na kuzungumziwa na Yesu mwenyewe kwenye **Yohana 12:44-45**. D. A. Carson anahitimisha, "Usaidizi wa kipekee wa Mwana kwa Baba ndio kwa kifupi unaotuhakikishia kwamba Mwana alifanya kile Baba alichokitaka afanye, kwa uhakika, kile afanyacho Baba. . . . Imani hii ndani ya Yesu (mst. 44) siyo Imani ya mwanadamu wa kawaida, unabii mmoja zaidi, lakini Imani ambayo Mungu mwenyewe aliasisi kwa nguvu ya kujifunua mwenyewe, Neno kuuvaa mwili, Mungu/mwanadamu, Mwanae pekee—au vinginevyo siyo Imani kabisa. Na kwa ukaribu sana ni Mwana, Neno, lililotambulishwa na Baba (1:1, 18), kwamba kumwona Yesu ni kumwona Baba aliyemtuma (*cf.* 14:9)." (Carson 1991: 451-52)

[8] Tofauti na maneno ya Mohamedi mwenyewe kwenye Korani na kwenye Hadithi kwamba hakuweza kufanya miujiza, baadaye desturi zilimpa sifa ya miujiza (labda kwa nguvu ya kumfananisha na sifa za Yesu). Miujiza inayodaiwa ni pamoja na: miujiza ya uponyaji (al-Bukhari: 2942, 3701, 4210); miujiza ya kuongezeka kwa chakula au kinywaji (al-Bukhari: 4102; Muslim: 1807a); maji kutiririka katikati ya vidole vyake (al-Bukhari: 169, 200, 3576, 4152; at-Tirmidhi: vol. 1, book 46, no. 3631, 3633; an-Nasa'i: vol. 1, book 1, no. 76, 77); na kuugawanya mwezi kwenye vipande viwili (al-Bukhari: 3636, 3637, 3868, 3870; Muslim: 2800b; at-Tirmidhi: 2182, vol. 1, book 44, no. 3289). Abdul-Mohsin 2006: 181-83, 190-92, al-Athari 2005: 106-07, na Parshall 1994: 51-59 iliyoorodheshwa na kudaiwa kuwa miujiza.

"Kuugawa mwezi" imeandikwa kwenye **Q. 54:1-2** ("*Saa ya (hukumu) imekaribia, na mwezi umefunga*"). Abdel Haleem anaonyesha "Baadhi ya wachambuzi wa kiasili hushikilia kwamba mtazamo huu unaelezea tukio halisi lililotokea wakati wa nabii, lakini kwa uwazi linazungumzia mwisho wa dunia" (Haleem 2005: Q. 54:1n.a; angalia pia Ali 2006: Q. 54:1n.5128). Kwa kutolea maoni yake kwenye *Sahih al-Bukhari*: 3868 ("Watu wa Mecca walimwuliza mjumbe wa Allah kuwaonyesha muujiza. Hivyo aliwaonyesha mwezi uliogawanyika mara mbili nusu tofauti na ambavyo waliuona kwenye mlima Hira') na **Q. 54:1** (Sahih, "*Saa imekaribia, na mwezi umegawanyika [vipande viwili]*"), the Muslim website Quran-Islam.orgobserves kwamba "neno [vipande viwili] halipatikani kwenye Korani ya Kiarabu. Ni wazi kwamba yaliongezwa na watafsiri ili kuyaleta maneno ya Kikorani kufanana na yale ya Hadithi! Hadithi hii ni mfano wa nyingi ambazo kwa wazi zinawasilisha mtafaruku kwenye kweli za Kikorani. Jambo lililo la muhimu ambalo wote wale wanaoamini haditi hizo ambazo kweli hizo za Kikorani zimeonyeshwa kwao ndio wanaosisitiza kutokuiamini Korani." ("Nabii Mohamedi aliugawanya mwezi?" 2001-2019: n.p.) "Mkanganyiko wa wazi wa kweli za Kikorani" Pamoja na madai yote ya asili kwamba Mohamedi alifanya muujiza wowote, kwa kuwa Korani inathibitisha kwamba hakutenda muujiza wowote. Mawdudi kwenye maoni yake anatambua kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kutenda "Miujiza ambayo hakupewa mwingine yeyote kabla yake na wala baada yake [ikiwa ni pamoja na Mohamedi]" (A'la Mawdudi n.d.: Q. 43:59n.53). "Mohamedi alikuwa mtenda miujiza, Kwa kweli kwenye utoto wake alikuwa na hadithi za miujiza na kwenye fasihi za kidesturi zaweza kuwa kweli, laweza kuwa neno rahisi kujibu kwenye changamoto hii. Bado kwenye Korani yote, popote lilipoulizwa swali la kama alionyesha ishara ya nabii kabla ya kuinuka, jibu wakati wote lilikuwa kwenye kundi la kukataa." (Gilchrist 1994: 134)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

siri, na miujiza mingine" (Al Qushairi 2002-2014: Q. 3:49, maoni na fafanuzi imeongezwa) *Kashani Tafsir* anaongeza, "Na nitawaeleza pia kile mlichokula, [kwa vitu vile] mlivyoshiriki kwenye tamaa zenu na starehe, na kile mlichokihifadhi kwenye nyumba zenu, haya ni yale, yaliyoko kwenye nyumba zenu ambayo hayaonekani [sic.] kwa njia ya msukumo na mkazo. Hakika kwa hayo ni ishara kwenu, kama ni Waamini." (al-Kashani 2002-19: Q. 3:49, maoni) Kuthibitisha kwamba Yesu anajua hata makusudi na malengo ya mioyo na mawazo ya watu!

Masih anaelezea kwa ufupi, "Upo uthibitisho wa hali ya juu au ukiri ulio bora Zaidi kwa upande wa Mohamedi kwa Uungu wa Kristo kuliko huu. Alikiri kwamba Kristo anajua kweli zilizositirika na anaweza kuzisoma siri za mioyo ya wanadamu. Anauelewa usiri wako kwa kina. Anaweza kuyadhihirisha matendo yako kwamba ni mazuri au maovu, kwa sababu anajua yote. Hakuna ambaye anaweza kuficha chochote Kwake." (al-Masih 1993: 26) Kwa kuwa hayupo ajuaye yasiyoonekana isipokuwa Mungu (angalia **Q. 2:33; 3:5; 6:59; 9:94, 105; 10:20; 11:5; 13:9; 16:19, 23; 20:7; 21:110; 23:92; 24:29; 27:65; 31:34; 64:18**), lakini Yesu anayajua yasiyoonekana, hivyo kwa usahihi ni lazima Yesu awe Mungu (i.e., Mungu alikuja ulimwenguni kama mwanadamu).

Kwa maneno mengine, Mohamedi alikiri, "*Si waambii kwamba kwangu zipo hazina za Allah, wala siyajui yale yaliyositirika*" (**Q. 6:50**). Kwenye sura zingine, Mohamedi alisema, "*Kama ningekuwa na ujuzi wa yasiyoonekana, Ningeyazidisha mambo yote mazuri, na hakuna uovu ambao ungenigusa: Mimi ni mhubiri tu, na mleta habari za furaha kwa wale wenye imani.'"* (**Q. 7:188**) Kwenye **Q. 10:20** kwa maelezo ya Mohamedi anajiweka mwenyewe kwenye hali ya ile ile kama wasioamini wanaotaka kujua yasiyoonekana, *"Nao walisema: Kwanini hakuna ishara iliyotumwa kwake na Bwana wake? kusema: Yasiyoonekana ni kwa Allah pekee; kwa hiyo mimi pia kwa uhakika nasubiria, pamoja nanyi ni miongoni mwa wale wangojao."* (Shakir)

K. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyefundisha kwa mamlaka ya Kiungu*

Q. 43:63 inasema, *"Wakati Yesu alipokuja na Ishara ya wazi, Alisema: "Sasa nimekuja kwenu na Hekima, na ili kuyaweka wazi mambo ambayo kwayo mmekuwa mkiyashindania: kwa hiyo mche Allah na kunitii Mimi."* **Q. 3:55** kwa nyongeza alisema, *"Wale wakufuatao Yesu nitawaweka juu kuliko wale walioikataa imani,kwa siku ile ya kufufuka"* Yusuf Ali anaonyesha, "Wale *wataakaokufuata wewe* inawahusu pia Waislamu (ambao watayafuata mafundisho ya msingi ya Yesu) na Wakristo (wanaodai kumfuata Yeye)" (Ali 2006: Q. 3:55n.396).Kwa uwazi wa kifungu hiki, Makala iitwayo "Uislamu wa kweli kwa mtazamo wa Wakristo" inaeleza "Kila mtu anayetaka kuja kwa Mungu na afuate neno la sheria, manabii na maneno ya Yesu yaliyoithibitisha sheria. Muislamu wa kweli hutamani kuujua ufunuo wote wa Mungu. Kwa hiyo hawezi kuidharau Sheria, Manabii na Injili. Muislamu wa kweli atayatii maneno ya Yesu." ("Uislamu wa Kweli" 2014: Ni nani atakayetufundisha sisi Uislamu wa kweli? nukuliwa **Q. 5:44, 46-47; 43:63**)

Q. 3:50 inaenda mbali zaidi; inamnukuu Yesu alivyosema, *"(Nimekuja kwenu), kuwashuhudia Sheria ambazo zilikuwa mbele yangu. Na kuvihalalisha sehemu ya vile ambavyo vilikuwa (Kabla)vimeharamishwa kwenu; Nimekuja kwenu na ishara itokayo kwa Bwana wenu. Hivyo mche Allah, na mnitii Mimi."* Ibn Kathir anatoa maoni, "Sehemu ya Aya hii inaashiria kwamba 'Isa alifuta baadhi ya sheria za Tawrah na kuwaeleza Wayahudi ukweli kuhusu baadhi ya mambo ambayo kwayo walikuwa wakishindania" (Ibn Kathir, *Tafsir,* n.d.: Q. 3:50, anatoa maoni; angalia pia Al Qushairi 2002-2014: Q. 3:49, maoni). Hili ni wazi kama Allah anavyosema *"<u>Tulifuta</u>"* ufunuo wetu (**Q. 2:106**). Kwa maneno mengine, Yesu siyo tu kwamba alithibitisha sheria (Torah) lakini alikuwa na *mamlaka juu ya sheria hizo.* Kwa kuwa Sheria zilikuwa za Mungu, Mungu pekee ndiye mwenye mamlaka juu ya sheria zake mwenyewe. Mungu pekee ndiye mwenye mamlaka ya "kufuta" sheria zake. Kwa kufanya kile ambacho Mungu pekee ndiye angekifanya, Yesu alithibitisha kwamba alikuwa kwa uhakika, Mungu aliyekuja duniani kama mwanadamu.

Kwa maneno mengine, Mohamedi alisema wazi (**Q. 46:9**), "*Mimi siyo kitu halisia miongoni mwa wajumbe wengine*" (Sahih) au, kama Ali alivyotafsiri, "*Mimi siyo mleta au muasisi wa mafundisho mapya miongoni mwa wajumbe*." Aliambiwa pia kwamba ashauriane na watu wa Kitabu (i.e., Wakristo na Wayahudi) ili kwamba aweze kufahamu maana ya ufunuo uliokuja kwake (**Q. 10:**94). Mohamedi alidai kuthibitishiwa kile tu alichofunuliwa kabla (**Q. 41:43;** angalia pia **6:90**).

L. *Yesu, siyo Mohamedi, aliyepandishwa mbinguni akiwa hai ambako bado akingali hai*

Q. 4:158 inasema, "*Allah alimwinua yeye [Yesu] kwake Mwenyewe"* (angalia pia **Q. 3:55**). Kwa kusema kwamba Allah alimwinua Yesu juu *kwake mwenyewe,* Korani inathibitisha kwamba Yesu "alirudi kwenye enzi ya Mungu mahali alipotoka" (Gilchrist 2015: 91). Kwa maneno mengine, Yesu hakupaa kwenye ufalme wa mbingu ya kawaida – alirejea kwenye uwepo wa *Baba yake* juu sana ya mbingu na akakaa kwenye mkono wakuume wa kiti cha Enzi cha Mungu Mwenyewe" (Ibid.). Hili linamaanisha kwamba Yesu ni njia ya

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mbinguni kwakuwa Yeye mwenyewe yuko kule. Kama tulivyoona, Mohamedi hajui kama ataweza kufika mbinguni siku moja hapo baadaye (**Q. 46:9**; al-Bukhari: 7018; angalia pia 1243, 3929). Hili linamaanisha pia kwamba Yesu yuko hai sasa, Miaka 2000 iliyopita baada ya kutembea hapa duniani. Kwa maana nyingine, Mohamedi alikufa na kuzikwa kule Medina. Kaburi lake pekee lipo pamoja nasi hata leo. Kwakuwa Yesu yu hai na Mohamedi amekufa, hata kulingana na Korani, Yesu ni Mkuu kuliko Mohamedi.

M. ***Yesu, siyo Mohamedi, atakayekuja tena ulimwenguni kuhukumu na kutawala***

Q. 43:61 inasema, *"Na (Yesu) atakuwa ni ishara (kwa kuja kwa) Saa ya (hukumu): kwa hiyo usiwe na shaka kuhusiana na (Saa), lakini nifuate mimi: hii ni Njia ya moja kwa moja."* Hilali-Khan alilitafsiri hili kwa njia hii: *"Na wewe ['Iesa (Yesu),mwana wa Mariamu utajulikana kuwa ishara ya (kuja kwa) Saa ya (Siku ya kufufuka) [i.e. 'Iesa's (Yesu) kurudi tena duniani]. Kwa hiyo usiwe na shaka kuhusiana na hilo (i.e.Siku ya kufufuliwa)."* Kwenye Hadithi, Mohamedi anathibitisha kwamba Yesu atarudi tena duniani: "Mjumbe wa Allah alisema, 'Kwake Yeye ambaye nafsi yangu ipo mikononi mwake, hakika (Yesu) Mwana wa Mariamu atawajia miongoni mwenu na atawahukumu wanadamu kwa haki (kama Mtawala wa haki)'" (al-Bukhari: 3448; angalia pia 2222, 2476). Maoni ya Karim kwenye *Mishkat ul-Masabih* anasema kwamba tukio la pili Kristo ni "Ijma [i.e., Makubaliano ya jumuiya ya Kiislamu kwenye masuala ya kidini] ambayo yanahitajika kwa Uislamu" (Karim 1939: 4:79).

Wakati atakaporudi, Utawala wa haki wa Yesu utakuwa kwa ulimwengu wote. Tena, Yesu anafanyia kazi sifa ya Uungu, kwa sababu kama **Q. 6:57** inasema, *"Niambie: 'Kwangu Mimi, Nina (fanya) kwa ishara ya wazi kutoka kwa Bwana, lakini mlimkataa. Mtakachoona kikiwaharakisha, hakitatokana na nguvu zangu. Amri zinabaki kwa mmoja tu ambaye ni Allah: Atatangaza kweli, na ni hmhukumu bora.'"* Yesu pekee ndiye "Mtawala wa Haki" kwa sababu haki ni kama Allah *"atatangaza kweli,na ni mhukumu bora miongoni mwa mahakimu."* Yesu pekee ni "Mtawala wa Haki" kwa sababu kama ambavyo Allah *"hutangaza kweli, na Yeye ni Hakimu aliye bora zaidi ya wote,"* hivyo Yesu *ni* "Neno" na "Roho" toka kwa Mungu. Yesu pekee ndiye mtawala wa haki kwa sababu tofauti na Mohamedi, Yeye pekee ndiye"Masihi," hana dhambi yeyote, na ni mkamilifu "Mtakatifu" (**Q. 19:19**). Yesu pekee ndiye Mtawala kwa sababu Yeye pekee ndiye ambaye hakuguswa na Shetani (al-Bukhari: 3286) na kwa hiyo "ni mtakatifu, nafsi isiyo na hatia . . . aliyeivaa kweli, wa uhakika, mwenye haki, na mwenye ubora wa hali ya juu" (A'la Mawdudi n.d.: Q. 4:171n.213). Yesu pekee ndiye Mtawala wa Haki kwa sababu anajua yasiyoonekana, hata "mawazo na nia za watu" (al-Kashani 2002-19: Q. 3:49, maoni). Kulingana na Korani, Mohamedi hana hata moja ya sifa hizo. Mohamedi alikufa na, kulingana na Korani, tofauti na Yesu hatarudi "kuwahukumu wanadamu kwa haki."

N. ***Hitimisho***

Kulingana na Korani yenyewe hakuna aliye kama Yesu, hakuna hata Mohamedi. Kama ambavyo mmoja wa waandishi alivyoliweka kulingana na sifa zote ambazo Korani imezisema kuhusiana na Yesu, "Haya yote hayaleti maswali ya msingi ya kwamba ni jinsi gani 'mwanadamu' mtu anaweza kuziunganisha sifa zote hizo hapo juu kwake Yeye mwenyewe? Tunamfahamu mtu yeyote ambaye anaweza kujisifu kwa kujiita angalau mbili tu kati ya sifa hizi kuwa ni zake? Kwa habari ya Yesu, mtu angeweza tu kuhitimisha kwamba alikuwa mwanadamu wa Kipekee. Na kwamba ni Mungu!" (Nehls 2011: 53)

IX. <u>Tabia za Mohamedi</u>

Q. 33:21 inasema, *"Umewekeza kwa mjumbe wa Allah hali ya mwonekano ulio bora (wa tabia) kwa yeyote ambaye tumaini lake ni kwa Allah na kwa Siku ya mwisho, na kwa wale wanaojihusisha na kumsifu Allah."* Muislamu Professor Abdul-Mohsin aliorodhesha tabia na kanuni za Mohamedi kama ushahidi wan nne au ishara ya Unabii wake.[9] Abdul-Mohsin anasema, "Kabla ya ujio wa Mohamedi hapakuwa na ukamilifu wa maadili uliotumika kama ushahidi wa unabii" na "uadilifu mkamilifu wa nabii ulikuwa ni ushahidi wenye nguvu ambao uliwafanya watu wengi kumwamini Mohamedi, hata kabla ya kushuhudia miujiza iliyo dhahiri" (Abdul-Mohsin 2006: 213, 214). Emerick anasema kwamba Mohamedi "anachukuliwa na Waislamu kama kielelezo kilicho bora kwa mume, baba, rafiki, mlezi na mwanasiasa" (Emerick 2004: 131). Abdul-Mohsin alimwita "mfano wa mwanadamu mkamilifu" na "mwenye hali ya ukamilifu na mfano kwa wanadamu wote" (Abdul-Mohsin 2006: 56-57)

Korani na Hadithi kwa kweli zinafunua tabia zingine tofauti na muhimu za kuangalia kuliko tathmini

[9] Shuhuda nyingine tatu alizozijadili ni Korani yenyewe, Miujiza inayodaiwa kutendwa na Mohamedi, na unabii unaomhusu Mohamedi unaodaiwa kuwa kwenye Biblia. Suala la miujiza ya Mohamedi limejadiliwa hapo juu kwenye kipengele cha **2.VIII.H.** ***Yesu, siyo Mohamedi, ni "Ishara" kwa watu wote duniani***. Korani na unabii wa Mohamedi unaodaiwa kuwa kwenye Biblia utajadiliwa kwenye sura ya **5. BIBLIA NA KORANI**.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

iliyofanywa na Abdul-Mohsin na Emerick. Wakati akiwa bado Maka, Mohamedi alikutana na upinzani na kwa kweli, hakujibu kwa hasira wala kwa lazima; kwa wakati huo hakuwaamuru wafuasi wake (ambao wengi wao walikuwa ndugu na wachache kwa idadi yao) kupigana au kuanzisha vita, kwa kuwa aliangalia mwenyewe kiurahisi kama "mhubiri" aliyetumwa na Allah (**Q. 2:119; 14:4; 42:7; 43:3; 46:12**). Alikuwa anafurahia ndoa ya mke mmoja tu ambaye ni, Khadijah. Kwa sababu Khadijah alikuwa tajiri, alikuwa ametosheka kwenye mahitaji yote (Ibn Abbas 2016: Q. 93:8, maoni). Aliishi maisha rahisi, mtu wa mpangilio, kwa kiwango kikubwa, aliendelea hivyo kwa maisha yake yote (Gilchrist 1994: 57-58; Parshall 1994: 43-44). Hata hivyo, mazingira yalibadilika, hasa hasa alipohamia Madina mwaka 622. Baada ya wakati huo Mohamedi alikuwa shujaa-nabii-mtawala kwenye usimamizi wote wa dini na nchi. Tabia yake halisi hapo ilifunuliwa. Ilikuwa hivyo kwa sababu kwa sasa alikuwa na nguvu za kuamrisha na kupata chochote alichokitaka—na kile alichokitaka na kwa jinsi alivyoendelea ndivyo alivyoendelea kudhihirika ninini hasa kilichokuwa kwenye uhalisia wa moyo wake kiliifunua tabia yake.

Kwa kuwa Mohamedi ni kiini na kielelezo kwa Waislamu, ni muhimu kuichunguza tabia yake—kama ilivyofunuliwa na mambo muhimu kwenye maisha yake—kwa kulinganisha na tabia ya Yesu Kristo. Hili ni la kweli kwa kuwa Mohamedi alijilinganisha mwenyewe na Yesu Kristo: "Mimi ninafanana sana na Yesu Kristo miongoni mwa wanadamu wote" (Muslim: 2365b; see also 2365a, c; al-Bukhari: 3442, 3443).

A. *Mohamedi na pesa*

Kwenye **Q. 6:90** Mohamedi aliamriwa kufuata mfano wa manabii wengine na asitoze fedha kwa ujumbe wake wowote: *"wale ambao ni (manabii) ambao wanapokea mwongozo wa Allah: Pokea nakala ya mwongozo ambao waliopokea; Unaosema: 'Sikuuliza tunu yeyote kwenu kwa kufanya haya: Hili ni Zaidi ya ujumbe kwa mataifa'"* (Ayat zilizofuata zinaelekeza kanuni hii kwa Mohamedi: **12:104; 25:57; 42:23; 52:40; 68:46**. Ayat zinazofuata zinatoa maelekezo hayo kwa manabii wengine: **Q. 10:71-72** [Nuhu]; **11:29** [Nuhu]; **26:109** [Nuhu], **145** [Salih], **164** [Lutu], **180** [Shu'ayb]; **26:124-27** [Hud]; **36:20-21** [Wajumbe wengine]). Pamoja na amri hii toka kwa Allah (ambayo inawiana na maisha ya kila siku ya manabii wa KiBiblia), Tamaa ya utajiri ya Mohamedi inafunuliwa wazi wazi kwenye Korani na kwenye Hadithi. Matukio mawili yanaifunua tabia ya Mohamedi kuhusiana na tamaa yake ya utajiri na jinsi ambavyo hakuwajali maskini. Kwenye **Q. 7:188** Mohamedi anasema, "*Kama ningekuwa na ujuzi wa kuona yasiyoonekana, Ningezidisha mema yote, na hakuna baya ambalo lingenigusa*." Mohamedi alikuwa anasema kwamba kama angekuwa na ujuzi wa kuona yasiyoonekana angetumia ujuzi huo "*kujipatia mema mengi na hakuna dhara ambalo lingenigusa.*" Kwa maneno mengine, jitihada zake zilikuwa za kibinafsi na nia yake yote ilikuwa ni kujinufaisha mwenyewe kwa mema mengi na kujiepusha na madhara yeye mwenyewe badala ya kuwalinda na kuwabariki wengine. Kwenye tukio jingine, Mohamedi "alipuuza swali la mtu kipofu aliyekuwa amependezwa na Uislamu, kutokana na masumbufu yake ya kujaribu kumfukuzia mtu ambaye alikuwa na mali ili kumshawishi kuingia kwenye Uislamu" (Dirks 2008: 187). Allah alimkemea Mohamedi kwajambo hilo, kama **Q. 80:1-6** ilivyoandika. Kwa kumkubali tajiri Zaidi ya maskini, Mohamedi aliufunua uhalisia wa moyo wake.

Wakati Mohamedi alipokuwa mtu wa vita aliweza kuitendea tamaa yake kazi ya kupata fedha na utajiri. **Q. 8:1** (Hilali-Khan) anasema, *"Walimuliza yeye (Ee Mohamedi SAW)vipi kuhusu nyara za vita. Akasema: 'Nyara ni kwa ajili ya Allah na Mjumbe wake'"* (angalia pia **Q. 59:7**). **Q. 8:41** inawaamrisha watu wa Mohamedi kumpa yeye (Mohamedi) moja ya tano ya nyara zilizochukuliwa vitani. Kwa nyongeza ya hiyo moja ya tano ya nyara za vita, Mohamedi pia alipokea "sehemu maalum" ya nyara zinazoitwa "*safi*," kama ambavyo hadithi inasimulia: "Nabii alikuwa na sehemu maalum kwenye hazina iliyoitwa safi. Hii ingekuwa ni mtumwa kama angetamani au binti mtumwa kama angemtamani au farasi kama angemtamani. Angevichukuwa hivi kabla ya kugawiwa ile moja ya tano." (Abi Dawud: 2991) Mohamedi alipata "sehemu yake maalum" kwenye nyongeza ya gawio la moja ya tano la nyara hata kama hakushiriki vitani yeye mwenyewe (Abi Dawud: 2992-93). Kwenye tukio moja, Mmoja wa wapiganaji wa Mohamedi, Dihyat Al Kalbi, alimpokea binti mtumwa kama sehemu ya gawio lake kutoka kwenye nyara; hata hivyo, "Wakati Yeye [Mohamedi] alipomtazama yule binti, alimwambia yule mpiganaji 'chukua binti mwingine kutoka kwenye mateka hawa.' Ndipo nabii alipomweka yule binti mtumwa na kumwoa." (Abi Dawud: 2998; angalia pia 2996-97; al-Bukhari: 947, 2228)

Kwa nyongeza ya ile moja ya tano ya nyara na "sehemu yake maalum" (ikiwa ni pamoja na mwanamke yeyote ambaye angemtamani, hata kama angekuwa wa mtu mwingine), Mohamedi alipokea kiwango cha kueleweka cha mali isiyohamishika: "Malik ibn Aws al-Hadthan alisema (Abi Dawud: 2967). Kwa matokeo hayo, Korani inasema kwamba Allah *"alikupata wewe [Mohamedi] ukiwa maskini, na kukufanya tajiri (kujitosheleza mwenyewe na kujiridhisha mwenyewe, nk.)"* (**Q. 93:8**, Hilali-Khan; angalia pia al-Bukhari: 2298 ["Allah alimtajirisha Nabii kwa nyara"]).

"Uislamu wanaweza kudai kwamba Mohamedi alitumia utajiri wake kuwasaidia wale walikuwa na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

uhitaji na kwamba yeye mwenyewe hakuishi maisha ya anasa. Hili liko kinyume na uhalisia, kwa kuwa suala tulilo nalo ni kwamba Mohamedi alikuwa na utajiri mkubwa kama matokeo ya Allah kuwaamuru Uislamu kumpa nabii sehemu kubwa ya nyara zao, ingawa Korani inasema kwamba nabii hakupokea mshahara wala zawadi kutoka kwa watu!" (Shamoun na Katz, "Faida" n.d.: n.p.)

B. ***Mohamedi na wanawake***

Q. 4:1 inazungumza juu ya umoja wa asili wa mume na mke (Bwana *"alikuumba wewe kama mtu mmoja, aliumba, kwa asili yake, Mwenza wake"*). **Q. 3:195** inaashiria mfanano wa vipaji kwa wanaume na wanamke (*"Siwezi kujuta wala kupoteza kazi yangu ya kuwaumba ninyi kuwa mwanaume au mwanamke"*; angalia pia **Q. 16:97**). Hata hivyo, wanawake na wanaume (hasa wanawake walioolewa) hawaonekani kuwa na haki sawa kama wanadamu kwenye Korani: *"Wamaume ndio wenye mamlaka juu ya wanawake kwa [haki ya] kile ambacho Allah alichowapa mmoja na mwingine"* (**Q. 4:34**, Sahih); *"wao (wanawake) wanayo haki sawasawa na hao (wanaume) juu yao kwa huruma, na wanaume wana kiwango cha juu kwao"* (**Q. 2:228**, Pickthall). Ibn Kathir anatolea maoni yake juu ya aya hii, "Wanaume wana nafasi kubwa Zaidi ya Wanawake kimwili na hata kitabia, hali, utii (wa wanawake kwao), kufanya matumizi, kuyaangalia maslahi yao na kwa ujumla, kwenye maisha haya *na yale yajayo*" (Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 2:228, maoni na fafanuzi imeongezwa).

Kwa sababu ya nafasi za juu, Korani inawaruhusu wanaume kuwapiga wake zao (wanawake hawana haki ya kuwapiga waume zao):*"Na wale mnaowaogopa waweza kuwa waasi muwakemee; wafukuzeni kwenye viti vyao,na muwapige,"* **Q. 4:34** (Arberry).[10] Kwa nyongeza, wanaume wapokee sehemu mara dufu ya urithi wa wanawake (**Q. 4:11, 12, 176**); ushahidi wa mwanaume mmoja mahakamani ni sawa na wa wanawake wawili (**Q. 2:282**); wanawake, lakini siyo wanaume, wanapaswa kujifunika kila mahali isipokuwa nyuso zao na mikono wanapokuwa kwenye maeneo ya watu wengi (**Q. 24:31**; angalia Jalal 2017: Q. 24:31, maoni); Wanaume , lakini siyo Wanawake, wanaweza kuoa Zaidi ya mke mmoja (**Q. 4:3**) na wanaweza kuoa na kufanya mapenzi na msichana ambaye hajavuna ungo bado (**Q. 65:4**); na wanawake wanahesabiwa, kimsingi, kuwa ni mali za waume zao:*"Wake zako ni kama shamba lako. Unaweza kuingia shambani mwako kwa njia yeyote uitakayo"* (**Q. 2:223**, Sarwar).

Kwenye Hadithi, Mohamedi alieleza mtazamo unaofanana na huo kuhusiana na jinsi alivyowaweka wanawake kwenye daraja la chini, ni pamoja na:

- <u>Kimsingi wanawake ni waovu na wanaostahili kupigwa:</u> "Nilimsikia Nabii akisema, 'Ishara za uovu

[10] Baadhi ya watetezi wa Uislamu hujaribu kufifisha ukweli kwamba Korani imeruhusu wanawake wapigwe. Yahiya Emerick anaelezea mfano wa Mohamedi akiunyanyua mswaki wake juu alipoulizwa mwanume atumie nini kumchapa mke wake (Emerick 2004: 160). Ali na Hilali-Khan hata anaongeza neno "kwa upole" kwenye mahusiano baada ya neno "wapigwe" kwenye **Q. 4:34**, ingawa "Kiarabu halisemi wapigwe polepole, linasema tu kwamba wapigwe" (Spencer 2009: 20). Zaidi, kifungu kinaashiria kwamba "kupigwa kunakuja kama onyo la mwisho wakati tendo la ndoa limezuiliwa. Kupigwa polepole baada ya tendo la ndoa kuzuiliwa ni kitendo cha kutokuridhika na kwamba hakileti maana yeyote. . . . Kupiga ni lazima kuwe kwa nguvu kuliko kutoridhika na tendo la ndoa ili kuwa na matokeo yoyote." (Newton na Haqq 2006: 13)

Mohamedi hasisitizi kwamba kupiga wanawake kufuate maelekezo yaliyoandikwa na sheria kwa umakini au kuwa kwa "wepesi." Hadithi inatuambia kwamba "Nabii alisema: Mwanaume hawezi kuulizwa kwanini anampiga mke wake" (Abi Dawud: 2147; angalia pia Ibn Majah: vol. 3, book 9, no. 1986). Kwenye hadithi moja, Aisha (Mke kipenzi cha Mohamedi) anasema kwamba Mohamedi alimwacha usiku mmoja alipokuwa anadhani amelala. Aliamka na kumfuatilia. Wakati aliporudi "alinipiga kifuani kwa nguvu jambo lililoniumiza" (an-Nasa'i: 3964; see also 3963). Kwenye hadithi nyingine, "Habibah binti wa Sahl alikuwa mke wa Thabit ibn Qays Shimmas. Alimpiga na kumvunja sehemu. Hivyo alikuja kwa Nabii baada ya kupambazuka, na alimlalamikia juu ya mume wake. Nabii alimwita Thabit ibn Qays na alimwambia (Yeye): Chukua baadhi ya mali zake na ujitenge na huyo mwanamke. Aliuliza: Hiyo ni haki, Mjumbe wa Allah? Alimwambia: Ndiyo. Alisema: Nilimpa bustani mbili za kwangu kama mahari yake, na tayari zipo kwenye umiliki wake. Nabii alisema: Zichukue na ujitenge naye." (Abi Dawud: 2228; angalia pia 2227) Kumbuka kwamba mwanamke huyu alikuwa amepigwa kiasi cha kuvunjika mfupa, bado Mohamedi hata hakumwadhibu au hata kumwuliza swali huyo mwanaume aliyempiga huyo mwanamke. Badala ya kumfunga jeraha la mwanamke, Mohamedi aliagiza huyo mwanamke arudishe mahari aliyokuwa amepokea, hili linamaanisha kwamba, ingawaje ni yeye aliyekwenda kumlalamikia mume wake, alipaswa kuvumilia kipigo kikali na tena arudishe mali zake; mwanaume hakupoteza chochote na sasa anao uwezo wa kumlipia mwanamke mwingine mahari! Hali kadhalika, al-Bukhari: 5825 anaeleza kwamba mwanamume alimpiga mke wake kipigo kikali kiasi kwamba nguo ya uso wake ilikuwa na alama za kijani: "mwanamke (alikuja), akiwa amejifunga utaji wa kijani (na kumlalamikia [Aisha] mume wake na kumwonyesha alama ya kijani kwenye ngozi yake iliyosababishwa na kipigo). Ni tabia ya wanawake kusaidiana mmoja na mwingine, hivyo Mjumbe wa Allah alipokuja, Aisha alisema, 'Sijawahi kuona wanawake wanaoteseka kama wanawake walioamini kwenye Uislamu. Angalia! Ngozi yake ni ya kijani kuliko hata nguo yake!'"—bado Mohamedi hakumhukumu mume kwa kumpiga mkewe usoni.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

zipo kwenye vitu vitatu: Farasi, mwanamke na nyumba'" (al-Bukhari: 2858; angalia pia 110, 2859, 5093, 5094; Abi Dawud: 3921); na "Wanawake ni kama ubavu. Unapojaribu kuunyoosha, utauvunja. Na kama utamwacha pekee yake utamfaidi, na uovu utabaki ndani yake." (Muslim: 715l; angalia pia 1467a, b, 1468a; al-Bukhari: 5184; angalia pia 3331, 5184, 5185, 5186);

- Wanawake wana makosa kwenye ufahamu wao, na kwenye dini, na huwafanya wengi waende jehanamu: "Hata Mjumbe wa Allah alipoenda nje kwenye Musalla (kufanya maombi) ya 'Id-al-Adha au maombi ya Al-Fitr. Basi alimpita mwanamke na kusema, 'Ee Mwanamke! Toa sadaka (changizo), kwa kuwa nimewaona wengi wa wale wakaao kwenye Ziwa la moto walikuwa ni ninyi (wanawake).' Wakauliza, 'Kwanini iwe hivyo, Ee Mjumbe wa Allah?' Alijibu, 'Mnalaani wakati wote na hamna shukurani kwa waume zenu. Sijamwona mwingine yeyote ambaye amepungukiwa na ufahamu na dini kuliko ninyi. Mwanaume mwangalifu na mwenye umakini aweza kupotoshwa na mmoja wenu.' Mwanamake akauliza, 'Ee mjumbe wa Allah! Upungufu wetu ni upi kwenye ufahamu na dini?' Alisema, 'Ushahidi wa wanawake wawili je siyo sawa na ushahidi wa mwanaume mmoja?' Wakajibu kwa kuthibitisha. Alisema, 'Huu ni upungufu kwenye uelewa wake. Siyo ukweli kwamba mwanamke hawezi kuomba wala kufunga anapokuwa kwenye hedhi?' Wanawake wakajibu kwa kuthibitisha. Akasema, 'Huu ni upungufu wake kwenye dini.'" (al-Bukhari: 304; angalia 1462, 5196);
- Wanawake hufuta maombi ya wanaume na wanalinganishwa na punda na mbwa: "Anasimulia Aisha: Vitu vinavyofuta maombi vimetajwa mbele yangu (na hivyo ni): mbwa, punda na mwanamke. Nikasema, 'Umetulinganisha sisi (wanawake) na punda na mbwa.'" (al-Bukhari: 514; angalia pia 511; Ibn Majah: vol. 1, book 5, no. 949, 950, 951)
- Mwanamke hawezi kuwa pekee yake na mwanaume au kusafiri isipokuwa pale anapokuwa amefuatana na mwanaume: "Anasimulia Ibn Abbas: kwamba alimsikia Nabii akisema, 'Hairuhusiwi kwa mwanaume kuwa na mwanamke pekee yao, na hakuna mwanamke atakayesafiri isipokuwa na Muhram (i.e. mume wake au mtu ambaye hataweza kumwoa kwa sababu yeyote milele; e.g.Baba yake, kaka yake nk.).'" (al-Bukhari: 3006; angalia pia Muslim: 1341c)
- Kazi ya mwanamke kwa mume wake ni ya msingi hata kuliko ile kazi yake kwa Allah: "Abdullah bin Abu Awfa alisema 'Wakati Muadh bin Jabal alipokuja kutoka Sham, alimsujudia Nabii ambaye alisema: "Ni nini hii, Ee Muadh?" Alisema: "Nilienda Sham na kuwaona wakiwasujudia maaskofu wao na wale wanaowaheshimu na Mimi nilitaka kufanya hivyo kwako." Mjumbe wa Allah akasema: "Usifanye hivyo. Kama ningemwamuru yeyote kusujudia chochote Zaidi ya Allah, Ningewaamuru wanawake wawasujudie waume zao. Mmoja ambaye nafsi ya Mohamedi ipo mikononi mwake! Hakuna mwanamke ambaye angekamilisha kazi yake kwa Allah mpaka pale ambapo angekamilisha kazi yake kwa mumewe. Kama angemhitaji (kwa mahusiano) hata kama angekuwa juu ya kitanda cha Ngamia, huyo mwanamke hapaswi kukataa.'" (Ibn Majah: vol. 3, book 9, no. 1853; angalia pia 1852; Abi Dawud: 2140; al-Bukhari: 814)

Mtazamo huu juu ya wanawake umedhihirishwa kwenye mahusiano ya Mohamedi mwenyewe na wake zake. Mara kabla ya Mohamedi kwenda Medina, mkewe mwenye miaka 50, Khadijah, alikufa. Baada ya kifo chake, Mohamedi alifunua tabia yake halisi kuwahusu wanawake. **Q. 4:3** aliwaruhusu wanaume kuona hadi wanawake wanne lakini kama tu angewatendea wote kwa haki (au, kama ambavyo *taarifa kwa umma wa Uislamu itakavyokuwa imetolewa*, "Pale tu ambapo mwanaume anavyo kwa utele" ["Muislamu anaweza" n.d.: n.p.]). Miongozo hiyo haikutenda kazi kwa Mohamedi. Hivyo, kufuatia kifo cha Khadijah, "Mohamedi alioa wanawake wengi kama alivyotaka na akawaweka wengine wengi kwenye sehemu yake maalum (harem) kama masuria. Idadi ya wake zake ilitofautiana kati ya tisa na kumi na tatu, na wengi wao hawakuwa na chaguo kwenye jambo lolote—kwa 'ufunuo wa kiungu,' kila mwanamke aliyemtamani alimchukua pia." (Sundiata 2006: 363) Lakini wakati Mohamedi angefanya mambo yake ya muhimu kama atakavyo na mwanamke, wake zake hawakuruhusiwa kuolewa tena baada ya kifo chake (**Q. 33:53**).

Mwanamke aliyekuwa na kibali Zaidi kwake alikuwa ni Aisha. Kama Aisha alivyosimulia, "Mjumbe wa Allah alinioa Mimi wakati nikiwa na umri wa miaka sita, na alikamilisha ndoa na Mimi wakati nikiwa na miaka tisa, na nilikuwa nikicheza na wanasesere (an-Nasa'i: 3378; angalia pia 3255; al-Bukhari: 3896, 5133, 5134, 5158; Muslim: 1422b, d; Abi Dawud: 2121). Anaelezea pia kwamba alikuwa "akicheza (swing) aina Fulani ya muziki na mmoja wa marafiki zake wa kike" wakati Mama yake alipompeleka kwa Mohamedi kufunga ndoa yao (al-Bukhari: 3894; angalia pia Abi Dawud: 4935).

Sundiata alivyochunguza: "Mohamedi alikuwa 'Nabii peke yake' aliyefanya kila kitu kwa faida yake mwenyewe na kujistahilisha—kwa gharama za waumini wengine ikiwa ni lazima. Allah aliandaa kila kitu ili kwamba Mohamedi asipate ugumu kwa kila kitakachomkabili. Allah wa Mohamedi ni aina ya mungu ambaye mwanadamu wakati wote anaweza kumtengeneza; mungu atendaye kile tu kinachotupendeza; mungu ambaye huandaliwa kubadilisha amri zake ili kuchukuliana na matamanio yetu; mungu ambaye yupo kutenda amri zetu

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

baada ya kushauriana na sisi; mungu ambaye yupo kwa ajili yetu lakini yupo kinyume na maadui zetu; mungu ambaye huonyesha Rehema kwetu lakini hutoa haki kwa yeyote yule; mungu dhaifu asiye na kusudi na asiye na maamuzi." (Sundiata 2006: 367)

Kukataa kwa Mohamedi kuwatendea kwa usawa na haki wake zake kulipelekea wao kugawanyika kwenye makundi mawili yanayokinzana. Maumivu yao ya kutokutendewa kwa usawa kuliwapelekea baadhi ya wake zake kudai kwake Zaidi ya tukio moja kuomba watendewe haki—lakini aliwakatalia, kama *Sahih al-Bukhari* anavyotolea taarifa kwa hadithi ndefu (al-Bukhari: 2581; angalia pia 2580) Wivu na uadui ni asili ambayo imejengeka kwenye ndoa za wake wengi kwa sababu haiwezekani kupenda na kuwatendea wanawake wengi kwa usawa (kama **Q. 4:3** inavyodai). Kwamba hilo lilikuwa baya zaidi kwa Mohamedi kwa sababu, kwa **Q. 33:51**, hakuweza kuwa "makini" kwa wake zake na haikuwezekana. **Q. 66:3-4** na Hadithi (al-Bukhari: 6691; vol. 6, book 60, no. 435) inafunua wivu na hila miongoni mwa Wake za Mohamedi na mabishano na malalamiko juu yake. Kwa kweli, kuna wakati ambao hali ilikuwa mbaya kiasi kwamba Mohamedi aliwaza kuwataliki wake zake wote, kama ambavyo mshirika wake Umar alivyoelezea: "Kutokana na wivu wa wake za Nabii, walijiwezesha wenyewe kwa wenyewe kinyume na Nabii, hivyo niliwaambia, 'Inaweza kuwa , kama atawataliki ninyi nyote, kwamba Allah atampa yeye, badala yenu wanawake walio bora Zaidi yenu.' Hivyo Aya hii ilifunuliwa (66.5)." (al-Bukhari: vol. 6, book 60, no. 438) Mara tena, Allah alikuja kuokoa kwa Aya ambayo wazi wazi ilikusudia kwaonya na kuwaogopesha wanawake: *"Ingewezekana kama angewataliki ninyi (wote) kwamba Bwana wake atampa wengine badala yenu, wanawake bora kuliko ninyi, Waislamu (wanaomwamini Allah),waumini, wanaomtii Allah, humgeukia Allah kwa toba, kumwabudu Allah kwa ukunjufu, kufunga au kuhama (kwa ajili ya Allah),awali walioolewa na mabikira"* (**Q. 66:5**).

Mohamedi alijihalalishia yeye mwenyewe leseni kwa wanawake kwamba hakumruhusu mtu mwingine yeyote yule—kujamiiana na binti ambaye hajavunja ungo, kuchukua mke wa mwanao wa kuasili, kufanya tendo la ndoa na Dada, kufanya ngono nje ya ndoa, kuonyesha upendeleo kwa wake zake, na kuzidisha wanawake Zaidi ya kiwango kile ambacho Korani yenyewe imeruhusu mwingine yeyote—na yale yote yaliyoruhusiwa na ufunuo wa Kikorani kimsingi yalielekezwa kwenye tabia yake ya ziada (mara nyingi ufunuo uliotolewa"baada ya kweli" kuhalalisha kile ambacho tayari alikuwa ameshakifanya). Hata miongoni mwa wake zake mwenyewe, wivu ulizidi, hila, na upendeleo vinaonyesha tabia ya Mohamedi kuwa ni tabia ambayo siyo ya kuigwa na "*hakuwa mfano mzuri (wa tabia)*" (**Q. 33:21**). Gilchrist anaelezea kwa kifupi, "Badala ya kuwa mfano wa ni jinsi gani ndoa za wake wengi zinavyoweza kuwa na uhusiano mzuri, simulizi ya ndoa za Mohamedi zinakusudia kuimarisha ndoa ya mke mmoja Kibiblia. Hiyo swali la kujiuliza kwamba ni namna gani mwanaume anaweza kuwatendea wake zake wengi kwa usawa kwa kila mmoja, swali halisi ni kwamba ni jinsi gani atakavyowatendea sawa kwa ajili yake mwenyewe. . . . Imeendele bila kusema kwamba mume kwa kweli hawezi kupokea kwa ukweli kule kujitoa kwa mke wake kwake kama atakuwa anaugawanya upendo wake kwa jeshi la washiriki." (Gilchrist 1994: 84-85)

C. *Mohamedi na nguvu*

Kadiri nguvu za Mohamedi zilivyoongezeka, "Alihalalisha kila kitendo chake, bila kujali kilikuwa na sura mbaya kiasi gani, kama mtendaji wa Allah—na kujitangaza mwenyewe kama mfano mkamilifu kwa wanadamu wote. Hatimaye alijiinua mwenyewe kwenye kiwango ambacho 'Allah na mtume wake' wasingeweza kutofautishwa. Msemo 'Allah na mtume wake' ulienea kwenye sura zote za watu wa Medina—kwa upinzani mkali toka kwa watu wa Maka." (Sundiata 2006: 331, e.g., **Q. 3:31; 4:14, 65, 69, 80; 7:157; 8:20; 33:66, 71; 47:33; 48:10; 57:7, 28; 59:7; 64:8**) Kama ambavyo hadith inavyosema, "Chochote ambacho Mjumbe wa Allah alikiharamisha, ni sawa na kile ambacho Allah alikiharamisha" (at-Tirmidhi: 2664). Kwenye Hadithi nyingi zinamnukuu Mohamedi akitamka, "Yeyote anayenitii Mimi, Humtii Allah; na yeyote asiyenitii mimi, hamtii Allah" (Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 3; angalia pia vol. 4, book 4, no. 2859; al-Bukhari: 2956, 2957, 7137; Muslim: 1835a, b, c; an-Nasa'i: 4193, 5510). Alijiwekea pia utii kwa viwango vyake yeye mwenyewe vya kumuingiza Paradiso: "Mjumbe wa Allah alisema, 'Wafuasi wangu wote wataingia Paradiso isipokuwa wale watakaokataa.' Walisema, 'Ee Mjumbe wa Allah! Ni nani atakayekataa?' Alisema, 'Wote watakaonitii mimi wataingia Paradiso, na wale wote wasionitii mimi ndio wale ambao wamekataa (kuiingia).'" (al-Bukhari: 7280) Maadai yake yalikuwa wazi kiasi kwamba alidai kwamba alifanya maamuzi kwa kushauriana na Allah; Vivyo hivyo, wafuasi wake wasingeuliza chochote alichokiamua au kuwa na uchaguzi mwingine Zaidi ya kutii kila kitu alichokisema bila kuuliza maswali: *"Haikubaliki kwa Mwamini, mume au mke, wakati jambo limeamuliwa na Allah na Mjumbe wake kuwa na uchaguzi mwingine kuhusiana na uamuzi wao: kama mtu yeyote angeacha kumtii Allah na Mjumbe wake, kwa hakika angekuwa kwenye njia isiyo sahihi"* (**Q. 33:36**).

Aliwatawala Waislamu kabisa. Kujihakikishia utawala wake, Mohamedi aliondoka au kuipinga adhabu

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

ya kifo kwa Uislamu: “Ali aliwachoma baadhi ya watu na habari ikamfikia Ibn Abbas, ambaye alisema, Ningekuwa kwenye nafasi yake Nisingewachoma, kama alivyosema Nabii, ‘Usimwadhibu (mtu yeyote) kwa adhabu ya Allah.’ Bila shaka, Ningewaua, kwakuwa Nabii alisema, ‘Kama mtu yeyote Muislamu atakayeikataa dini yake, Mwueni.’” (al-Bukhari: 3017; angalia pia an-Nasa’i: 4019, 4059, 4061, 4062, 4063, 4064, 4721, 4743; at-Tirmidhi: 1402, 2158; Abi Dawud: 4352, 4765; Ibn Majah: vol. 3, book 20, no. 2533, 2534)

D. ***Mohamedi na mauaji***

Mohamedi alikazia matakwa yake kwa ukatili wa kutisha. Baada ya kuhamia Madina, Mohamedi alikuwa kiongozi wa jeshi lenye nguvu. Kwa asili yake, vita ni ukatili. Hata hivyo ukatili wa Mohamedi ulikuwa ni pamoja na kuwachinja wafungwa wasiokuwa na usaidizi na kuwauwa wasiokuwa na hatia kulikosababishwa na hasira yake mwenyewe. Kwa mfano, Baada ya vita vya mchanga mwaka AD 627 wakati makabila tofauti yalipoizingira Madina lakini yakashindwa na nguvu ya Mohamedi (tukio limerekodiwa kwenye **Q. 33:9-27**), Jeshi la Mohamedi liliwazunguka robo ya kabila la Wayahudi wa Banu Qurayza. Waliomba rehema au wapelekwe utumwani kama ambavyo Mohamedi aliwafanyia makabila mengine mawili baada ya vita vingine. Badala yake, Mohamedi alimteua Sa’d b. Mu’adh ambaye alitangaza hukumu “kwamba wanaume ni lazima wauawe, mali kugawanywa, na wanawake na watoto wachukulie kama mateka” (Ibn Ishaq 1955: 464). Ishaq anaeleza kwamba “baadaye Mtume alienda nje Madina sokoni (ambalo hata sasa soko hilo lipo leo) na kuchimba mashimo ndani yake. Baadaye aliagiza waletwe na aliwakatia vichwa vyao kwenye mashimo hayo walipokuwa wakiletwa kwake kwa mafungu. . . . Walikuwa kati ya watu 600 au 700 kwa wote, ingawa baadhi husema idadi ilikuwa kubwa kufikia kama 800 au 900.” (Ibid.; angalia pia Gilchrist 1994: 73-75) **Q. 8:67** (Hilali-Khan) wanathibitisha Imani yenye maadili ya Mohamedi ya kufanya *“mauaji makubwa (miongoni mwa maadui zake)”* Badala ya kuchukua *“wafungwa wa kivita (na kuwaachia huru kwa malipo).”* Mtazamo wa Mohamedi kuhusu wafungwa waliokamatwa ulionyeshwa wakati wa ushindi wake uliofuata kwenye vita vya Badr, alikuwa na mfungwa aliyeitwa ‘Uqba aliuawa. Ibn Ishaq anaelezea, “Wakati mtume alipoagiza yeye auawe, ‘Uqba alisema, ‘Lakini ni nani atakayewaangalia watoto wangu, Ee Mohamedi?’ ‘Kuzimu,’ alisema.” (Ibn Ishaq 1955: 308) Ukatili wake haukuishia vitani tu ulijumuisha pia masuala yake mwenyewe. Maisha ya Ibn Ishaq ni jinsi gani Kinana b. al-Rabi alivyodaiwa kuwa na baadhi ya hazina ambazo Mohamedi alizitaka. Ishaq anaeleza, “Hivyo mtume alitoa amri kwa al-Zubayr b. al-Awwam, ‘Mtese hadi atakapoeleza kile alicho nacho,’ hivyo alimwashia moto kwenye jiwe kubwa na kwenye kifua chake mpaka alipokuwa amekaribia kufa. Baadaye mtume alimpeleka kwa Mohamedi b. Maslama na alikikata kichwa chake.” (Ibn Ishaq 1955: 515) Mohamedi pia aliagiza kuuawa kwa Abu Rafi, Myahudi aliyeonekana kumwangukia Mohamedi kwa kubadilisha mwelekeo wa kuabudu kutoka Yerusalemu kuelekea Maka (Sundiata 2006: 351; angalia al-Bukhari: 4039, 4040; Ibn Ishaq 1955: 482-83).

Mohamedi aliamuru kuuawa kwa Abu ‘Afak na Asma, binti wa Marwan, walioonekana kwamba hawana “hatia” kubwa kuliko kila mmoja kuandika shairi kuelezea kutokuridhishwa kwao na Mohamedi kwa kuwaua watu mabli mbali (Ibid.: 675-76).Vivyo hivyo Mohamedi aliamuru kuuawa kwa maadui zake wengine. Kwenye mazingira haya aliwaruhusu wauaji kuwadanganya na kuwahadaa wahanga wao na kuwaua kwenye joto la damu. Mmoja wa wahanga hao ni Ka’b bin Ashraf, Myahudi, aliyeuawa kwa “hatia” ya kukusanya Aya za “matiti ambazo zilikuwa zinatumika kiasili kuwatukana wanawake wa Kiislamu” (Ibn Ishaq 1955: 366-68; angalia al-Bukhari: 3032, 4037; Muslim: 1801).

Sunan Abi Dawud anaelezea tukio lingine ambalo Mohamedi alikubali mauaji ya mama mjamzito kwa sababu tu alionyesha kutokukubaliana na kitendo cha Mohamedi kwa mkuu wa watumwa wake: “Mtu moja kipofu alikuwa na mama yake mtumwa ambaye alikuwa akimtukana Nabii na kumdhihaki. Alimkataza lakini hakuacha. Alimkemea lakini hakuacha tabia yake. Usiku mmoja alianza kumtukana Nabii na kumdhalilisha. Hivyo alichukua kisu cha mezani, alikiweka tumboni mwake, akakisukuma, na kumwua. Mtoto aliyekuja kati ya miguu yake alichafuka kwa damu iliyokuwa pale. Wakati asubuhi ilipowadia, Nabii aliarifiwa kuhusiana na hilo. Aliwakusanya watu na kusema: ‘Na waamuru kwa Allah mtu aliyetenda kitendo hiki na nawaamuru kwa mamlaka yangu kwake kwamba asimame.’ Alirukia kwenye shingo za watu na kutetemeka yule mtu akasimama. Alikaa mbele ya Nabii na kusema: ‘Mjumbe wa Allah! Mimi ni bwana wake; alikuwa akikudhalilisha wewe na kukudhihaki. Nilimkataza, lakini hakuacha, na Nilimkemea, lakini hakuacha tabia yake. Ninao watoto wawili kama mawe ya thamani kutoka kwake, na alikuwa mwenzi wangu. Usiku uliopita alianza kukudhalilisha na kukudhihaki wewe. Hivyo nilichukuwa kisu cha mezani, nikakiweka tumboni mwake nikakisukuma hadi nilipomwua.’ Kwa haraka Nabii alisema: ‘Ee kuwa shahidi, hakuna kisasi kitakacholipwa kwa ajili ya damu yake.’” (Abi Dawud: 4361) Aina hii ya vitendo inaonyesha moja kwa moja tabia ya Mohamedi na Unabii wake: “Nabii wa kweli wa Mungu anaweza kuidhinisha mauaji ya damu ya baridi ya Mama na Mtoto wake? Mauaji ya mtoto asiye na hatia hayakuwa kitu kwake? Mauaji ya watu wawili

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

yamefanyika na Mohamedi wala halikumsumbua wala kulichunguza kugundua kama muuaji alikuwa akidanganya ili kukwepa adhabu." ("Korani kukosa sifa" 2013: Mohamedi alijikosesha sifa yeye mwenyewe ya kuwa Nabii wa kweli)

Haya hayakutengwa na matukio yasiyo ya kawaida. Nehls na Eric wanaeleza, "Wakati tukijifunza juu ya maisha ya Mohamedi, tuligundua kwamba aliamuru kwa uchache mauaji 27 " (Nehls na Eric 2009: 33; angalia pia Sundiata 2006: 349-61; Gilchrist 1994: 63-77). Hatimaye, kama ilivyoelezwa hapo juu, aliamuru mauaji ya yeyote yule atakayeuacha Uislamu (al-Bukhari: 3017; angalia pia Muslim: 1676c; an-Nasa'i: 4016, 4019, 4058, 4059, 4061, 4062, 4063, 4064, 4721, 4743; at-Tirmidhi: 1402, 1413, 2158; Abi Dawud: 4352; Ibn Majah: vol. 3, book 20, no. 2533, 2534; vol. 3, book 21, no. 2659, 2660). Aliongeza kwamba "hakuna Muislamu atakayeuawa kwa kumwua asiyeamini " (an-Nasa'i: 4744; angalia pia 4735, 4745, 4746; al-Bukhari: 111, 6903, 6915; Abi Dawud: 2751; at-Tirmidhi: 1412; Ibn Majah: vol. 3, book 21, no. 2658). Yupo hata mmoja atakayesema kwa unyofu kwamba huu "*ni mwelekeo mzuri (wa tabia)*"? Iwe ndiyo au siyo nzuri, huu ndiyo ulikuwa mwelekeo wa tabia ya Mohamedi, na inaushawishi Uislamu na Waislamu hadi leo.

E. *Hitimisho*

Kwenye maeneo yote haya makuu ya maisha tumeangalia, utofauti uliopo kati ya Mohamedi na Yesu Kristo yamewekwa wazi na kwa kina. Tabia halisi ya Mohamedi kwa wazi imefunuliwa baada ya kupata nguvu kule Madina. Wakati alipokuwa na uwezo wa kufanya hivyo, Mohamedi alizindua fursa maalum ya kujipatia utajiri yeye mwenyewe na hata aliagiza al-Zubayr b. al-Awwam kuteswa na kukatwa kichwa ili apate pesa. Kwa upande mwingine Yesu alisema, *"Mbweha wana pango, na ndege wa angani wana viota; lakini Mwana wa Adamu hana pa kulaza kichwa chake"* (**Math 8:20; Luka 9:58**). Aliingia Yerusalemu kwa mara ya mwisho na punda wa kuazima (**Math 21:1-6; Marko 11:1-6; Luka 19:29-35**) na alikula chakula chake cha mwisho kwenye chumba cha kuazima (**Math 26:17-19; Marko 14:12-16; Luka 22:7-13**). Kwa kurudia rudia Yesu alifundisha juu ya hatari ya kupenda fedha na jinsi inavyomgeuza mtu kwenye kumwabudu Mungu (e.g., **Math 6:19-24; 13:7, 22; 19:16-26; Marko 4:7, 18-19; 10:17-27; Luka 8:7, 14; 12:13-34; 16:1-13; 18:18-27**). Alifundisha, *"Ni heri kutoa kuliko kupokea"* (**Matendo 20:35**; angalia pia **Math 5:42; Marko 12:41-44; Luka 6:30, 38; 21:1-4**). Na maisha ya Yesu yalifanana na mafundisho yake; alitoa kila alichokuwa nacho, hata kile ambacho yeye mwenyewe hakuwahi kukimiliki (nguo aliyokuwa ameivaa, **Math 27:35; Marko 15:24; Luka 23:34**)—kwa kweli alitoa maisha yake—kwa sababu ya wengine.

Mohamedi hakufungamana na sheria alizoziweka kuhusiana na ndoa na kujamiiana lakini badala yake alimchukuwa mwanamke yeyote aliyemtaka bila kujali kama alikuwa mtoto akichezea mwanasesere au mke wa mwanae mwenyewe. Alionyesha upendeleo miongoni mwa wakeze na Masuria kilichopelekea wivu kwenye ndoa na mafarakano. Kwa maana nyingine, kinyume na ndoa za wake wengi za Kiislamu na fursa maalum ya ndoa nyingi za Mohamedi, Yesu alifundisha kwamba Mungu alisimika *"Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mke . . . na hao wawili watakuwa mwili mmoja; hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja"* (**Marko 10:6-8; Math 19:4-6**). Zaidi, kinyume na nia ya ubinafsi ya Mohamedi juu ya wanawake na kijamiiana, Yesu alisema, *"lakini mimi nawaambia, Kila mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake"* (**Matt 5:28**). Mtu mmoja anaweza kuuliza kiuhalisia ninani ambaye maadili ya ndoa na mahusiano ya kujamiiana aliye bora, wakueleweka, na mwenye upendo wa kweli.

Mohamedi alijichukulia kwa nguvu zote na kwa ajili yake mwenyewe. Aliasisi sheria kwa wengine ambazo hazikutenda kazi kwake na kuwatishia wale wote waliompinga kwa kuwaua kimwili na kuwahukumu hukumu ya milele kuzimu. Kwa maana nyingine, Usiku kabla ya Yesu kukamatwa ili kuuawa aliwaosha wanafunzi wake miguu, kitendo ambacho kingefanywa na mtumwa wa nyumbani. Aliwaambia, *"Basi alipokwisha kuwatawadha miguu, na kuyatwaa mavazi yake, na kuketi tena, akawaambia, Je! Mmeelewa na hayo niliyowatendea? Ninyi mwaniita, Mwalimu, na, Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na Mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi."* (**Yohana 13:12-15**) Wakati wawili wa wanafunzi wake wakitafuta jinsi ya kumtendea kwa uzuri zaidi, Yesu akiwaambia, *"Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu yeyote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi."* (**Math 20:25-28**; angalia pia **Marko 10:42-45; Luka 22:25-27**) Kwenye tukio jingine aliwafundisha wanafunzi wake, *"Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote"* (**Marko 9:35**; angalia pia **Math 20:16**). Tena , mtu anaweza kuuliza swali gumu ni yupi kati yao (Yesu na Mohamedi) ambaye maadili ya nguvu/mamlaka yanaelekeza kwenye furaha na ubora wa Utu.

Mohamedi aliwatendea wale waliompinga, kwa ukatili uliopitiliza hata wale ambao kwa uchache sana

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

waliandika hata vifungu vya ushairi tu kuelezea mawazo yao juu ya vitendo vya kiongozi wao ambavyo hawaridhiki navyo. Aliwaamuru washiriki wake kudanganya, kuhadaa, na kuwaua wale ambao hawampendi Mohamedi, nayeye mwenyewe aliwachinja mamia ya watu wasio na msaada. Kwa namna nyingine, Yesu alisema, *"Heri wenye rehema; Maana hao watapata rehema"* (**Math 5:7**). Baadaye kwenye ujumbe wake alifundisha, *"Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, USIUE, na mtu akiua, itampasa hukumu. Bali mimi nawaambieni, Kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto."* (**Math 5:21-22**) Tena aliendelea kufundisha, *"Mmesikia kwamba imenenwa, UMPENDE JIRANI YAKO, na, Umchukie adui yako; lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi."* (**Math 5:43-45**) Mwishoni mwa mafundisho yake hayo Yesu alihitimisha kwa maneno machache *"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii"* (**Math 7:12**; angalia pia **Luka 6:31**). Yesu hakufundisha haya kwa wengine tu, lakini alikiishi kile alichokifundisha. Wakati Yesu anakamatwa, mwanafunzi wake Petro alivuta upanga wake na kukata sikio la kulia la mtumwa wa kuhani mkuu; Lakini Yesu alisema, *"'Yesu akajibu akasema, Mwe radhi kwa hili. Akamgusa sikio, akamponya."* (**Luka 22:51**; angalia pia **Math 26:51-52; Marko 14:47; Yohana 18:10-11**) Tena, ni wazi kwamba maadili ya maisha ya Yesu hutuongoza kwenye usuluhishi na Amani miongoni mwa watu, Wakati ambapo maadili ya maisha ya Mohamedi yanatuongoza kwenye hasira, chuki, ukatili na vita.

Hakuna hata eneo moja ambalo tunaweza kusema kwamba Mohamedi alilazimishwa na mazingira yaliyozidi uwezo wake wa kujizuia kutenda matendo yote maovu aliyoyatenda. Wakati alipokuwa akitenda matendo hayo alitumia nguvu zake zote. Vivyo hivyo, matendo ya mtu hufunua kile kilichopo kwenye moyo wake—moyo wake wa kweli—kama vile ambavyo Yesu aliwafundisha: *"Akasema, Kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi."* (**Marko 7:20-23**; angalia pia **Math 15:19-20**) Mohamedi alikuwa akishtakiwa na dhamira kwenye kila neno ambalo Yesu aliliorodhesha ambalo linaweza kumnajisi mtu; hayo machache tuliyoyaangalia hapo juu kuhusu maisha yake na kufunuliwa kwa tabia yake, kwa kiwango cha juu, Mawazo maovu ya Mohamedi, uasherati, mauaji, kutamani, uovu, hadaa, uzinzi, na kiburi. Dhambi hizo siyo suala dogo tu kwa "kiwango cha chini"—siyo "nafasi ya kosa dogo" (Dirks 2008: 187) au "makosa yasiyotegemewa kwenye hukumu iliyotolewa na nabii asiye na dhambi" (Emerick 2004: 201). Badala yake, kile ambacho Korani na hadithi zenyewe zilivyoelezea hapo juu ni dhambi za kina za tabia ya Mohamedi kwa sababu zinaandaliwa "*kutoka moyoni* na *kutoka ndani yake*". Hivyo basi zinafunua uhalisia wa asili yake. Kwa namna nyingine, hata Korani inatambua kwamba Yesu hakushtakiwa na dhamira kwa hayo au dhambi nyingine yeyote na hakuwa na hata kosa moja. Asili na tabia ya Yesu ilikuwa safi na zilikuwa njema kwa ujumla wake—na maisha yake yalidhihirisha hilo. Tukiyalinganisha maisha ya Yesu na Mohamedi na tabia zao kwa pande zote, ni wazi kwamba ni ya nani yanayodhihirisha *"mfumo mzuri wa mwenendo"* (**Q. 33:21**) na wa nani haudhihirishi.

Tukio hili, kama mengine kwenye maisha yake yote, linafunua kwamba siyo Mohamedi wala "ufunuo"wake vilivyoinuka Zaidi ya kiwango cha ufahamu wake na uelewa wa mazingira yake kwenye karne ya saba ya Arabia. Vivyo hivyo, aliwachukia, walioonekana kuwa maadui zake, na kuwaamuru wafuasi wake kuwaua wale ambao hawaukumbatii Uislamu. Kwenye tofauti ya wazi, Yesu hakuwahesabu kuwa maadui wale ambao hawakumkubali lakini aliweza kuwasamehe maadui zake halisi, na aliwafundisha wafuasi wake *"kuwapenda maadui na kuwaombea wale wanaowaudhi/wanaowatesa"* (**Math 5:44**). Yesu alijidhabihu mwenyewe kwa ajili ya wengine; Mohamedi aliwadhabihu wengine kwa ajili yake. Hata mahusiano yake na wafuasi wake yalitofautiana: Yesu hakutuita sisi "watumwa" kama ifanyavyo Korani (e.g., **Q. 2:23; 4:172; 14:31; 17:53; 25:63; 39:10, 53**), lakini alituita "marafiki" zake (**Yohana 15:15**) na "wana" (**Math 5:9**). Bila kujali kuwa alikuwa Mwana wa Mungu, Yesu aliosha miguu ya wanafunzi wake. Kuna mtu aliyewahi kuwaza kwamba Mohamedi angeweza kufanya hivyo? Ni kweli kwamba wafuasi wa Yesu wote siyo wakamilifu, wa kupendeka, na kusameheka—lakini Yesu alikuwa hivyo. Ni ukweli pia kwamba wafuasi wa Mohamedi siyo wote wenye vurugu, chuki, na makatili—lakini Mohamedi alikuwa hivyo. Mtu mmoja angeuliza: Ulimwengu ungekuwa bora, wenye Amani tele na mahali pa kupendeza kama watu wangefuata mafundisho ya Yesu au ya Mohamedi?

3. DHAMBI NA WOKOVU

I. Utangulizi

Sultan Mohamedi Khan alianzisha mjadala ambao uliigusa mioyo ya dini zote, ikiwa ni pamoja na Uislamu na Ukristo: "Ninavyoendelea kufikiri zaidi, ndivyo ushahidi unavyoendelea kuwa dhahiri kwangu

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kwamba wokovu ni pumzi ya muhimu ya dini na msingi wa lazima. Bila huo dini hiyo siyo dini. Zaidi sana, Nimetafakari kwamba kila mtu amkubali mtu huyu, kama jina lake linavyoashiria, ni kifungu cha kusahauliwa, kutokutii, na kutenda makosa. Maisha yake hayakubakia kuwa masafi tu kama kabisa kwa uhakika kutokuwa na hata na doa la dhambi. Dhambi ilikuwa asili ya pili ya mwanadamu. Ni ukweli kusema kwamba 'kujikwaa ni kwa mwanadamu'. Swali ni jinsi gani mtu anaweza kuepuka uwajibikaji na adhabu? Jinsi gani mtu anaweza kuokoka? Uislamu je wana nini cha kusema kuhusiana na hili? Na ujumbe wa Ukristo ni upi? Ni kazi yangu kuchunguza suala hili muhimu kwa ukunjufu na bila kuwa na upendeleo wa upande mmoja." (Khan 1992: 11)

Yapo mambo mengi ya kufanana baina ya Ukristo na Uislamu kuhusiana na suala la dhambi, lakini zipo pia tofauti za wazi. Nafasi ya Ukristo na Uislamu kuhusiana na dhambi na wokovu inaashiria nafasi zao kumhusu Yesu Kristo: tofauti baina ya wawili hawa zinaenda kwenye kiini cha jambo lenyewe—asili ya dhambi, asili ya mwanadamu, na dawa ya dhambi (jinsi ya kuokoka).

Khan anajinyooshea kidole yeye mwenyewe (na kwetu sisi) kwanini masuala haya ni ya muhimu sana: "Sultan, anatafakari kwamba wewe ni mtoto wa muda na ulimwengu unapita. Wakati utakapokufa, nchi yako na urithi wako havitakuwa na faida kwako; wala familia yako na marafiki hawatakuwa na msaada kwako. Vyote hivi ni mali ya ulimwengu huu pekee. Ni Imani yako tu ndiyo itakayokwenda Zaidi ya kaburini. Kwa hiyo siyo busara kusahau maisha ya milele na furaha ya Kiroho kwa ajili ya maisha haya ya kupita." (Ibid.: 29) Kwa sababu ya umuhimu wa suala hili na " kazi ya kuchunguza suala hili muhimu kwa ukunjufu na bila kuwa na upendeleo wa upande mmoja," tutajaribu kufanya hivyo kwenye sura hii.

II. <u>Dhambi na Wokovu Kulingana na Ukristo</u>

Biblia imeliweka suala hili kwa mapana na uthabiti (i.e., kweli zimeunganishwa kwa kina na kwa uthabiti) maelezo ya asili ya dhambi, asili ya uanadamu, na kuokolewa (wokovu) kwa mwanadamu kutoka kwenye tatizo la dhambi. Muundo mkuu uko kama ifuatavyo:

A. *Maana ya dhambi*

Msisitizo wa Kibiblia kuhusiana na dhambi unaanzia kutoka kwenye uhusiano wa Mungu na viumbe wake. Hivyo, chanzo cha dhambi kulingana na Biblia ni kile ambacho John Stott anachokiita "kutokuwa na Mungu na kujitegemea mwenyewe kwa dhambi" (Stott 1986: 90). Kwa maneno mengine, "Kila dhambi ni kufunguliwa kwa kile Yesu alichokiita 'amri iliyo kuu na ya kwanza' [*"MPENDE BWANA MUNGU WAKO KWA MOYO WAKO WOTE, NA KWA ROHO YAKO YOTE,NA KWA AKILI ZAKO ZOTE."* (**Math 22:36-38; Marko 12:28-30**)], siyo tu kwa kushindwa kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, lakini kwa matendo kukataa kumtambua na kumtii kama Muumbaji na Bwana wetu. . . . Mbaya zaidi, tumethubutu kutangaza kujitegemea wenyewe, kujitawala, ambapo ni kudai nafasi ambayo Mungu mwenyewe ndiye anayeimiliki. Dhambi siyo kutubia ufa kutoka kwenye viwango vya kuamini; Kiini chake ni chukizo kwa Mungu (Warumi. 8:7), kuanzisha matendo ya uasi kinyume na Mungu." (Ibid.) Maandalizi haya ya dhambi hututenga sisi na Mungu (**Isa 59:1-2**)

Kwa sababu ya hili hakuna chakushangaza kwamba kwenye Amri Kumi za kwanza mbili zimeandaliwa maalum na moja kwa moja kinyume na *ibada ya sanamu,* i.e., kuinua chochote au yeyote Zaidi ya Mungu (**Kut 20:1-6; Deut 5:6-10**). Martin Luther alieleza: "Wale wote ambao kwa wakati wote hawamwamini Mungu na kwenye kazi au mateso,maisha na kifo, kuamini kwenye kibali chake, neema na mapenzi mema, lakini hutafuta kibali kwenye vitu vingine au kwao wenyewe, hawaishiki Amri ya kwanza, na huabudu sanamu halisi, hata kama wakizishika Amri zingine zote, na kwa nyongeza maombi yote, kufunga, kutii, uvumilivu, usafi na kutokuwa na hatia na yale yote ambayo watakatifu waliyoyasema. Kazi iliyo kuu haipo, bila hiyo zingine zote hazina maana lakini ni dihaka za kawaida, kujionyesha na kujifanya, bila kuwa na matokeo yoyote kwao." (Luther 1520: X) Timothy Keller aliliweka hili hivi, "Iliyo ya kwanza kabisa kwenye Amri kumi ni 'Usiwe na miungu mingine Zaidi yangu [**Kut 20:3; Kumb 5:7**].' Hivyo, kulingana na Biblia, njia ya msingi ya kuifafanua dhambi siyo tu kwa kufanya mabaya, lakini kwa kufanya vitu vizuri kuwa kwenye *hatima* ya vitu. Ni kutafuta kuanzisha ufahamu wa kibinafsi kwa kufanya vitu vingine kuwa vya msingi kwa umuhimu wako, kusudi, na furaha kuliko uhusiano wako na Mungu." (Keller 2008: 162) Hivyo, kwa ufahamu halisi kimsingi ambaye hujeruhika zaidi tunapotenda dhambi ni Mungu. David alilitambua hili wakati alipokuwa anatubu alipotenda dhambi ya uzinzi na Bathsheba na kumlilia Mungu, *"Nimekutenda dhambi Wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako."* (**Zab 51:4**). Hata hivyo, Kwa sababu Mungu wakati wote ni mwema na ni mtawala wa ulimwengu wote, kutenda dhambi kinyume chake ni lazima kutagusa kila kitu kinginecho, i.e., dhambi hutuumiza sisi wenyewe, huwaaumiza wengine, na huumiza ulimwengu.

Mungu *"hamjaribu mtu"* kutenda dhambi (**Yak 1:13**); badala yake, msingi wa mwanadamu wa kujiamini mwenyewe na kujitenga na Mungu kunatuongoza kwenye kila dhambi maalum, i.e., kila uovu wa

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kitabia itendwayo na watu (angalia **Yak 1:13-15**). Dhambi hizo zaweza kuwa za kutokujizuia, kushindwa kutenda kile ambacho Mungu ameagiza (i.e., dhambi ya *uasi*; e.g., **Luka 12:47; Yak 4:17**), au dhambi yaweza kuwa ya matendo, kufanya kile ambacho Mungu amekataza (i.e.,dhambi ya *uasi*; e.g., **Kut 20:13-16**). Kwa sababu dhambi huanzia kwenye mahusiano ya watu na Mungu, dhambi hukaa siyo tu kwenye matendo ya nje lakini pia nia ya ndani na tabia ya moyo: kile kinachoelezwa nje kwa maneno na matendo ni kiashiria cha kile kilichoko ndani kwenye moyo wa mtu (**Kut 20:17; Mith 23:7; Math 5:21-22, 27-28; Marko 7:20-23**). Kwa hiyo, Ukristo hauwezi kupunguzwa na orodha ya "nini cha kufanyika na nini kisifanyike."

B. ***Asili ya dhambi na madhara yake kwa watu***

Kwenye historia ya mwanadamu, **Mwanzo 3** inaelezea kwamba dhambi ilianzia kwenye bustani ya Edeni wakati Shetani alipomjaribu Hawa; wote Adamu na Hawa hawakumtii Mungu na wakala kutoka kwenye tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Dhambi ya Adamu na Hawa ilileta madhara kwao wenyewe kisaikolojia (**Mwanzo 3:7**), kwa kibinafsi (**Mwanzo 3:16**), na uhusiano na Mungu (**Mwanzo 3:8-10**). Kwa nyongeza, kulingana na mtazamo wa Kibiblia ufahamu wa wanadamu wote ulikuwa kwenye ile hali ya"Adamu" (**Warumi 5:12-19; 1 Wakor 15:22**). Hivyo, Dhambi ya Adamu na Hawa ilileta madhara kwa kila mmoja wetu kwa historia yote na kuleta matokeo mabaya kimaadili na kitabia kwa asili ya mwanadamu. Hiki ndicho kile kinachojulikana kama "Anguko" la mwanadamu. Dhambi iliingia kwa Adamu na Hawa baada ya anguko, na kwa kila mwanadamu kwa kuwa Adamu na Hawa walizaliwa kwenye hali ya udhaifu kimaadili—maandalizi ya ndani ya kutenda dhambi —kinachofanya kutambuliwa kwa dhambi ulimwenguni kote kama maisha ya watu (e.g., **Mwanzo 8:21; Zab 51:5; 143:1-2; Yer 17:9; Marko 7:20-23; Warumi 3:9-18, 23; 5:12-14; 7:14-24**). Kwa kweli dhambi inakaa ndani ya watu; ni "sheria" au nguvu ambayo inatenda kazi ndani ya kila mtu (**Warumi 7:5, 8-11, 14-24; Wagal 5:17; Waeb 3:12-13**). Mungu alimwonya Adamu kwamba tunda lililokatazwa kwa hakika atakufa (**Mwanzo 2:17**). Kanuni iyo hiyo inatumika kwa watu wote: *"Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi"* (**Warumi 5:12**).

Hili ni fundisho la "dhambi ya asili." "Dhambi ya asili siyo ile dhambi ambayo Adamu na Hawa waliitenda. Hayo yalikuwa ni *matokeo* ya dhambi ya kwanza. Dhambi ya asili ina nafasi kwenye hali yetu ya dhambi, uovu wetu wa dhambi, kutoka kwenye hisia zetu ambazo kwazo dhambi hutenda kazi. Kwa maneno mengine, *tunatenda dhambi kwa sababu sisi ni wenyewe dhambi.* Sisi siyo wenye dhambi kwa sababu tumetenda dhambi. Kwa kuwa anguko la mwanadamu sasa ni asili ya kila mwenye mwili hutusukuma na kutupelekea kutenda dhambi." (Sproul 2002: 34, fafanuzi imeongezwa.) Uovu wetu wa ndani ni ule ambao hata matendo yetu mema siyo yaliyosafi lakini yanakubalika, kwa kiwango kimoja au kingine, madoa ya ubinafsi wetu, kujitafutia utukufu wetu wenyewe, au yanasukumwa na mambo kama vile woga, dhamira, kiburi, choyo, etc. Vivyo hivyo, dhambi inaweza kuelezewa kimsingi kwa njia mbili tofauti: kama vile "kuwa vibaya sana na kuvunja sheria zote au kuwa nzuri sana na kuzishika sheria zote na kuwa wenye haki binafsi" (Keller 2008: 177). Hii ndiyo sababu Isaya anasema kwamba *"na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi"* (Isa 64:6).

Zaidi, uovu wetu ni ule ambao hatuwezi kuvifikia viwango vyetu wenyewe kikamilifu, ila Mungu pekee. Kuzungumza Kiroho, uovu wetu ni kwamba "kila mtu aliyezaliwa ulimwenguni humu amechafuliwa na anguko kiuadilifu na kimaadili kwa wanadamu wote, na watu hawana nguvu ya kujijenga wenyewe , mpaka waokolewe na Mungu" ("Dhambi ya asili" n.d.: Utangulizi; angalia **Yohana 3:3, 5; 6:44, 65; 8:34; Warumi 6:16-17, 20; 8:6-8; 1 Wakor 2:14; Waef 2:1-3; 8-9; Waeb 11:6**). Kwa sababu dhambi ni sehemu ya asili itendayo kazi ndani yetu ambayo hututenga na Mungu na kuharibu hata matendo yetu mema ya nje, Biblia kwa usahihi inaeleza watu kuwa "watumwa wa dhambi" (**Yohana 8:34; Warumi 6:6, 16-17, 20; 7:14**). Hivyo, *"kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Hakuna mwenye haki hata mmoja. Hakuna afahamuye; Hakuna amtafutaye Mungu. Wote wamepotoka, wameoza wote pia; Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja."* (**Warumi 3:10-12**) Bila Mungu kuingilia kila mtu angebaki *"Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu;"* (**Waef 2:1**).

C. ***Kutokuwezekana kwa mtu kujiokoa mwenyewe kwa matendo yake mema***

Kila mmoja wetu anaujua moyo wake kwamba tunalo tatizo la kimsingi ndani yetu ambalo hatuwezi kuliondoa/kulifuta. Watu wengi hujaribu kudhoofisha umuhimu wa hili kwa kusema maneno kama vile "kukosea ni kibinadamu." Hata hivyo, ni lazima kuangalia kwamba mahusiano yetu na Mungu yakoje. Utakatifu wa Mungu ndio msingi. Dhambi ni kinyume cha utakatifu wake. Kinachoweza kuelezwa kwa karibu na utakatifu wa Mungu ni Hasira yake. Hasira ya Mungu ni "majibu matakatifu kwa matendo maovu". . . . Kilicho muhimu kwenye wazo kuu la Biblia kuhusu utakatifu na hasira ya Mungu ni ukweli kwamba haviwezi kuishi

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

pamoja na dhambi. Utakatifu wa Mungu huifunua dhambi; hasira yake hupingana nayo. Hivyo dhambi haiwezi kumfikia Mungu, na Mungu hawezi kuivumilia dhambi." (Stott 1986: 102, 103, 106; angalia **Hab 1:13; Warumi 1:18**)

Yapo matokeo ya muhimu kwenye haya yote, yanayoitwa, "Mungu hapendezwi na mawazo yetu maovu na tabia zetu asili ya utakatifu wake kwa kina huchukizwa na mambo hayo. Kama alivyo Mungu mkamilifu, hawezi kudharau uovu wowote. Uongo kidogo ni chukizo kwa mtu ambaye ni mkweli. Hisia ndogo sana za kujisikia kumchukia mtu mwingine ni kumpuuza yule mtu ambaye ni upendo. Kutokana na asili ya Mungu ya utakatifu na ukamilifu hawezi kujifanya kipofu kwa kutokuona tabia mbaya ya mwanadamu kama vile siyo kitu kwake." (Alexander 2008: 130) Hivyo hivyo, "Kama Mungu anaweza kuwa mkweli kwa asili yake ya haki, kila uovu ni lazima uadhibiwe. Kwa nyongeza, Kama Mungu atamhukumu na kumwadhibu Shetani, basi ni lazima wakati wote ahukumu na kuadhibu . . . kiumbe kingine chochote ambacho kitaasi kinyume na mamlaka yake ya Kiungu." (Ibid.: 131; angalia **Warumi 2:16; 2 Wakor 5:10; Waeb 9:27; Ufu 20:10-15**)

Watu wengi hufikiri kwamba Mungu atawakubali (kuwaokoa) kama wakitenda "matendo mema" ya kutosha" Wanafikiri, "Kama matendo yangu mema yatakuwa mengi kuliko matendo yangu mabaya, Nitakubalika!" Hata hivyo, mtazamo huo wa wokovu ni wa kimakosa na ulioshindwa kwa angalu sababu nne:

- Kwanza, kwa sababu Mungu mwenyewe ni Mtakatifu na mkamilifu kimaadili, hicho ndicho kiwango ambacho Mungu hutuchukulia (**Math 5:48**). Hata hivyo, "mara mtu anapotenda dhambi, hawezi kuwa mkamilifu" (Sproul 2002: 94; angalia pia ibid.: 53). Kama ambavyo John Stott alivyoonyesha, "Kama tungekuwa wa kusamehewa, ni lazima tulipe kile tunachodaiwa [angaliaAnslem 1903: I:11]. Hata hivyo hatuwezi kufanya hilo, kwetu wenyewe au kwa watu wengine. Utii wetu wa sasa na matendo yetu mema hayatoshelezi kwa dhambi zetu, Kwakuwa haya hata hivyo bado yanatuhitaji. Hivyo hatuwezi kujiokoa wenyewe." (Stott 1986: 119)
- Pili, hata matendo yetu mema yamechafuliwa na dhambi. Kwa kweli, kama tunatenda matendo mema ili kuepuka adhabu ya Mungu na Jehanamu, hilo pekee linafanya matendo yetu mema *yasiwe* "mema." Sababu ni hii kama kinachotusukuma ni kuepuka jehanamu kwa kutenda "matendo mema," basi matendo hayo kwa ufafanuzi ni, ubinafsi na kujitegemea mwenyewe, e.g., wakati tunapowasaidia maskini, kimsingi tunajisaidia *wenyewe* kuiepuka jehanamu. Hivyo, hakuna kiwango cha matendo mema, kwakuwa hayo yenyewe tayari yameghubikwa na dhambi ya ubinafsi, yaweza kuwa kwa ajili ya kufidia dhambi nyingine.
- Tatu, haiwezekani kabisa kujua kama mtu "ametenda vya kutosha" matendo mema au ametoa sadaka za kumtosheleza Mungu. Timothy Keller anaeleza, "Maadili na viwango vya kiroho vya kila dini viko juu sana, na Mafarisayo [i.e., wote wanaojaribu kujiokoa wenyewe kwa kufanya matendo mema na kutii sheria za dini] wanajua kwa kina kwamba hawaishi kikamilifu kwa viwango walivyojiwekea. Hawaombi mara zote kama ambavyo wanatakiwa. Hawawapendi na kuwatumikia majirani zao kwa viwango viwapasavyo. Mawazo yao ya ndani siyo masafi kama ambavyo wanatakiwa." (Keller 2008: 178)
- Nne, hakuna kiwango cha matendo mema ambacho kinaweza kubadilisha asili ya dhambi na tabia ya dhambi kwenye mioyo yao. Hivyo, matendo mema hayabadilishi uovu, watenda dhambi kuwa wenye haki, watu watendao dhambi kwenye vithaminisho vyao; hubaki wakiwa watu wenye dhambi. Kama Mungu angewaruhusu watu wenye dhambi kuingia mbinguni na kwenye nchi mpya ambako watu wataishi milele (**Ufu 21-22**), mbingu na nchi mpya vingekuwa na uovu milele. Mungu asingekuwepo hapo kabisa, "dhambi haiwezi kumfikia Mungu, na Mungu hawezi kuivumilia dhambi" (Stott 1986: 106). Kwakweli, kuuruhusu uovu wa ndani wa mwanadamu na tabia ya dhambi, mbingu ingegeuzwa kuwa Jehanamu.

Kwa kuwa hatuwezi kujiokoa wenyewe, "wengine wanaweza kusema kuwa tatizo siyo kubwa sana kwa sababu Mungu kwa wema wake hataziangalia. Mungu angefanya hivyo kama tu angekuwa tayari kukubaliana na Uadilifu wake mwenyewe au kuidhabihu Haki yake." (Sproul 2002: 94) Hata hakimu wa kidunia asipoikaza hukumu yake lakini akamwacha mwenye hatia bila kumhukumu atajulikana ulimwenguni kote kwamba siyo mtenda haki.[11] Hii ndiyo sababu Mungu hawezi kusema tu, "Katika Rehema na Huruma zangu, Ninawasamehe

[11] Biblia inasema kwamba adhabu ya mwisho ya dhambi zetu kinyume cha Mungu ni kile ambacho kinaitwa *"ziwa la moto"* au *"mauti ya pili"* (**Ufu 19:20; 20:6, 10, 14-15**). Wakati baadhi ya vikwazo kwenye wazo hili, kwa uchache vipo vipingamizi viwili kwa majibu haya: (1) haki, na (2) kuheshimu utu wa mtu na uchaguzi wake. Nicola Yacoub Ghabril anaelezea mwitiko wa kwanza: "Sheria za kijamii na za Kiislamu zinaeleza kwamba adhabu ya kosa au jinai lazima iwe kali au kulingana na dhambi aliyoitenda. Kwa mfano, kama mwanafunzi shuleni amemtukana mwanafunzi mwenzake, huadhibiwa kidogo, pale ambapo kama angemtukana mwalimu angefukuzwa shuleni. Kwa vigezo vya kisheria, kama mtu akimtukana yule ambaye wana umri sawa au kwa namna moja au nyingine wanalingana huhesabiwa kuwa ni kosa, lakini kama akimtukana Hakimu adhabu yake huwa ni kubwa. Hata hivyo, kama akimtukana Mfalme hukumu yake huwa ni kubwa zaidi. Lakini akitenda dhambi kinyume na Mungu, ambaye ni Ukuu wake haufananishwi na wa yeyote yule na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

enyi watenda dhambi." Kufanya hivyo kutakuwa siyo kutenda haki na kutawafanya watenda dhambi kuishi na kuichafua mbingu nan chi mpya milele. Kwa namna nyingine, kama ambavyo tumezungumza hapo juu, wanadamu hawawezi kujiokoa wenyewe. Kwa sababu wanadamu wote ni waovu kwenye mioyo yao na watenda dhambi kwa mawazo yao mbele za Mungu, maneno, na matendo, hakuna kiwango cha "matendo mema," kushika sheria, au matendo mengine ambavyo vyaweza kuwa fidia kwa dhambi zetu. Hivyo, kama vikiachwa kwao wenyewe, wanadamu wote wametenda na wanastahili tu hukumu ya Mungu. Hili lingesababisha kuwaza sana juu ya tatizo: "Mwanadamu kama mtenda dhambi anadaiwa na Mungu kwa ajili ya dhambi zake kile ambacho hawezi kukilipia, na hawezi kuokolewa asipolipa" (Anselm 1903: I:25).

D. ***Wokovu kulingana na Ukristo: kile Kristo alichokikamilisha pale msalabani***

Ni Ukristo pekee wenye majibu ya kuaminika na ya wazi kwa tatizo hilo hapo juu. Ukristo pekee ndio unaolitambua na kulichukulia kwa umakini suala la "anguko" la mwanadamu, kimo cha dhambi, utakatifu na ukamilifu wa Mungu, kutokuwezekana kwa Mungu na dhambi kuishi pamoja, ukweli kwamba wanadamu wote wametenda na wanastahili hukumu kwa dhambi zao, na kutokuwezekana kwa wanadamu kwa jitihada zao kujiokoa wenyewe. Tofauti ya Ukristo ni Yesu; tofauti ya Ukristo ni msalaba. Keller anaelezea, "Imani zingine kubwa zinao waasisi ambao ni waalimu wa kuwaonyesha njia ya Wokovu. Ni Yesu pekee aliyedai kimsingi *kuwa* njia ya wokovu mwenyewe." (Keller 2008: 174)

Anselm wa Canterbury aliliweka hili kwa njia hii: Kwa sababu mwanadamu *hawezi* kutosheleza deni lake kwa Mungu, "hakuna hata mmoja isipokuwa Mungu mwenyewe *anaweza* kuleta utoshelevu huo. Lakini hakuna hata mmoja lakini mwanadamu ni *lazima* afanye hili, vinginevyo mwanadamu hawezi kuleta utoshelevu. Kama ikiwa ni lazima, kama ilivyoonekana kwamba ufalme wa mbinguni umeandaliwa kwa ajili ya wanadamu, na hili haliwezi kukamilika mpaka hapo ambapo utoshelevu uliosemwa hapo mwanzo utakapokamilishwa, ambao hakuna mtu awezaye isipokuwa Mungu na hakuna mwingine isipokuwa mwanadamu anatakiwa kukamilisha, ni lazima Mungu ambaye pia ni mwanadamu kulikamilisha hili. . . . Kwa hiyo basi, ili kwamba Mungu-mwanadamu afanye hili, ilikuwa ni lazima kwamba ili hili litendeke ni Mungu kamili na mwanadamu kamili awepo ili awe fidia kwa hili. . . . Kwakuwa ni hivyo basi, ni lazima kwamba Mungu-mwanadamu astahili kuikamilisha kila asili, siyo kwa ulazima mdogo kwamba asili zote hizi mbili kuungana ndani ya mtu mmoja, kama ilivyo kwa mwili huo huo nafsi hizo hukaa pamoja kwa kila mwanadamu; kwa vinginevyo haiwezekani kwa nafsi zote mbili kuwa Mungu kamili na mwanadamu kamili." (Anselm 1903: II:6-7) Yesu pekee ndiye aliyezifikia sifa hizo.

Ni kwa muujiza huu wa kuungana kwa Mungu na mwanadamu kwa mwanadamu Kristo kilichomwezesha Mungu kuistahimili na kuivumilia adhabu ya msalaba. Yesu aliyaishi maisha ambayo tunapaswa kuyaishi *kama wanadamu*: Kwa ukamilifu alimheshimu Mungu Baba katika kila kitu; *Alijaribiwa katika kila kitu kama tujaribiwavyo, wala hakutenda dhambi"* (**Waeb 4:15**). Hili lilimpa sifa ya kuwa

---

Mtakatifu, adhabu yake itakuwa kubwa kwa kiasi gani! Bila shaka atahukumiwa kwa mateso makali yasiyo na ukomo." (Ghabril 2003: 20)

Timothy Keller anaelezea mwitikio wa pili: "Kwenye Warumi 1-2 Paulo anaeleza kwa Mungu, kwenye hasira yake kinyume na wale wanaomkataa, 'huwaachilia' kwenye misukumo ya tamaa za dhambi za mioyo yao. . . . Kwenye Waefeso 4:19 inasema kwamba watenda dhambi hujitia wenyewe kwenye tamaa zao za dhambi. Inamaanisha kwamba adhabu mbaya Zaidi ambayo Mungu atawaadhibu wenye dhambi ni kuwaachilia kwenye tamaa za mioyo yao. Hili linamaanisha nini? Tamaa ya dhambi ya moyo wa mwanadamu ni kwa uhuru wake mwenyewe. Tunahitaji kujichagulia na kuziendea njia zetu wenyewe (Isaya 53:6). . . . Kuzimu ninini basi? Ni utendaji wa Mungu wa kutuachilia kuiendea njia ambayo tumejichagulia wenyewe kuiendea, kuwa wenyewe 'viongozi wa matakwa yetu, manahodha wa nafsi zetu wenyewe,' kwenda mbali na uongozi wa Mungu. Ni Mungu kutuachilia kwenye himaya ambayo tumejaribu kuipata kwa maisha yetu yote. . . . Wazo la Kuzimu halieleweki sana kwa watu kwa sababu wanaiona kama adhabu iliyo sawa na kwamba adhabu hiyo ingetolewa kwa kiwango cha uwiano mdogo, hatua za uongo zenye kikomo (kama vile kutokuukumbatia Ukristo.) Pia, kama vile hakuna mtu anayemjua mwenzake (hata wao wenyewe) ikionekana kwamba ni mbaya Zaidi na wanastahili jehanamu. Lakini mafundisho ya Kibiblia kuhusu Jehanamu yanajibu mitazamo yote miwili. Kwanza, yanatueleza kwamba baada ya maisha haya watu hupokea kile ambacho wao wenyewe wamekipa nafasi ya juu Zaidi ikiwa ni kumpa Mungu nafasi ya kuwa Bwana na Mwokozi wao au kuwa waokozi na mabwana wa maisha yao wenyewe. Pili, yanatueleza kwamba Kuzimu ni matokeo ya asili. Hata kwenye Ulimwengu huu ni wazi kwamba ubinafsi badala ya kumtanguliza Mungu humfanya mtu kuwa mwovu na kipofu. . . . Kwa namna nyingine, nafsi ile ambayo imeamua kuyaelekeza maisha kwa Mungu na Utukufu wake huelekea kwenye ongezeko la furaha na ukamilifu. Tunaweza kuziona 'njia walizojichagulia' hata kwenye maisha haya. Lakini kama Biblia inavyofundisha, nafsi zetu zitaendelea milele, hebu fikira ni wapi ambako aina hizi mbili za nafsi zitakakokuwa kwa mabilioni ya miaka. Kuzimu ni njia ambayo mtu hujichagulia kwa uhuru wake mwenyewe kuiendea milele. Tulitaka kukaa mbali na Mungu, na Mungu, kwa haki yake ya milele, alituongoza kule tulikotaka kwenda." (Keller 2009: sec.3)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

mwakilishi wetu, kuzichukua dhambi zetu mwenyewe na kulipia adhabu ambayo vinginevyo tungepaswa kulipia kitu ambacho kamwe tusingeweza (**Warumi 8:1-4; 2 Wakor 5:21; Wagal 3:13; Wakol 2:13-14; 1 Tim 2:5-6; 1 Pet 2:24**). Kama Keller alivyoeleza, "Mungu hakuachilia maumivu kwa mtu mwingine yeyote, lakini badala yake aliyastahimili maumivu, vurugu, na uovu wa ulimwengu yeye mwenyewe. Hivyo basi, Mungu wa Biblia siyo kama miungu ambayo hudai damu zetu ili kutuliza hasira zao. Badala yake, ni Mungu aliyekuwa mwanadamu na kujitolea damu ya uhai wake ili kuheshimu haki ya kimaadili na huruma za pendo lake ili kuuangamiza uovu wote bila kutuangamiza sisi wenyewe. . . . Kwanini *ilimpasa* Yesu afe ili kupatikana kwa msamaha wetu? Lilikuwepo deni ambalo lilipaswa kulipwa—Mungu mwenyewe alililipa. Kulikuwa na adhabu iliyopaswa kubebwa—Mungu mwenyewe aliibeba. . . . Haki na huruma hazikukosekana msalabani—zote zilitimizwa pamoja. Kifo cha Yesu kilikuwa ni lazima kama Mungu kweli atachukulia haki yake kwa umakini na bado aendelee kutupenda." (Keller 2008: 192-93, 197) Au, kama Sultan Mohamedi Khan alivyoliweka, "Mungu ni mwenye Haki na Rehema. Kama Kristo aliahidi wokovu bila Kuyatoa Maisha yake, hitaji la Rehema kwa hakika lingekuwa limekamilishwa. Ili kuweza kulitosheleza hitaji la Haki pia, Kristo alilipa fidia, ambayo ilikuwa ni damu yake ya thamani. Kwa njia hii Mungu aliudhihirisha Upendo Wake kwetu." (Khan 1992: 26) John Stott anaelezea kwa kifupi, "Moyo wa dhambi ni mwanadamu kuwa mbadala wake mwenyewe mbele za Mungu, wakati ambapo moyo wa Wokovu ni Mungu kuwa mbadala wa mwanadamu. Mwanadamu hujiinua mwenyewe kinyume na Mungu na kujiweka mwenyewe mahali ambapo ni Mungu pekee anayestahisili kuwepo; Mungu alijidhabihu mwenyewe kwa ajili ya mwanadamu na kujiweka mahali ambapo ni mwanadamu pekee aliyestahili kuwepo. Mwanadamu hudai Haki ambazo ni mali ya Mungu pekee; Mungu alizikubali adhabu ambazo zilimstahili mwanadamu pekee." (Stott 1986: 160)

Kristo alizibeba adhabu zetu msalabani ili tusikabiliwe na adhabu ya Mungu kwa dhambi zetu; alisahauliwa msalabani ili kwamba sisi tukubaliwe. Katika Kristo, tuko huru mbali na adhabu na makosa yetu ya dhambi kana kwamba tumejilipia fidia yote sisi wenyewe (**Warumi 6:3-7; Wagal 2:20**). Zaidi ya hayo, wakati tunapomkubali Kristo yeyote yaliyo kweli kwake, sasa huwa kweli kwetu: hakuyaondoa makosa yetu kwa kulipia dhambi zetu yeye mwenyewe, lakini pia alitupa sisi haki yake. Hivyo, ni ndani ya Kristo tu hatuhukumiwi, lakini tumekubalika kweli, kupendwa, na kuheshimiwa na Mungu.

Ni kwa kuyajua hayo hapo juu pekee kunakoelezea kilio cha Yesu pale msalabani, *"Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?"* (**Math 27:46; Marko 15:34**) Mtetezi wa Uislamu kwa hakika hakuelewa kabisa kilichokuwa kikiendelea wakati Yesu alipokuwa akitoa kilio hicho. Kwa mfano, Hilali anaeleza, "Hili ni tangazo la wazi la kutokuamini kulingana na mamlaka yote ya kitheolojia" (Al-Hilali 1998: 913). Abdullah Hadi Al-Kahtani alisema kwamba pale msalabani Kristo alikuwa akijaribu "kumdanganya Shetani" na "maneno hayo . . . yalisemwa ili kwamba Shetani angejua kwamba yeye [Yesu] alikuwa 'Mungu' au 'Mwana wa Mungu'" (Al-Kahtani 1996: 14-15). Siyo Hilali wala Kahtani ambao hata hawapo karibu na kuufikia ukweli. Kwa kile kinachoendelea?

Ukristo, tofauti na Uislamu, unatambua kwamba "Msamaha wakati wote huwa kwenye kundi la kugharimiwa kwa mateso" (Keller 2008: 193). Wakati mtu anakosewa na kuharibiwa, jambo la kwanza"ni kudai kwamba [mkosaji] alipie uharibifu. La pili kumkatalia kutokulipa chochote. . . . Kumbuka kwamba kwenye uchaguzi wowote gharama za uharibifu ni lazima kubebwa na *mtu fulani.* Kama atabeba gharama kwa matendo, lakini deni halitaishia hewani. . . . [Kumsamehe mtu kuna maanisha kwamba] unabeba na unalipia deni, *kuchukuwa gharama zake zote wewe mwenyewe* badala ya kuzipeleka kwa mtu mwingine" (Ibid.: 187, 189, fafanuzi imeongezwa) Kumsamehe mtu kuna maanisha kwamba siyo tu unagharimia kwa upotevu wa asili lakini pia kwamba unamkatalia mtenda makosa kulipia kile alichokitenda. Hivyo, msamaha wote unahusisha maumivu—na jinsi kosa na jeraha lilivyo, ndivyo ilivyo gharama na maumivu ya mtu anayesamehe.

Gharama kubwa ya dhambi zetu na kile zilichomgharimu Mungu kutusamehe sisi (i.e., *"Mwanae Mzaliwa wa pekee,"* **Yohana 3:16**) zilifunuliwa na Yesu pale msalabani. Kile Yesu alichokifanya pale msalabani ni kupokea hukumu, kulipia gharama, na kujichukulia adhabu kwa dhambi za wanadamu. Kwanini Yesu alilia, *Mungu wangu, Mungu wangu,kwanini umeniacha?"* John Stott anaelezea kwa kifupi: "Hali ya uhalisia wa kutengwa na hofu kuu vilichukuwa nafasi baina ya Baba na Mwana; vilikubaliwa kwa hiari na wote wawili Baba na Mwana; ni kwa kulingana na dhambi zetu na tuzo yake ya haki; na Yesu alielezea hili kwa giza kuu na hofu, kwa kusahauliwa na Mungu kwa , kunukuu mstari wa maandiko pekee ambao kwa usahihi alieleza kwamba umetimizwa kikamilifu" (Stott 1986: 81).

Kilio cha Yesu pale msalabani kinafunua jambo jingine: utii wake mkamilifu (**Wafil 2:8**). Kwa maisha yake yote ya hapa duniani Kristo mwenyewe alielezea kwa kurudia rudia kwamba hakufanya lolote kwa ajili yake mwenyewe lakini alifanya kile ambacho Baba angekifanya (**Yohana 5:19, 30; 6:38; 8:28; 12:49; 14:10**). Alilia kwa*"<u>Mungu wangu</u>"* linafunua mahusiano ya kina na Baba yake. Pale msalabani, Yesu alivumilia mateso na laana ya milele toka kwa Baba (**Wagal 3:13**); bado aliendelea kumtii Baba kwa vyote hadi mwisho. Mbali na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kuwa“tangazo la wazi la kutokuamini,” kilio chake kilinukuliwa kutoka **Zab 22:1**, zaburi ya Daudi, ambaye alikuwa nabii (angalia **Matendo 2:30**). Kwa kuinukuu zaburi hii kwenye mazingira hayo, Yesu alikuwa akisema kwamba **Zab 22:1** ilihusika na kwamba ilikamilishwa kwa kile kilichofanyika msalabani. Yesu alielewa kwa uhalisia kile kilichokuwa kinaendelea. Kwenye hali hiyo, alikuwa akisema, “Ninakuamini wewe Baba, Ninaamini kwenye mpango wako wa wokovu kwa nafsi zilizopotea, na Ninakupenda sana kiasi kwamba nitatii mapenzi yako yote, ingawa inamaanisha kutengwa kabisa na wewe na kuvumilia mateso ya kuzimu yaliyounganishwa na dhambi za wanadamu.”

Kile alichokifanya Kristo pale msalabani kinaonyesha, kwa njia ambayo hakuna dini nyingine ambayo inaweza kukielezea, jinsi ambavyo watu wanathamani kwa Mungu. Keller anahitimisha, “Yesu aliteseka pasi na kipimo kuliko nafsi nyingine yeyote ya mwanadamu kule kuzimu ya milele, bado alituangalia na kusema, ‘Ilikuwa inastahili hivyo.’ Ni nini kitakachotufanya sisi kujisikia wenye kupendwa na wa thamani Zaidi kuliko hiki? Mwokozi amewasilishwa kwenye Injili kwa mapana kupitia kwake kuzimu yenyewe bila ya kutupoteza sisi, na hakuna mwokozi mwingine aliyewahi kujionyesha na aliyetupenda sisi kwa gharama kama hiyo.” (Keller 2009: sec.4)

Kwa sababu Injili—na wokovu wa watu—msingi wake ni kile Kristo alichokifanya, wokovu “hautapatikana” kwa kutenda “matendo mema.” Badala yake, wokovu *ulitolewa* na Mungu kama *zawadi* ya *neema yake; unapokelewa* na watu *kwa Imani* kwenye Kristo pekee. Kama **Waef 2:8-9** inavyosema, *“Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.”* Kuokoka kunamaanisha kutubia dhambi zetu, kukubali kile Kristo alichokifanya kwa ajili yetu, na kumgeukia Kristo kama Bwana wa maisha yetu (**Math 11:28; Marko 1:14-15; Yohana 1:12; 3:16; 17:3; Matendo 26:20; 1 Yohana 1:8-9**). *Westminster Confession of Faith* (1646) kwa ufupi: “Kanuni ya imani itendayo kazi ni kukubali, kupokea, na kumwangalia Kristo pekee kwa kuhesabiwa Haki, kutakaswa, na uzima wa milele” (Westminster 1646: XIV:2).

E. ***Matokeo ya dhambi na wokovu kulingana na Ukristo***

Uelewa wa Biblia na ukweli kwamba Kristo aliishi maisha ambayo tunapaswa kuyaishi na kufa kifo ambacho tulipaswa kufa (i.e., kulipia gharama na kupokea hukumu na adhabu), ilikuwa na matokeo muhimu ambayo siyo ya kweli kwa dini nyingine yeyote.

1. <u>Fundisho la “anguko” la mwanadamu linawapa Wakristo msingi wa wazi wa kupambana na uovu.</u> Abbas Sundiata anaeleza, “Mtazamo wa kiulimwengu kuhusu Biblia unawafanya Wayahudi na Wakristo kung’ang’ana kinyume na madhara ya ulimwengu tunaouona kama umeanguka na usio wa kawaida. Tunang’ang’ana kwa sababu tunaamini kwamba tunalo jukumu la kutenda kwenye ukombozi wake. Mtazamo huo hutufanya tuweze kupambana na matatizo yaletwayo na ulimwengu usio wa kawaida kwa kuamini kwamba lipo suluhisho. Kwa wale walio na mtazamo huo wa dunia, kila kitu kina thamani na maana; muda ni muhimu na waweza kukombolewa badala ya kupotezwa au kuuruhusu tu upite, na kila mmoja anayo thamani kubwa kwa sababu anayo sehemu ya kutendea kazi kwa kazi hii ya ukombozi. . . . Hapana shaka kwamba fundisho la kuanguka la Wakristo wa Judeo linajifananisha na ukweli wa ulimwengu; linaeleza uwepo wa dhambi na uovu kwenye ulimwengu ulioumbwa na mtakatifu, mwema, anayetupenda, na Mungu mwenye nguvu; inathibitisha uhuru wetu wa kuchagua; linatueleza kile kilichofanyika kwa niaba yetu na Mungu badala yetu wenyewe na kututia moyo kujibidisha kubadilisha mazingira yetu wenyewe.” (Sundiata 2006: 213-14)
2. <u>Wale wote ambao wameungana na Yesu kwa Imani wanao uhakika wa Wokovu wao.</u> Kama wokovu ungetegemea hata sehemu ndogo tu ya jitihada zetu, tusingekuwa na uhakika kabisa kwamba “tumefanya vyakutosha” kuutimiza wokovu. Hata hivyo, Kwa sababu Mungu katika Kristo alifanya kwa ajili yetu kile ambacho tusingeweza kukifanya, Wakristo wanaweza kuwa na uhakika kwamba milele watabaki wameokolewa (angalia, e.g., **Yohana 3:36; 6:37, 47; 11:25; 1 Yohana 5:11-12**). Kwa sababu adhabu ya dhambi ilikwisha kulipiwa na deni lilikwisha kukamilishwa halitadaiwa tena kabisa kwa yeyote aliye katika Kristo.
3. <u>Kuokolewa na kuunganishwa na Kristo hubadili hali ya kisheria ya Wakristo.</u> “*Kwa uhakika* Msalaba hufungua nguvu ya dhambi, kuishusha hasira ya Mungu, kuosha hatia na madoa ya dhambi, huwarejeza Walioamini kwa Mungu, na kuufikia ushindi juu ya maadui wa kifo cha kiroho duniani” (Demarest 1997: 196). Pale msalabani, siyo tu kwamba dhambi zetu ziliwekwa juu yake, lakini pia haki yake iliwekwa juu yetu! Kama **2 Wakor 5:21** inasema, *“Yeye [Baba] asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi[Kristo] kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.”*Hili linahusika na suala la watu wenye dhambi kurithi mbingu na nchi mpya: yeyote aliye ndani ya Kristo *“nisiwe na haki yangu mwenyewe ipatikanayo kwa sheria, bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile*

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

itokayo kwa Mungu, kwa imani" (**Wafil 3:9**).

4. Kuokolewa na kuunganishwa na Kristo huwabadilisha Wakristo kutoka ndani. Wakati mtu anapokuja kwa Kristo, hupokea moyo mpya (**Ezek 36:26; 2 Wakor 3:3**), ufahamu wa Kristo (**1 Wakor 2:16**), na Roho kutoka kwa Kristo (**Ezek 36:26; Yohana 14:17**). Hivyo, chanzo cha ulinzi na nguvu ya kuishi mwenye haki kimsingi siyo ya nje (kufananishwa na sheria na sherehe za kidini) lakini ni za ndani—ni Yesu, kupitia neno lake, ufahamu, na Roho, ambaye sasa anaishi ndani na kuishi na watu wake. Kwa ndani maana yake ni waamini kupewa na Kristo, mchakato wa kuwatakasa na kuwabadilisha watu wa Kristo hauepukiki na huanzia ndani *"Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake [i.e., Yesu Kristo]"* (**Warumi 8:29**).

5. Kuokolewa na kuunganishwa na Kristo huwapa Wakristo mahusiano ya ndani na Mungu kupitia Kristo. "Injili ya Wakristo ni hii Mimi ni mkosaji sana kiasi kwamba Yesu alikufa kwa ajili yangu, bado mimi ninapendwa na ni wa thamani kiasi kwamba Yesu aliona fahari kufa kwa ajili yangu. Hili hutuelekeza kuwa wanyenyekevu na wenye ujasiri wa hali ya juu kwa pamoja. . . . Siwezi kujiona bora Zaidi ya yeyote, na bado sina chochote cha kuthibitisha kwa yeyote." (Keller 2008: 181) Hivyo, tunaweza *"Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri"* (**Waeb 4:16**; angalia pia **Waeb 7:19**). Wakristo wanaweza kuwa na ujasiri huu kwa sababu wanajua wanao uhusiano wa kina na Mungu, kwa sababu Kristo anaishi "ndani" ya Waamini (**Yohana 14:20; 17:23; Warumi 8:10; Wagal 2:20; Waef 3:17; Wakol 1:27; 1 Yohana 3:24; Ufu 3:20**) na Waamini wanakaa"ndani ya Kristo" (e.g., **Warumi 8:1; 12:5; 16: 6, 7, 9-10; 1 Wakor 1:2, 30; 4:10, 15; 15:18, 22; 2 Wakor 1:21; 5:17; 12:2; Wagal 1:22; 3:28; 6:15; Waef 1:3; 2:6, 10; Wafil 1:1; Wakol 1:2; 1 Wathes 2:14; 4:16; 1 Tim 3:13; 2 Tim 3:12; File 23; 1 Pet 5:14**).

6. Kuokolewa na kuunganishwa na Kristo kunawapa Wakristo kusudi na maana ya kuishi. Kwa vigezo vya uhalisia wa maisha, Ukristo, tena, ni wa kipekee ukilinganisha na dini nyingine yeyote, ikiwa ni pamoja na Uislamu. "Dini huongozwa kwa kanuni 'Ninatii—kwa hiyo ninakubaliwa na Mungu.' Lakini kanuni iongozayo Injili ni hii, 'Nimekubaliwa na Mungu kwa sababu ya kile Kristo alichokifanya—kwa hiyo Ninatii.'" (Keller 2008: 179-80)[12]

Kama ilivyoelezwa hapo juu, wakati mtu anapokuwa amempokea Yesu na kuingia kwenye uhusiano wa kiutendaji na Yeye, *kwa uhakika* mtu hupokea vyanzo (moyo mpya, ufahamu mpya, na Roho mpya) ambavyo humwezesha Mwamini kuishi kwenye upya wa kimaadili na maisha ya kumheshimu Mungu. Mfano *binafsi* wa mateso ya Kristo kwa niaba yetu hufungulia nguvu mpya ya kimaadili ambayo hudhihirisha nia zetu, kusudi, na tabia" (Demarest 1997: 196). Hali hii ni sawa na ile ya kupendana na mtu: "Upendo wako hukufanya kuonyesha bidii kwa kukubaliwa na yule umpendaye. . . . [Wakati unapooana na mpendwa wako] Je wewe husema, 'Safi! Nipo ndani! Sasa naweza kufanya vile nitakavyo'? Bila shaka hapana. Sasa hutasubiri hata pale mpendwa wako atakapouliza kutendewa jambo moja kwa moja kwa ajli yako. Utashirikisha chochote utakachoona kinawapendeza wote. Hakuna kusukumwa wala kutakiwa kutenda, bado matendo yako yanakuwa yamebadilishwa ghafla na ufahamu na moyo wa mtu umpendaye." (Keller 2008: 183) Hii ndiyo sababu **Warumi 6:1-2** inasema, *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?"*

III. Dhambi na Wokovu Kulingana na Uislamu

Kwa njia ya Kimsingi, Uislamu hutumia mbinu tofauti na Ukristo kwenye masuala yote mawili ya

[12] Tumeokolewa kwa *kusudi*: *"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu. Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."* (**Waef 2:8-10**) Kazi tuzifanyazo baada ya kumpokea Kristo kwa imani "ni kielelezo cha hali ya Kiroho ya moyo wa mtu. . . . Hukumu siyo uwiano wa matendo mema dhidi ya mabaya. Badala yake, kazi huonekana kama ushahidi usio na kosa kwa unyofu wa moyo; zinaeleza kuamini au kutokuamini, uaminifu au kutokuwa mwaminifu. Hukumu itafunua ikiwa ama unyoofu wa mtu umekuwa na Mungu na mwanakondoo au pamoja na maadui wa Mungu." (Ngundu 2006: 1576; angalia **Math 6:19-21; 24:45-51; 25:31-46; Luka 42-48; Wafil 2:12-13; 1 Tim 6:18-19; Waeb 6:10-12; 1 Yohana 4:7-21**)

Daniel Shayesteh anahitimisha kwa kuonyesha, "Tunaelewa kwamba kile kinachoitwa ulimwengu wa Ukristo umeshindwa kwa kiwango kikubwa kujisalimisha wenyewe kwa Yesu Kristo. Kwa hiyo, ni kwa *kutokuamini* kwenye Yesu Kristo ambako kumeeneza uasherati miongoni mwa wale ambao kwa hakika wanaishi chini ya jina la Ukristo. Maana kwa Injili ya Yesu Kristo, kuna aina moja tu ya Ukristo duniani, wale tu ambao wameokolewa kutoka kwenye utawala wa uasherati. Kwa hiyo, Waislamu wasichukulie uasherati wa wale wanaojiita jamii ya Wakristo kama ishara ya kuwepo mapungufu kwenye Imani ya Kikristo." (Shayesteh 2004: 204, fafanuzi imeongezwa)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

dhambi na wokovu. Kinyume na mbinu ya Kikristo, hata hiyo, mbinu ya Uislamu kwa ndani haitabiriki kuhusu masuala yote mawili.

A. ***Asili ya ubinadamu na mahusiano ya dhambi kulingana na Uislamu***

Korani imeunganisha maelezo ya Adamu na Hawa kula tunda lililokatazwa kwenye bustani ya Edeni (**Q. 2:35-37; 7:10-25; 20:115-23**). Hata hivyo, Korani pia inasema, *"Hakuna mtu yeyote mwenye[dhambi] isipokuwa kinyume naye (pekee),na hakuna mbeba mzigo atakayebeba mzigo wa mwingine"* (**Q. 6:164**, Hilali-Khan); *"Apokeaye ulinzi, hupokea kwa faida yake mwenyewe: ambaye hukengeuka hufanya hivyo kwa kupotea kwake mwenyewe: Hakuna mbeba mzigo atakayebeba mzigo wa mwingine"* (**Q. 17:15**); na *"Hakuna mtu mwenye mzigo (wa dhambi) atakayebeba mzigo (wa dhambi) wa mwingine"* (**Q. 53:38**, Hilali-Khan; angalia pia **Q. 4:111; 7:23; 35:18; 39:7; 53:38-39**). Uislamu huchukulia maandiko haya kwamba hayatumiki kwa watu wa sasa tu bali pia kwa wakati wa Adamu na Hawa. Kwa hiyo nafasi ya "Mamlaka" ya Uislamu hukataa kwamba dhambi ya Adamu na Hawa ndiyo iliyosababisha anguko la mwanadamu na kukataa fundisho la"Dhambi ya Asili." Emerick anasema, "Uislamu hukataa kabisa wazo lolote la dhambi ya asili na kusema kwamba sote tulizaliwa tukiwa safi. Ndiyo, Adamu na Hawa walitenda dhambi, Korani inasema, lakini Mungu aliwahurumia walipoomba Rehema zake. Hakuna dhambi ambayo iliufuatilia uzao wao." (Emerick 2004: 46) Aliongeza, "Hatuna makosa ya ndani kama vizazi au kuwa wenye dhambi kiasili" (Ibid.: 150). Kahtani anaeleza, "Uislamu haukubaliani na wazo lolote la 'anguko la mwanadamu', hakuna wazo la'dhambi ya asili'. Hakuna mtu yeyote ambaye amezaliwa nayo, hakuna ugumu wa lazima ambao mtu hawezi kujiondoa mwenyewe. Mwanadamu yeye hana hatia. Alizaliwa bila hatia. Hakika, alizaliwa kwenye ukamilifu aliopewa kwa maelfu, akiwa na kitengo cha ufahamu, na hisia za ndani za kumjua Mung wa kweli." (Al-Kahtani 1996: 24) Karim anasema kwamba "Kila mtoto anayezaliwa kwenye dini (ya Uislamu) 30:30Q na kama huyo hana dhambi" (Karim 1939: 3:123). Hali hiyo ya kutokuwa na dhambi hubakia hadi "kwenye umri wa kuweza kuwa na uchaguzi binafsi" (Ibid.) au wa balehe (Zawadi n.d.: n.p.). Kwa kweli, Asili ya nafsi ni kwenye kung'ang'ana kutenda yaliyo mema" (Karim 1939:3:122).

Ni nini kulingana na Uislamu, wanachokiona kuwa nai dhambi ya mwanadamu? Makala kwenye IslamAnswering.com inasema, "Chochote kimtokacho mtu baada ya kuzaliwa ni matokeo ya ushawishi wa nje na msukumo wa kweli. . . . Kama atachagua kuwakilishwa na nguvu ya dhambi badala ya nguvu ya wema, atakuwa akiongezea sehemu ya nje kwa asili yake iliyo safi. Kwa nyongeza hii ya sehemu ya nje mwanadamu mwenyewe anawajibika." ("The Concept" 2009: n.p.) Emerick analiweka hili hivi, "Kwa sehemu kubwa tu wasahaulifu kwamba maisha ninini, na Shetani hutumia tamaa na matamanio yetu kuelezea hili" (Emerick 2004: 150).

B. ***Wazo la uadilifu kwenye Uislamu***

Kwenye Uislamu, uadilifu, wema, na uovu havihusiani na viwango vya kidunia vya haki na ubaya ambavyo ni msingi wa asili na tabia ya Mungu mwenyewe na kuandikwa kwenye moyo wa mwanadamu kama Ukristo ufundishavyo. Badala yake, kulingana na Uislamu, Ni maamrisho na makatazo maalum ambayo yamejaa kwenye Korani na Hadithi ambazo huamua ninini kilicho au kisicho cha kimaadili, wema, au uovu. Kufikia "Furaha ya milele Baada ya maisha haya," Suhaym anaeleza kwamba Allah "amezisimika sheria na amri zake kwa ajili yako ili umtii Yeye. Kwa hiyo kama unaamini, tii [sic.] Maamrisho yake na ujiepushe na yale aliyokukataza, utafikia kile ambacho amekuahidia wewe" (As-Suhaym 2006: 221; angalia pia al-Athari 2005: 135). Kwenye maelezo yake kwenye *Mishkat,* Karim anaelezea kifupi: "Yapo makundi mawili ya kazi za mwanadamu, kazi zimhusuzo Mungu na kazi zihusuzo Uumbaji wake. Kazi hizi zote zimeainishwa wazi wazi kwenye Korani na Hadithi. Hitimisho la kazi hizi huitwa sifa, na kuzipuuzia au kuzivunja huitwa dhambi. . . . Kwa kuwa hitimisho la sheria za Korani na Hadithi ni kwa mujibu wa kutunza nafsi kutoka kwenye moto na kwa mchakato wa kuendelea." (Karim 1939: 3:121-22)

Maagizo yafuatayo ya Korani na Hadithi, *Encyclopaedia fupi ya Uislamu* inaeleza, "Sheria za Allah haziingiliki kwa akili, ni *ta'abbudi,* i.e. mwanadamu anapaswa kuzikubali bila kuzijadili, ikiwa ni pamoja na mkanganyiko wake na sheria zake za kutokutabirika, kama busara ambayo ni vigumu kuifikia. Mtu asiiangalie kwa ulazima wa sababu na ufahamu, wala kwa kanuni; ni kwenye msingi wa mapenzi ya Allah ambayo hufungamanishwa na kanuni." (Gibb na Kramers 1953: 525) Hili limethibitishwa na **Q. 5:101-02** ambayo inasema, *"Usiulize maswali kuhusiana na vitu ambavyo, vikiwekwa wazi kwako vitakusababishia matatizo. . . . Baadhi ya watu waliokutangulia waliuliza maswali hayo na kwenye maelezo hayo waliipoteza Imani yao."* Abdullah al-Athari ananukuu mambo mengi ambayo wanazuoni wa Kiislamu wameyaeleza kuwa na madhara kwamba Korani imetaja lakini haikufafanua au kwamba Mohamedi hakufafanua kwa majibu ya maswali ya washiriki wake (mfano, Sifa za Allah, uoni wa Allah, jinsi gani Allah "alivyopanda kwenye kiti chake cha

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

ufalme" [**Q. 20:5; 57:4**], ni jinsi gani alivyoshuka), "zikubali kama zilivyo, bila kuuliza ni jinsi gani . . . Kifupi kwake ni muhimu na kuuliza kuhusiana na hili ni *bid'ah* ["ugunduzi" ambao umekatazwa]." (al-Athari 2005: 86-87) Mawdudi anaeleza kwamba Mohamedi "aliwakataza watu kuwa wachunguzi na wachambuzi makini wa mambo yasiyo ya lazima kuhusiana na kila swali" (Mawdudi n.d.: Q. 5:101n.116). Kwenye hadithi iliyo mahiri sana, Mohamedi alisema, "Mtenda dhambi mkubwa miongoni mwa Waislamu ni mtu yule ambaye huuliza kitu ambacho hakijakatazwa, lakini kikakatazwa kwa ajili ya kuuliza kwake" (al-Bukhari: 7289; angalia pia Muslim: 2358b).

Kwa ujumla, uadilifu wa Kiislamu, mema na mabaya, yamefafanuliwa kwenye shari'ah ambazo zimeandaliwa kuyaongoza maisha yote Ya Waislamu na kutoa mwongozo kwa kila jambo ambalo litaikabili jamii ya Waislamu" (Emerick 2004: 55). Kwa hiyo, "kusudi haliwezi kuwa juu ya shari'ah," lakini "kusudi ni lazima lifanye kazi ndani ya mipaka ya shari'ah" (al-Athari 2005: 175). Msingi wa Shari'ah ni Korani na Sunnah; na kwakuwa Korani kimsingi imejengwa kwenye maneno ya Mohamedi, na Sunnah ni kwa mafafanuzi ya maneno na matendo ya Mohamedi, Kwa Uislamu "Mohamedi ni kiini, na kipimo cha kiwango ambacho matendo yote hupimwa" (Spencer 2009: 94). Kama Ram Swarup alivyoliweka, "Uadilifu hauamui matendo ya Nabii, lakini matendo huamua na kuelezea uadilifu (Swarup 2002: 11).

C. ***Wazo la dhambi kwenye Uislamu***

Dhambi ni suala gumu kwa Uislamu kwa sababu Uislamu" siyo tu mfumo wa mafundisho ya Kitheolojia, lakini pia huwakilisha madai mazito ya mtu wa kawaida asiye na shule. Uislamu ni utaratibu wa maisha ya familia na kwa jamii; unaelezea uvaaji sawa na sheria za ulaji kama ambavyo wameingiza sheria ya inayoongoza ndoa na urithi. Kwa uhakika kanuni hizi huangaliwa kwenye maombi, kufunga, na safari ya kwenda Maka, kanuni ambazo hazijawekwa kwenye mapenzi ya mtu. Kanuni hizi zina hali ya sheria za kidini, kutokuzitii hulifanya tendo husika (maombi , kwa mfano) kutokuwa na thamani mbele za Mungu." (Schirrmacher 2011: 13; angalia pia As-Suhaym 2006: 202-03) Kwa hiyo Emerick aliliweka hivi kwamba "Sheria za Uislamu ambazo zimetokana na miongozo iliyojaa kwenye Korani na mila ya mdomo ya Nabii Mohamedi, ni kitendawili cha kina kuhusiana na nini cha kufanya na nini kisicho cha kufanya, mema na mabaya, na mahusiano miongoni mwa watu" (Emerick 2004: 33).

1. <u>Chini ya sheria ya Uislamu, matendo yote ni *halal* (yanayoruhusiwa) au *haram* (yaliyokatazwa).</u> "Kwa kuishikamana na Roho ya Uislamu ya kupanga matokeo yote, yapo maeneo mawili ambayo kwa hayo matendo yanaweza kuhukumiwa. Haya ni yale ambayo yameruhusiwa, ingawa hayaelezwi; na yasiyopendeza ingawa siyo dhambi." (Emerick 2004: 264) Kwa kufuata misingi wa sheria hizi, wazo la kisheria la dhambi, Uislamu unayo mafungu mengi au madaraja ya dhambi. Upo msingi wa mgawanyiko kati ya "dhambi" "*kabirah*, 'kuu,' na *saghirah*, 'ndogo' (Hughes 1895: 594). Hata hivyo, Sheria za Kiislamu hazitofautishi kati ya hizo mbili. Kwa mfano, Karim anaelezea, "Kuvunja mojawapo ya kazi za msingi ambazo utendaji wake ni Farz (mujibu) na Wajeb (lazima) huitwa dhambi kuu. Kuvunja mojawapo ya kazi ndogo huitwa dhambi ndogo. Kuvunja kazi yoyote ambayo Nabii mtakatifu huzifanya mara kwa mara bila kuvunja nyingine yeyote ni dhambi kuu. Marudio ya mara kwa mara ya dhambi ndogo huifanya dhambi hiyo kuwa kubwa." (Karim 1939: 3:127) Hakuna orodha ya "dhambi kuu." Ghabril anaorodhesha 17 ambazo kwa ujumla zimekubaliwa kuwa dhambi kuu (Ghabril 2003: 15).Maelezo ya Karim kwenye *Mishkat* aliorodhesha 53 (Karim 1939: 3:128-29).

2. <u>Dhambi zilizo kuu kwa Uislamu ni *shirk* (ushirika wenza na Allah) na *kufr* (kutokuamini).</u> Dhambi iliyo kuu kabisa ni *shirk,* ambayo ni Ushirika wenza na Allah. Mmoja wa waandishi wa Uislamu aliliweka hivi, "Mauaji, kubaka, kuwashambulia watoto na mauaji ya halaiki. Haya ni baadhi ya makosa na jinai ya kutisha yanayotokea duniani siku hizi. Wengi wanaweza kufikiri kwamba haya ni makosa mabaya iwezekanavyo ambayo yaweza kutendwa. Lakini lipo moja ambalo laweza kuwa kubwa Zaidi ya makosa hayo yakiwekwa kwa pamoja: Ni jinai ya shirk." ("Shirk" 1997: Utangulizi) "Kwa lugha ya kueleweka, shirk maana yake ni ushirikiano au kushirikisha au mshirika. Hata hivyo, Kiislamu ni kujitoa kwa mwingine kuliko kwa Allah, kile ambacho ni mali ya Allah pekee. Hili linamaanisha kwamba sehemu za uumbaji wa Allah zimepewa nguvu na sifa ambazo ni kwa ajili ya Allah, kama vile, wakati wote kutokumwabudu mwingine Zaidi ya Allah pekee yake." (Ibid.: Ukweli wa Shirk)

Zipo aina kuu mbili za *shirk:* kubwa na ndogo; lakini pia zipo "zilizositirika [au zisizoonekana] shirk" ambazo zaweza kuwa kubwa au ndogo ("The types" 2016: n.p.; At-Tamimi 2002: 212-15). Shirk kubwa ni "kutoa aina yeyote ya Ibada kwa kingine chochote tofauti na Allah" (At-Tamimi 2002: 212; angalia pia "Shirk" 1997: Shirk kwenye kumwabudu Allah [Eebaadah]). Tamimi anaorodhesha makundi madogo ya *Shirk* kubwa (1) ugunduzi (i.e., kuomba mwingine tofauti na Allah [**Q. 29:65**]); (2) malengo, mapenzi, na makusudio (i.e., kuyatamani maisha ya ulimwengu [**Q. 11:15-16**]); (3) kutii

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

(i.e.,utayari wa kutii taratibu za wengine kwa kutokumtii Allah [**Q. 9:31**]); na (4) kupenda (i.e., kuonyesha mapenzi kwa wengine ambayo ni kwa ajili ya Allah pekee [**Q. 2:165**]) (At-Tamimi 2002: 212-14). Allah hatasamehe kabisa hata ile iliyoorodheshwa kama ndogo ya *Shirk* kubwa (angalia **Q. 4:48, 116; 17:39; 39:65; 98:6**).[13] Mohamedi alisema kwamba shirk ndogo ni "kujionyesha (kwa matendo mema)" (al-Asqalani n.d.: book 16, no. 1527; angalia pia At-Tamimi 2002: 2015; "The types" 2016: Mfano mmoja wa ash-Shirk ul-Asghar).

Shirk yaweza kuwa ni hila sana. "Shirk iliyositirika ni moja ya aina ya hatari sana ya shirk kama watu hawawezi kuona kama wameitenda hiyo dhambi" ("The types" 2016: Ash-Shirk ul-Khafie [Shirk iliyositirika]). Mohamedi alisema kwamba *Shirk* iliyositirika au isiyoonekana "imefichika hata Zaidi ya mstari wa siafu weusi kwenye jiwe jeusi wakati wa usiku wa giza" (At-Tamimi 2002: 215; angalia pia Abdul-Wahhab 2002: 141). Mohamedi pia alisema, "Hakuna kitu kinachosimama baina ya mtu na Shirk (miungu) isipokuwa kuacha kuomba, hivyo kama mtu ataacha kuomba atakuwa amefanya dhambi ya Shirk" (Ibn Majad: vol. 1, book 5, no. 1080). "Ibn 'Umar alimsikia mtu akisema: 'Hapana ila kwa Ka'bah' hivyo Ibn 'Umar alisema: 'Hakuna kingine cha kuapia zaidi ya Allah, kwa kuwa alimsikia mjumbe wa Allah akisema: 'Yeyote atakayeapa kwa kingine chochote isipokuwa kwa Allah, atakuwa ametenda kwa kutokuamini au shirk'" (at-Tirmidhi: 1535). Ibn Abbas alisema kwamba *shirk* "pia ni kusema: 'Kwa kutokuwa na mbwa huyu mdogo hapa nyumbani, mwizi angeingia.' au, kama kauli ya mtu kwa mshiriki wake: 'Kwa mapenzi ya Allah na kwa mapenzi yako…' au 'Hapakuwa na Allah na Fulani na fulani', nk. Usimtaje Allah na mtu au kitu kingine chochote kwa sababu hiyo ni *Shirk*." (Abdul-Wahhab 2002: 141). Abdul-Wahhab anaendelea hivi "ni dhambi kubwa [*Shirk]* kutenda matendo ya (haki) kwa kusudi la kidunia" (Ibid.: 129).

Kuhusiana na *shirk* ni kutokuamini(*kufr*). Athari anasema zipo aina mbili za *kufr: Kufr* kubwa ni kumweka mtu juu ya Uislamu na vitu vingine kutokuwa na nafasi. *Kufr* kubwa inaitwa *kufr* ya imani: "Hiki ni kile kinachoenda kinyume na Imani na kudhoofisha Uislamu, kitakachomfanya mtu afungiwe Jehanamu milele. Kinaweza kuchukua umbo la Imani, maneno au matendo. Vimegawanywa kwenye mafungu matano." (al-Athari 2005: 144) Mafungu hayo matano ni: (1) *Kufr* kwa kutokuamini i.e., kuamini kwamba Wajumbe ni waongo au kudai kwamba Allah ameruhusu au kukataza kitu ambacho mtu anakijua siyo sababu; (2) *Kufr* ya kiburi kukataa kufuuata ukweli wa Uislamu ingawaje mtu amethibitisha kwamba ni kweli; (3) *Kufr* ya kugeukia mbali, i.e., kwa kuamini au kutokumwamini mjumbe au kudharau ukweli; (4) *Kufr* ya unafiki, i.e., kujionyesha kwa nje kufuata kile ambacho mjumbe ameleta , wakati huo huo kwa ndani unadharau na kukikataa; (5) *Kufr* ya mashaka, i.e., kuwa na mashaka na baadhi ya mambo ya Nabii na kushakia kumfuata. (Ibid.: 144-46; angalia pia At-Tamimi 2002: 216-17)

3. Matokeo mengine ya mtazamo wa Uislamu juu ya Uadilifu na dhambi. Kwa sababu mtazamo wa Uislamu juu ya uadilifu umejikita kwenye "kina cha kufanya na kutokufanya" kwenye Korani na kwenye Hadithi, matendo ya dhambi ambayo yatampeleka mtu Jehanamu ni kama vile orodha yake haina mwisho. Kwa mfano, Emerick anaeleza, "Wakati matendo yetu mema na mabaya yanapokuwa yamekaribia kutathminiwa, Mohamedi alisema kwamba maombi yetu yatatazamwa kwanza. Kama yakionekana yana mapungufu makubwa, basi Mungu hatayaangalia yale mengine yote yaliyosalia. Fikiria unaenda mahakamani ukiwa na ushahidi wote kwamba inakuacha huru na badala yake kutangazwa kwamba unahukumiwa kwa sababu ya makosa makini ambayo yametendeka kwa upande wako!" (Emerick 2004: 136) Zifuatazo ni baadhi ya sheria za Mohamedi ambazo zina adhabu ya milele:

- "Yeyote atakayefunga ndevu zake, au kuzisokota, au kutegemea amrulet, au kujiosha mwenyewe (baada ya kujiachia mwenyewe) kwa matope ya mnyama au mifupa, Mohamedi hana kitu cha kumfanyia." (an-Nasa'i: 5067)
- "Watu watakaopokea adhabu kali Zaidi kutoka kwa Allah ni wale wanaotengeneza picha." (al-Bukhari: 5950; angalia pia 2086, 2238, 5181, 5347, 5957, 5961, 5962)
- "Vitu viwili ni ishara ya kutokuamini kwa upande wa wale wanaovitamani: kudharau uzao wa mtu na kuwalilia wafu." (al-Nawawi, *Riyad*: book 18, no. 157; angalia pia no. 68)
- "Usivae Hariri na usivinywee vyombo vya dhahabu na fedha, na usile kwenye sahani ambazo zimetengenezwa kwavyo (i.e., dhahabu na fedha), kwa kuwa hivi ni vyao (wale wasioamini) kwenye ulimwengu huu." (Muslim: 2067g; angalia pia 2065b, c, 2067a; al-Bukhari: 5832, 5833, 5837; an-Nans'i: 5136, 5301; Abi Dawud: 3723; Ibn Majah: vol. 4, book 30, no. 3414)

[13] Abdul-Wahhab anaeleza, "Washiriki wa Mohamedi walieleza kwamba aya zilizofunuliwa kuhusu *Shirk* kubwa zilijumuisha Shirk ndogo pia" (Abdul-Wahhab 2002: 142). Kama hili liko hivyo, basi Allah pia hawezi kusamehe *shirk* ndogo.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

- "Uvaaji wa waamini kuvaa mavazi mafupi na kuwa nusu ya mguuni na hahukumiwi kuwa na dhambi kama litakuwa nusu kati ya mguu na goti, lakini inayokuwa fupi juu ya magoti ni kwa ajili ya Jehanamu. Kwa siku ya kiama, Allah hatamwangalia huyo avaaye nguo fupi kwa kiburi." (Abi Dawud: 4093; angalia Ibn Majah: vol. 4, book 32, no. 3574; al-Nawawi, *Riyad*: vol. 4, no. 15)

Hatimaye, matendo yasiyokuwa ya kukusudia hakika yaweza kuwa dhambi, hata *shirk*. Kwa mfano, **Q. 12:106** inasema, *"Wengi wao wanamwamini Allah lakini bado wanafanya Shirk (wanaabudu mungu zaidi ya mmoja)."* Abdul-Wahhab anaeleza, "Kutumia vibaya *Ad-Dahr* (muda) ni kumkosea Allah. . . . Kitu chaweza kuwa ni matumizi mabaya *hata kama siyo jambo la kukusudia moyoni (kwa mtumiaji mbaya)*." (Abdul-Wahhab 2002: 147, fafanuzi imeongezwa) Kwenye jambo jingine, "Jundub anaeleza kwamba Mjumbe wa Allah alieleza kwamba mtu alisema: Allah hatasamehe hili na lile (mtu). Kwa hilo Allah aliyeinuliwa mwenye Utukufu alisema: Huyo ni nani ambaye ananiamrisha mimi kwamba siwezi kumsamehe kwa fulani na fulani; Nimemsamehe Fulani na fulani na kufutiliaa mbali matendo yae (ambaye aliapa kwamba Sitamsamehe)." (Muslim: 2621) Abdul-Wahhab anakumbusha kwamba aliyeyasema hayo alikuwa mwabudu mwaminifu, lakini "neno lake moja limeyaangamiza maisha yake hapa duniani na kwenye ulimwengu ule Ujao. . . . Kwenye *Hadithi* imeelezwa kwamba mara nyingi mtu hunena maneno ambayo hakuyakusudia lakini madhara yake ni kaburi (i.e., adhabu kali)." (Abdul-Wahhab 2002: 183) Kama ilivyoelezwa hapo juu, "Shirk iliyositirika ni moja ya muundo hatari zaidi wa Shirk ambao watu hawawezi kuona kama wameitenda" (Al-Aqeedah 2014: Ash-Shirk ul-Khafie [Shirk iliyositirika]).

D. *Tofauti na mafundisho yake rasmi, Uislamu kwa kweli unakubali kuwa mwanadamu anayo dhambi ya asili*

Mafundisho ya msingi ya Uislamu ni kwamba mwanadamu aliumbwa asiye na hatia na tabia yetu ya asili ni kung'ang'ana kutenda mema. Kwa hiyo mtu mmoja anaweza kutarajia baadhi ya watu—hasa Mohamedi mwenyewe—kutenda kulingana na walivyopaswa "kutokuwa na hatia" na "tabia ya asili" wasingetenda dhambi. Hilo siyo la muhimu. Kwa kweli Uislamu unatambua kwamba kila mwanadamu anayeishi na yeyote aliyewahi kuishi, ikiwa ni pamoja na Mohamedi, ni watenda dhambi.[14] Hivyo, **Q. 35:45** inaeleza, *"Kwama Allah angewahukumu watu kulingana na kile wanachostahili. Nyuma ya dunia asingelisaza hata kiumbe kimoja kikiwa hai"* (angalia pia **Q. 16:61; 103:2**). Mohamedi alisema, "Kila mwana wa Adamu ni mtenda dhambi, na mtenda dhambi aliye bora ni yule aliyetubu" (at-Tirmidhi: vol. 4, book 11, no. 2499). Ali anakiri kwamba "hakutakuwa na wokovu kwa hata mmoja wetu kama tutatembea tu kwenye jangwa letu" (Ali 2006: Q. 35:45n.3940).

Ujumla wa dhambi siyo tu matokeo ya "ushawishi wa nje na misukumo ya kweli" ("The Concept" 2009: n.p.). Badala yake, kinyume na ukiri wa fundisho lao wenyewe kwamba mwanadamu alizaliwa safi na kiasili anasukumwa kwenye mema, Uislamu, kama Ukristo, kweli huchukulia ujumla wa dhambi za mwanadamu kuwa ni asili ya uovu wa ndani wa wanadamu wote. Mafundisho ya Uislamu yanatupa sababu tatu tofauti kwa dhambi ya kuzaliwa ya mwanadamu:

1. <u>Dhambi ya mwanadamu imehusishwa na jinsi ambavyo Allah alimwumba mtu tangu mwanzo.</u>
Mistari mingi ya Korani inaashiria kwamba Allah alimwumba mwanadamu na uovu au asili ya dhambi: *"Mwanadamu aliumbwa dhaifu"* (**Q. 4:28**); *"Hakika, mwanadamu ameachiliwa kuwa mtenda makosa na asiye na shukurani"* (**Q. 14:34;** angalia pia **Q. 33:72**);*"Ni sisi tuliomwumba mwanadamu, na tunajua ni jinsi gani nafsi yake ilivyo na mawazo potofu"* (**Q. 50:16**); *"Hakika mwanadamu ameumbiwa kukosa uvumilivu"* (**Q. 70:19**); *"Na [kwa] nafsi na Yeye ambaye aliipanga na kuivuvia [ikiwa na utambuzi wa] uovu wake na haki yake"* (**Q. 91:7-8**, Sahih).[15] Kwa kuielezea aya hii hasa, Mohamedi anathibitisha kwamba Allah ndiye aliyeivuvia (i.e., "kupulizia ndani") dhambi ndani ya nafsi ya mwanadamu: "Tafakari nafsi na Yeye aliyeiumba ikiwa kamilifu, baadaye *kuipulizia ndani yake dhambi* na maana yake ya Kiungu (huruma)" (Muslim: 2650, fafanuzi imeongezwa). Mohamedi pia alisema, "Allah aliweka sehemu ya uzinzi ambao mwanadamu angeitamani. Hakutakuwa na namna ya kuiepuka." (Muslim: 2658a; angalia pia al-Bukhari: 6243; al-Nawawi, *Riyad*: book 18, no. 112) In **Q. 2:30**, wakati Allah akiandaa kumwumba mwanadamu makamu wake duniani malaika walijibu, *"Utamweka hapa mtu ambaye atapaharibu na kumwaga damu?"* Mwitikio huo uliashiria kwamba Malaika walikuwa wanajali, *hata kabla dhambi yenyewe haijatendwa*, dhambi hiyo isingeepukika kwa

[14] Tarajio pekee kwenye hili ni Yesu Kristo (angalia hapo juu, kipengele cha **2.VIII.E.** ***Yesu, siyo Mohamedi, asiye na waa, mtakatifu, na asiye na dhambi wala kosa toka alipozaliwa***).

[15] Kumbuka kwamba sehemu ya aya hii kwenye mabano tafsiri imeongezwa na mtafsiri na haipo kwenye maandishi ya asili. Wakati yanapoondolewa, aya huashiria kwamba ni Allah ambaye aliivuvia nafsi ya mwanadamu uovu wake.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

sababu ya dhambi ya ubinadamu, iliyoumbwa kwa asili. Ibn Kathir anakiri, "Malaika waliujua ukweli huu, kulingana na uelewa wao juu ya asili ya mwanadamu" (Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 2:30, maoni).

Hadithi inaendelea kuonyesha kwamba hata kutoka mwanzo wanadamu hawakuwa na uwezo wa kujiongoza wenyewe: "Wakati Allah alipomwumba Adamu ndani ya Paradiso, Alimwacha kama yeye alivyotaka aishi. Basi Ibilisi alimzungukia huko kuona kile halisi kilikuwa nini na wakati alipomkuta ana huzuni ndani yake, alitambua kwamba alikuwa *ameumbwa na asili ambayo asingeweza kuitawala yeye mwenyewe*." (Muslim: 2611a, fafanuzi imeongezwa) Hivyo, **Q. 12:53** inathibitisha kwamba hali ya asili ya mwanadamu yote haikuumbwa kukabiliana na mema, lakini imeumbiwa kukabiliana na maovu: *"Wala siwezi kujiombea mwenyewe (kwa laumu):kwa (mwanadamu) nafsi yake hakika imekabiliwa na uovu, mpaka hapo Bwana wangu atakapoziruhusu Rehema zake."* Hilali-Khan anatafsiri hili kama *"Hakika, nafsi ya (mwanadamu) imekabiliwa na uovu."* **Q. 14:34** inaeleza, *"Hakika, mwanadamu ameachiliwa katika mambo yasiyo ya haki na kutokuwa na shukurani"* (angalia pia **Q. 33:72**). **Q. 18:60-82** inaeleza kisa cha ajabu cha Musa kukutana na Nabii aliyejulikana kama Al-Khidr ambaye Allah alimpa ujuzi na Rehema (**Q. 18:65**). **Q. 18:74** (Hilali-Khan) anasema, *"Hao wote wawili wakaendelea,hata walipokutana na kijana, yeye (Khidr) akamwua. Musa (Moses) akasema: 'Utamwua mtu asiye na hatia ambaye hajamwua mtu yeyote? Hakika, umetenda kitu ambacho ni "Nukra" (Munkar kubwa - iliyokatazwa, uovu, mambo ya kutisha)!'"* Kwenye Hadithi, Mohamedi alijaribu kuhalalisha mauaji hayo kwa kusema, "Kijana ambaye Khadir alimwua alikuwa siyo muumini *kwa asili yake* na kama angeachwa kuishi angewaingiza wazazi wake kwenye hali ya unajisi na kutokuamini" (Muslim: 2662a, fafanuzi imeongezwa).[16]

Khan ananukuu shairi la Khalifa wa kwanza, Mshiriki wa karibu wa Mohamedi Abu Bakr, "Ee Mungu, nawezaje kuokolewa, maana hakuna jema ndani yangu? Nimelemewa na maovu, lakini nayahitaji yaliyo mema." (Khan 1992: 17) Suhaym anaeleza kwamba toba humfanya mtu "kuijua halisi nafsi yake, ambayo inakabiliana na uovu" na "inamwezesha kujua kwamba amejawa na makosa na kutokukamilika" (As-Suhaym 2006: 217, 218).

2. Uovu wa mwanadamu umechangiwa na dhambi ya Adamu na Hawa ambayo ilileta madhara kwa kizazi chake. Uislamu unaonekana kuwa na toleo lao wenyewe la "anguko" la mwanadamu. **Q. 2:30** inasema, *"Tazama, Bwana wangu aliwaambia Malaika: 'Nitamwumba (vicegerent)vichwaji humu duniani.'"* Hivyo vichwaji vilikuwa wanadamu. **Q. 33:72** anaongeza, *"Kwa kweli tuliweka tumaini letu kwenye Mbingu na Dunia na Milima; lakini walikataa kulikubali, waliliogopa: Lakini mwanadamu alilikubali;- Hakika alikuwa mpumbavu na asiye na haki."* Yusuf Ali alilitolea hili maoni na kusema, "Mingu na Nchi na Milima, *i.e.,* viumbe vingine vya Allah, tofauti na mwanadamu, vilikataa kukubali kupokea tumaini hilo au wajibu, na tunaweza kufikiria kwamba vina furaha bila kuwa na uchaguzi wa mema na mabaya wapewavyo na mapenzi yao. Kwa kusema kwamba walikataa, tunayahusisha mapenzi, lakini tunayawekea ukomo kwa maneno kwamba hawakukubali kupokea uwezo wa kuchagua baina ya mema na mabaya. Walichagua kuyatoa mapenzi yao yote kwa mapenzi ya Allah, ambayo ni Hekima yote na Ukamilifu, na ambavyo vingeweza kuwapa furaha iliyo kuu zaidi ya kile kitengo cha uchaguzi ndani yao, kwa ujuzi wao usio mkamilifu. Wanadamu walikuwa wenye ujasiri mwingi na wajinga kuliachia hili, na matokeo yake ni kwamba mwanadamu kama kizazi alianza kutaabika." (Ali 2002: Q. 33:72n.3779) Kwa hili, mtu anaweza kusema kwamba asili ya Uanadamu ilikuwa asiye na uharibifu lakini kupitia dhambi alipatwa na uharibifu, i.e., "alianguka."

Maeneo mengine ya Korani na hadithi yanaliunganisha moja kwa moja anguko la mwanadamu na dhambi ya Adamu na Hawa kwenye Bustani, kama vile ambavyo Biblia inavyosimulia. **Q. 2:36-37**

[16] Hili halihalalishi kabisa. Kijana hakufanya chochote kiovu. Kumwua mtu ambaye hakufanya jinai yeyote ile si haki kwa kiwango chochote—isipokuwa, linawezekana kwa Uislamu peke yao. Hata *Tafsir al-Jalalayn* anaeleza kwamba "walikutana na kijana, *ambaye alikuwa bado hajafikia umri wa kubalehe*, akicheza na [wengine] vijana, ambaye miongoni mwao uso wake ulionekana usio na hatia—na yeye, al-Khidr, alimchinja, kwa kulikata koo lake na kisu wakati akiwa amelala chini, au kwa kukifyeka kichwa chake kwa mkono wake, au kwa kukipigiza kichwa chake ukutani" (Jalal 2013: Q. 18:74, maoni, fafanuzi imeongezwa). Kwakuwa kijana alikuwa bado hajabalehe, kulingana na mafundisho halali ya Uislamu alikuwa kwenye asili yake ya utakatifu, au fitrah na kwa hivyo hakuwa na dhambi. Kweli zilizoko kwenye simulizi hii ni, kulingana na Mohamedi, ni kwamba kijana hakuwa muumini (Muislamu), ambao ni ushahidi tosha wa msingi wa kumwua mtu. Sababu za Al-Khidr kumwua kijana zilikuwa za kutisha na mbaya zaidi: *"Na kama kwa kijana, wazazi wake walikuwa waumini (wa Uislamu), na tulimhofia kwamba angewakandamiza kwa uasi na kufuru"* (**Q. 18:80**). Kwa mujibu wa Al-Khidr, kijana asiye na hatia alikuwa mtoto wa wazazi wazuri wa Kiislamu, na yeye "alihofia tu" kwamba kijana angekuwa muasi na (mwenye kufuru) asiye amini! Kwa vyo vyote mtu angeliangalia hili, simulizi hii inaufunua upande wa uovu na vurugu za Uislamu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

inasema, *"Na Tulisema: Ewe Adamu, kaa wewe na mkeo katika bustani, na kuleni humo kwa maridhawa po pote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu msije mkawa miongoni mwa wadhalimu. Lakini Shetani akawatelezesha wote wawili humo na akawatoa katika ile (hali) walimokuwemo. Ndipo Tukawaambia: Nendeni, m-maadui ninyi kwa ninyi, na kao lenu ni katika ardhi na (mtapata) matumizi kwa muda'"* (angalia pia **Q. 7:22-25; 20:117-23**) Gilchrist anaonyesha kwamba "neno kuu hapa ni *ahbituu* ambalo linatokana na kiini cha neno *habt* likimaanisha kwenda chini au kushuka kutoka mahali pa juu kwenda mahali pa chini. 'Kuanguka chini!' ilikuwa ni amri, kama kusema wazi 'Ondokeni hapa!'" (Gilchrist 2002: 101; angalia pia "Kamusi ya Korani" 2009-2017: Q. 2:26, *ih'biṭū*) Ingawaje Allah aliwasamehe Adamu na Hawa (**Q. 2:37; 20:122**), Hakuwaruhusu kabisa kurudi Bustanini.

Zaidi, "anguko" la Adamu na Hawa halikuwaathiri wenyewe tu lakini pia kizazi chao. Kwa maneno mengine, kwa nyongeza ya kukubali fundisho la "anguko" la mwanadamu, Uislamu *pia* unakubali fundisho la "dhambi ya asili." Tunalijua hili kwa sababu adhabu ya Allah kwa Adamu na Hawa iliwahukumu vizazi vyote vya Adamu na Hawa kwa kuwafukuza wote kwenye bustani—bila kujali ukweli kwamba inadaiwa walizaliwa kwenye hali ya utakatifu, *fitrah,* na wasio na dhambi. Kumbuka kwamba Amri ya Allah kwenye **Q. 2:36** imeongeza watu "wote" siyo "wawili wao." Hivyo, kwenye mitazamo mingine wanadamu wote "katika Adamu," kama vile ambavyo Ukristo unafundisha. Mohamedi anayathibitisha haya kwenye hadithi, "Adamu na Musa walikutana, na Musa akamwambia Adamu 'Ewe Adamu! Wewe ndiye baba yetu uliyetukosesha na kututoa nje ya Paradiso'" (al-Bukhari: 6614; see also 3409, 7515, vol. 6, book 60, no. 260, 262; Muslim: 2643a, 2652a, b, c; Abi Dawud: 4701, 4702). Kama matokeo, "Mungu akatangaza kwamba wanadamu watakuwa na kutokukubaliana na chuki wenyewe kwa wenyewe kutoka sasa kwa sababu ya masumbufu ya tokea kuzaliwa ili kuumudu ulimwengu huu" (Emerick 2004: 94). *Simulizi* ya Tabari inaeleza, "Wakati Mungu alipowaweka Adamu na mke wake kwenye Paradiso yake, Aliwaruhusu kula kila tunda walilolitaka, isipokuwa tunda la mti mmoja. Hili lilikuwa ni kuwasumbua na hukumu ya Mungu ije juu yao *na vizazi vya* vitakavyofuata [imenukuliwa **Q. 2:35**]." (al-Tabari 1989: 275, fafanuzi imeongezwa)

Kwa nyongeza, adhabu ya Allah ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuishi hapa duniani "*kwa muda tu"* (**Q. 2:36**). Kwenye maoni yake juu ya aya hii, Ibn Kathir anaonyesha kwamba *"kwa muda"* maana yake "maisha yenye ukomo" (Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 2:36, maoni) Hivyo, Kifo cha mwanadamu ni matokeo ya dhambi ya Adamu na Hawa. Mwandishi mmoja Muislamu aliutumia mfanano huu kuhusiana na dhambi ya Adamu na Hawa na adhabu ya Allah: "Kama kwa matokeo ya dhambi ya Adamu, ambayo ilimsababishia kuondolewa kutoka bustanini, hili liliwagusa hata wale watakaofuata baada yake na hili ni la Asili tu. Kama mtu akilewa pombe na kupata ajali ya gari, na baadhi ya abiria wake kufa, dhambi ya Dereva itawadhuru abiria katika kufa kwao." (Abdulsalam 2006: The Divine Will)[17] Kwa kuyaona matokeo na hukumu ya Adamu na Hawa kwa vizazi vyao, dhambi ya Adamu na Hawa haikuwaangamiza wao wenyewe tu lakini kwa kila aliyefuata baada yao—halisi kama ambavyo fundisho la dhambi ya asili na anguko la mwanadamu linavyoeleza.

Kwenye Hadithi, Mohamedi kwa wazi alilizungumzia fundisho la dhambi ya asili. Kwenye muunganiko na siku ya hukumu alisema, "Allah, M-barikiwa na Aliyeinuliwa, atawakusanya watu. Waamini watasimama hadi Paradiso itakapoletwa karibu nao. Watakuja kwa Adamu na kumwambia: 'Ewe Baba yetu, tufungulie Paradiso.' Atasema: 'Kilichowatoa nje ya Paradiso ilikuwa ni dhambi ya Baba yenu Adamu.'" (Muslim: 195; angalia pia an-Nawawi, *Riyad:* book 1, no. 201) Penginepo, Mohamedi hali kadhalika alilitumia wazo kwamba dhambi ilipelekwa kwa wengine: "Lakini kwa Israeli, nyama haitaoza na lakini kwa Hawa, wanawake hawatawasaliti waume zao kabisa" (al-Bukhari: 3330; angalia pia 3399); na "Hakuna mtu atakayeuawa bila kosa, lakini kwa kushiriki (hili shitaka lake pia) liliangukia juu ya mzaliwa wa kwanza wa Adamu, kwa kuwa alikuwa wa kwanza kutanguliza mauaji" (Muslim: 1677a; angalia pia al-Bukhari: 3335, 6867, 7321; at-Tirmidhi: 2673; an-Nasa'i: 3985; Ibn Majah: vol. 3, book 21, no. 2616).[18]

Hivyo, ingawa Uislamu awali ulikataa fundisho la dhambi ya asili na anguko la mwanadamu,

[17] Abdulsalam anaendelea kusema, "Hili halimaanishi kwamba abiria wanapaswa kuhesabiwa dhambi ya dereva" (Abdulsalam 2006: The Divine Will). Ingawa hili ni kweli kwa upande mmoja, umuhimu wa fundisho la dhambi ya asili unatupeleka kwenye *matokeo* ya dhambi ya Adamu na Hawa kwa vizazi vyake, kama vile abiria wanavyoweza kuhusika na matokeo ya ajali iliyosababishwa na dereva mlevi.

[18] Hakika hii ni dhambi ya asili: "Kama Nikiua leo, Ninafanya hivyo kwa uchaguzi wangu mwenyewe pia [kama alivyofanya Kaini]. Kwa maneno mengine, Siui kwa sababu Kaini aliua, Lakini Natenda dhambi (kwa kuua), kwa sababu dhambi ilianza na Kaini. Ukubwa wa dhambi ya Kaini umekuwa urithi wetu, au kama Mohamedi alivyoliweka, *Tunashiriki* dhambi ya Kaini." (Prince 2011: 53, fafanuzi imeongezwa kutoka kwenye asili)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kiukweli hufundisha mafundisho haya yote mawili.

3. Uovu wa mwanadamu ulitoka moja kwa moja kwa Allah. Tumeona hapo juu kwamba Korani na hadithi zinafundisha kwamba Allah aliwaumba wanadamu na uovu, asili ya dhambi. Kuwaumba watu kwa hali hiyo Allah hakufanya hayo yote ili kuhakikisha kwamba kila mwanadamu anatenda dhambi. **Q. 4:88** (Hilali-Khan) inasema kwamba Allah kwa hakika ndiye aliyewasababishia watu kukosea bila tumaini wala dawa: *"Wale wanaopenda maisha ya dunia kuliko Akhera, na kuzuilia (watu) njia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotosha. Hao wamo katika upotevu wa mbali."* **Q. 14:4** (Hilali-Khan) anaongeza, *"Allah lakini anayetaka (upotevu) Anampoteza, na anayetaka (mwongozo) Anamwongoza"* (angalia piao **Q. 16:93**). Kwenye Hadithi Mohamedi alisema, "Hakuna nafsi ambayo haipo kati ya vidole viwili vya Mwenye Huruma kuu. Kama akipenda, Atailinda na kama Akipenda , Huipotosha." (Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 199; angalia pia 3834; Muslim: 2655; at-Tirmidhi: 3522) Kwenye hadithi kama hiyo, Mshiriki wa Mohamedi, Anas bin Maalik alisema, "'Ewe Nabii wa Allah! Tunakuamini wewe na kile ulichotuletea, lakini unatuogopa sisi?' Alisema: 'Ndiyo. Hakika nafsi zipo kati vidole viwili, vidole vya Allah, Huzibadili kama apendavyo.'" (at-Tirmidhi: vol. 4, book 6, no. 2140)

Allah pia amethibitisha kwamba wale watakaopotoka na wataangukia kwenye dhambi zaidi. Kwanza, Korani inaonyesha kwamba Allah mwenyewe alimsababisha Shetani atende dhambi: *"Tena Shetani Akasema, 'Kwa sababu Umenihukumu mpotevu kwa yakini nitawakalia katika njia yako iliyonyooka'"* (**Q. 7:16**, Sarwar); Arberry alilitafsiri hivi *"Sasa, kwa kunipotosha Mimi . . ."* Pili, Allah akawaambatanisha mapepo na watu wawe washiriki wao wa karibu:*" Na anayegeuka asimkumbuke Rahmani Tunamwekea Shetani naye anakuwa rafiki yake. Na kwa yakini hao wanawazuilia njia nao hudhani ya kwamba wanaongoka!"* (**Q. 43:36-37**) Kwa nyongeza, Allah alithibitisha kwamba mapepo watakuwa wakitenda kazi kwa sababu, kama Mohamedi alivyosema, "Mwovu hampotoshi yeyote kwa majaribu yake isipokuwa yule ambaye Allah amemkusudia kwenda Jehanamu" (Abi Dawud: 4614).

Hata Korani inasema kwamba Allah angemfanya mwanadamu mara moja na kwa amani, lakini kusudi lake muhimu kwenye uumbaji lilikuwa ni kuijaza Jehanamu kwa wajini na wanadamu: *"Na Tungalitaka, Tungempa kila mtu mwongozo wake, lakini imehakiki kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahanamu kwa wote hawa majinni na watu'"* (**Q. 32:13**; angalia pia **Q. 11:118-19**; **Q. 6:149; 13:31**). Hadithi nyingi zinathibitisha kwamba Allah aliwaumba watu hasa ili kuwapeleka Jehanamu: "Allah aliwaumba watu kwa ajili ya Paradiso, Aliwaumbia hiyo wakati wakingali kwenye viuno vya Baba zao bado, Na aliwaumba watu kwa ajili ya Jehanamu, Aliwaumbia hiyo wakati wakingali kwenye viuno vya Baba yao bado" (Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 82; angalia pia Muslim: 2662b, c; Abi Dawud: 4713; an-Nasa'i: 1947) Hadithi pia zinathibitisha kwamba Kusudi na furaha ya Allah kumwumba mwanadamu ilikuwa ni ili watende dhambi. Mohamedi alisema, "Kama hamtatenda dhambi, Allah atauondoa uwepo wenu na ataweka watu wengine ambao wametenda dhambi, na baadaye kuomba msamaha kutoka kwa Allah, na atawasamehe wao" (Muslim: 2748b; angalia pia 2749).

E. *Wokovu kulingana na Uislamu*

Kama vile Uislamu kwa ndani hawana nafasi iliyo sawa kulingana na asili ya mwanadamu na sababu ya dhambi, vivyo hivyo hawana nafasi iliyo sawa kuhusiana na jinsi gani watu wanaweza kuokolewa au kukombolewa kutoka kwenye dhambi zao na kwenda Paradiso badala ya Jehanamu. Kwa kiwango kidogo kupo kutokukubaliana kwenye mafundisho kuhusiana na jinsi gani watu wanaweza kuokolewa kutoka Jehanamu kwenda Paradiso: (1) Ulinganifu wa matendo ya mtu kati ya mema na mabaya; (2) Uchaguzi huru wa Allah wa kumsamehe mtu kwa sababu zake mwenyewe, bila kujali kazi za mtu; na (3) Tangazo la awali la Allah la kwamba wengine walielekezwa Paradiso tokea awali na wengine kuelekezwa Jehanamu tokea awali.

1. Wokovu ni ulinganifu wa kazi za mtu. **Q. 53:39** (Hilali-Khan) anaelezea msingi wa "Wokovu binafsi" falsafa ya Uislamu: *"Na mtu hatapata isipokuwa matunda ya juhudi yake; (mema au mabaya)."* **Q. 2:281** alionya kwamba mtu*"ogopeni Siku ambayo mtarudishwa kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila mtu atapewa sawasawa aliyoyachuma, nao hawatadhulumiwa."* Korani inayo mistari makumi ambayo inasema kwamba kibali cha Allah siku ya hukumu ya mwisho itakuwa juu wale ambao *"amini na utende kwa haki"* (e.g., **Q. 10:4; 11:23; 14:23; 17:9; 18:30, 46; 20:75, 82, 112; 22:14, 23, 50, 56; 28:67, 80; 32:19-20; 99:6-8**). Suhaym anaeleza, "Wanaomwamini Allah watakuwa na ujuzi wa hakika kwamba hakuna njia ya mafanikio na wokovu isipokuwa kupitia matendo mema ambayo humpendeza Allah" (As-Suhaym 2006: 179). Korani pia inaifananisha hukumu na mizani ambapo matendo mema na mabaya yatapimwa: *"Na Siku hiyo kipimo kitakuwa sawa. Basi atakayekuwa na*

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

uzani mzito, hao ndio watakaofaulu. Na watakaokuwa na uzani hafifu, basi hao ndio waliohasiri nafsi zao kwa sababu walikuwa wakifanyia jeuri Aya Zetu." (**Q. 7:8-9**; angalia pia **Q. 21:47; 101:6-9; 23:101-03**)

Hali siyo rahisi kama ambavyo ulinganifu wa mizani unavyoashiria. Korani inasema kwamba siku ya hukumu *watu wote* na mapepo yote kwanza *watatupwa Jehanamu*; ni wachache tu ambao baadaye wataokolewa kutoka Jehanamu: *"Je, mwanadamu hakumbuki ya kwamba Tulimwumba kabla hali hakuwa cho chote? Basi kwa kiapo cha Mola wako kwa yakini, Tutawakusanya wao pamoja na mashetani; kisha bila shaka Tutawahudhurisha pembezoni mwa Jahanamu, wakiangukia magoti. Kisha kwa yakini Tutawatoa katika kila taifa wale miongoni mwao waliomwasi zaidi Mungu wa huruma. Tena hakika Sisi Tunawafahamu sana wanaostahili zaidi kuunguzwa humo. Wala hakuna ye yote katika ninyi ila ni mwenye kuifikia. Ndiyo wajibu juu ya Mola wako uliokwisha hukumiwa. Kisha Tutawaokoa wale wamchao (Mungu); na Tutawaacha wadhalimu humo wakiangukia magoti."* (**Q. 19:67-72**, Hilali-Khan)

Kama hivi sivyo. Emerick anasema kwamba watu "wenye makosa au wasiokuwa nayo, watakuwa na safari ya kutisha kupitia kwenye daraja liitwalo *Sirat,* ambalo hutenganisha shimo la Jehanamu na kuelekea Paradiso kwa upande mwingine. *Sirat* ni nyembamba kama wembe na iliyojaa makali kama ya msumeno na ncha kali." (Emerick 2004: 73-74) Hadithi nyingi hulizungumzia hili: "Allah atawaita, na kama-Sirat (daraja) litakuwa kati ya kuzimu na Mimi (Mohamedi) nitakuwa wa kwanza miongoni mwa Mitume kulivuka daraja hilo nikiwa na wafuasi wangu. Hakuna hata mmoja isipokuwa Mitume ambao baadaye watawaeza kunena wakisema 'Ewe Allah! Tuokoe sisi. Ewe Allah Tuokoe Sisi.' Kutakuwa na ndoano kama miiba ya Sa'dan kule Jehanamu. . . . Ndoano hizo zitakuwa kama miiba ya Sa'dan lakini hakuna mtu hata mmoja isipokuwa Allah ajuaye ukuu wake kwa ukubwa na hizi zitawazunguka watu kulingana na matendo yao; baadhi yao wataanguka na kubakia Jehanamu milele; wengine watapokea adhabu (watakatwa vipande vidogo vidogo) na watatoka nje ya Jehanamu, mpaka hapo Allah atakapokusudia Rehema kwa yeyote Atakayependa miongoni mwa watu wa Jehanamu, Atawaagiza Malaika kuwatoa nje ya Jehanamu wale wote ambao hawamwabudu yeyote isipokuwa Yeye pekee. Malaika watawatoa kwa kuwatambua kwa kuwatazama wanavyoabudu, kwa kuwa Allah alikataza moto wa Jehanamu kuwala wale aliowatazama. Hivyo watatoka nje ya moto, utakula miili yote ya wanadamu isipokuwa alama ile ya kuabudu (sigjida). Kwa wakati huo watatoka nje ya moto wakiwa kama mifupa. Watamwagiwa maji ya uzima na kama matokeo ya kumwagiwa maji hayo watakua kama mbegu inayokulia kando kando ya mto unaofurisha maji. (al-Bukhari: 806; angalia pia 6573, 7437, 7438; see also Muslim: 195; an-Nawawi, *Riyad:* book 1, no. 201)

Bado kwenye hadithi nyingine kwa somo hilo hilo, chakushangaza Mohamedi anaeleza kwamba "wakati waamini watakapovuka salama kupitia juu ya darajani la Jehanamu, watasimamishwa darajani kati ya Jehanamu na Paradiso watakapopambana wenyewe kwa wenyewe kwa makosa waliyotendeana wakiwa duniani, na watakapokuwa wametakaswa kutokana na dhambi zao zote, wataruhusiwa kuingia Paradiso. Kwake Yeye na kwa yule ambaye mkono wa uzima wa Mohamedi utayatambua makazi yake Paradiso vizuri Zaidi ya alivyoyatambua makazi yake ya duniani humu." (al-Bukhari: 2440) Kwa karibu haiaminiki, watu "wanaoshwa na kutakaswa "(kwa kupambanishwa)" (al-Bukhari: 6535)

2. Wokovu ni uchaguzi wa Allah kusamehe, bila kujali kazi za mtu. Kwa mgogoro wa njia hiyo ya ajabu hapo juu wa hukumu na Wokovu, Wenye mamlaka wengi wa Kiislamu hujaribu kutenganisha matendo ya mtu na wokovu. Kwa mfano, kwenye Hadithi Mohamedi alisema, "Hakuna miongoni mwenu atakayeingia Paradiso kwa umuhimu wa matendo yake pekee. Wakasema: Mjumbe wa Allah, hakuna hata wewe? Kwa hilo akasema: Hata Mimi hapana, lakini kwamba Allah atanifunika Mimi na Neema na Huruma zake." (Muslim: 2816f; angalia pia 2816a, b, c, d, e, g, 2817c, 2818a; al-Bukhari: 5673, 6463, 6464, 6467; Ibn Majah: vol. 5, book 37, no. 4201)

Mstari huu wa mamlaka unanukuu maelezo ya mwanzo ya kila sura ya Korani isipokuwa sura ya 9 ambayo Allah huiita "Faida, Mwenye kurehemu." Aya nyingi huwaita watu kutubu na kuomba msamaha wa dhambi zao kwa Allah. Kwa mfano: *"Toba inayopokelewa na Mwenyezi Mungu ni ya wale tu wanaofanya uovu kwa ujinga, kisha wakatubia papo kwa papo; basi hao ndio Mwenyezi Mungu Huipokea toba yao; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima."* (**Q. 4:17**); *"Basi ama aliyetubia na akaamini na akafanya vitendo vizuri, ni karibu atakuwa miongoni mwa wapatao ufaulu"* (**Q. 28:67**; angalia pia **Q. 3:16-17; 47:19; 48:1-2**). Emerick ananukuu kisa cha Adamu na Hawa: "Uislamu hueleza kwamba baada ya muda Mungu aliwahurumia kwa toba na unyenyekevu wa wawili hao na akawafundisha jinsi ya kuomba msamaha Kwake. Basi, walipomsihi Mungu kwa Neema yake, unafikiri

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

nini? Aliwasamehe. Mwisho wa simulizi." (Emerick 2004: 94)

Hata hivyo, Wokovu kwa toba ya mtu na kuomba msamaha kwa Allah ni tatizo jingine kwa angalau sababu mbili:

- Kwanza, msamaha haufuti madhara ya dhambi na hukumu ya Mungu kwa dhambi. "Ni ukweli kwamba Mungu, kwa ukarimu wa pendo lake, alipenda kwamba mwanadamu aokolewe. Kwa jinsi gani? Ni kupitia toba? Lakini toba haiwezi kuwa kubwa Zaidi ya hukumu na, vivyo hivyo, kuiinua adhabu kwa sababu hii haitaweza kuyafikia madai ya Haki ya Mungu. Ni ukweli kwamba wakati toba inasimama baina ya mtu anayetubu kuzikwa kwa dhambi zingine, haifuti madhara ya dhambi inayoendelea na hukumu ya Mungu iliyoambatana nayo." (Jadeed 1996-2019: 11)
- Pili, msamaha siyo wa moja kwa moja wala wa kuhakikishiwa. Korani inasema kwamba Allah anaweza kukubali au kukataa toba ya mtu: *"Na wako wengine waliokiri dhambi zao; wakachanganya vitendo vizuri na vingine vibaya. Huenda Mwenyezi Mungu Akapokea toba zao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehemevu.."* (**Q. 9:102**, fafanuzi imeongezwa) Allah huonyesha Huruma kwa yeyote amchaguaye na kumwadhibu yeyote amchaguaye kwa sababu azijuazo yeye mwenyewe: *"Vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Mwenyezi Mungu; na kama mkidhihirisha yaliyomo katika mioyo yenu, au mkiyaficha, Mwenyezi Mungu Atawatakeni hesabu ya hayo; kisha Amsamehe Amtakaye, na Amwadhibu Amtakaye; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu."* (**Q. 2:284**); *"Na ni vya Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini; Humsamehe Amtakaye na Humwadhibu Amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehemevu."* (**Q. 3:129**, Hilali-Khan); *"Allah Hakika Mwenyezi Mungu Hasamehi (dhambi ya) kushirikishwa na cho chote, na husamehe yaliyo duni ya hayo kwa Amtakaye; na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, basi bila shaka yeye amekwisha potea upotevu wa mbali."* (**Q. 4:116**; angalia pia **Q. 5:8; 48:14**). Athari anasema kwamba kama mtu atakufa akiwa ametenda dhambi "ambayo haina ushahidi kwamba ameitenda ataanzisha *kufr* [kutokuamini]—hivyo suala lake litabaki na Allah: Kama akipenda, atamwadhibu, na kama akipenda, Atamsamehe" (al-Athari 2005: 141).

3. Wokovu huamuliwa na tangazo la awali la Allah. Njia nyingine ya mamlaka ya Kiislamu kuutenga wokovu na kazi za mtu na uchaguzi wa Allah wa kusamehe au kutokusamehe lakini kumweka mtu kwenye maisha ya milele kwa tangazo la awali la Allah. Tuliona kwenye sura ya awali kwamba sura ya sita ya Makala ya sita ya Uislamu kuhusu Imani (*imam*) ni Imani kwenye tangazo la awali la Allah, linalojulikana kama, kila kitu kinachotokea ulimwenguni humu, ikiwa ni chema na kibaya, Imani na kutokuamini, hutokea kwa mapenzi na amri ya Allah, na Allah hufanya chochote apendacho. Kwa mfano, **Q. 28:68** (Hilali-Khan) anasema, *"Na Mola wako Huumba Atakavyo na Huchagua: kwao hakuna hiari: Mwenyezi Mungu Ameepukana na upungufu, na Yu juu kabisa kuliko wale wawashirikishao naye."* **Q. 4:88:** *"Basi imekuwaje ninyi kuwa makundi mawili katika habari ya wanafiki, na hali Mwenyezi Mungu Amewageuza kwa sababu ya yale waliyoyachuma? Je, mnataka kumwongoza ambaye Mwenyezi Mungu Amemhukumu kupotea? Na Aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kwamba amekwisha potea, basi kwa ajili yake hutapata njia"*; **Q. 16:93:** *"Na Mwenyezi Mungu Angalitaka, kwa yakini angaliwafanyeni kundi moja; lakini anayetaka (upotevu) Anampoteza, na anayetaka (mwongozo) Anamwongoza; na hakika mtaulizwa juu ya yale mliyokuwa mkifanya.."* Tangazo la awali la Allah hasa limejumuisha maagizo na kuumba wengine kwenda Paradiso na wengine kwenda Jehanamu: *"Na bila shaka Tumewaumba wengi wa watu na majinni ambao mwisho wao ni Jahanamu! Mioyo wanayo lakini hawafahamu kwayo, na macho wanayo lakini hawaoni kwayo, Many are the Jinns and men we have made for Hell: They have hearts wherewith they understand not, na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotevu zaidi. Hao ndio walioghafilika."* (**Q. 7:179**); *"Na Tungalitaka, Tungempa kila mtu mwongozo wake, lakini imehakiki kauli iliyotoka Kwangu: Kwa yakini Nitaijaza Jahanamu kwa wote hawa majinni na watu'"* (**Q. 32:13;** angalia pia **Q. 11:118-19**).

Hadithi nyingi zinathibitisha hivyo: "Allah aliumba watu kwa ajili ya Paradiso, Aliwaumbia hiyo wakati walipokuwa wakingali kwenye viuno vya Baba zao, Na aliwaumba watu kwa ajili ya Jehanamu, Aliwaumbia hiyo tangu wakati wakiwa kwenye viuno vya Baba zao" (Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 82; angalia pia Muslim: 2662b, c; Abi Dawud: 4713; an-Nasa'i: 1947).

Mishkat inaeleza kwamba Mohamedi alisema, "Allah alimwumba Adamu kwa wakati aliomwumba. Hivyo alilipiga bega lake la kulia na akatoa kizazi cheupe kama vile walikuwa mbegu, na alilipiga bega lake la kushoto na akatoa huko kizazi cheusi kama vile walikuwa mkaa. Ndipo alipowaambia wale waliokuwa bega lake la kulia: Bila kujali elekeeni Paradiso. Aliwaambia wale wa

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

bega lake la kushoto: Bila kujali elekeeni motoni." (Al-Tabrizi 1939: 3:117-18, no. 454w)[19]

4. Suala la Maombezi. Kama ilivyoelezwa hapo juu, Uislamu unafundisha kwamba kila mmoja ni lazima abebe mzigo wake mwenyewe wa dhambi (**Q. 6:164; 7:23; 17:15; 39:53; 53:38**). Matokeo yake ni kwamba hakuna atakayeweza kumwombea mwenzake kwenye hukumu. Hivyo, Korani inasema, *"Basi hautawafaa uombezi wa waombezi"*(**Q. 74:48**) na *"Na iogopeni siku ambayo nafsi haitaifaa nafsi nyingine cho chote, wala hayatakubaliwa kwake maombezi, wala haitapokewa fidia kwake; wala hawatasaidiwa"* (**Q. 2:48**; angalia pia **Q. 2:254; 4:109, 123; 6:51, 70; 16:111; 31:33; 40:18, 40-41**). Hata Korani inakubali kwamba hata Mohamedi hataweza kuwaombea: *"Uwaombee [Mohamedi] msamaha au usiwaombee msamaha, hata ukiwaombea msamaha mara sabini, Mwenyezi Mungu Hatawasamehe. Hayo ni kwa sababu ya kuwa wao wamemkataa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, na Mwenyezi Mungu Hawaongozi watu wavunjao amri."* (**Q. 9:80**; angalia pia **Q. 39:19**) Kwenye Hadithi, Mohamedi anakiri kwamba hataweza kufanya chochote kuokoa hata kabila lake au hata familia yake, ikiwa ni pamoja na binti yake, mama, na baba: "Wakati Allah alipoifunua aya: 'Waonye ndugu zako wa karibu,' Mjumbe wa Allah aliamka na kusema, 'Enyi watu wa Quraish (au sema neno linalofanana)! Nunua (i.e. okoa) mwenyewe (kutoka kwenye moto wa Jehanamu) kwa kuwa sitaweza kuwaokoa kwenye adhabu ya Allah; Ewe Bani 'Abd Manaf! Sitaweza kukuokoa kwenye adhabu ya Allah, Ewe Safiya, Shangazi yake na Mjumbe wa Allah! Sitaweza kukuokoa kutokana na adhabu ya Allah; Ewe Fatima bint Mohamedi! Niombe chochote kutoka kwenye utajiri wangu, lakini sitaweza kukuokoa na adhabu ya Allah.'" (al-Bukhari: 2753; angalia pia an-Nasa'i: 3644, 3646, 3647, 3648; at-Tirmidhi: vol. 5, book 44, no. 3185) Mohamedi pia alisema, "Nilitafuta ruhusa ya kusihi msamaha kwa ajili ya mama yangu, lakini yeye [Allah] hakunipa" (Muslim: 976a; angalia pia 976b; Ibn Majah: vol. 1, book 6, no. 1572; an-Nasa'i: 2034; Abi Dawud: 3234), na "Mwanadamu akauliza: Baba yangu yuko wapi, Mjumbe wa Allah? Alijibu! Baba yako yupo Jehanamu. Alipomgeukia, alisema: Baba yangu na Baba yako wapo Jehanamu." (Abi Dawud: 4718)

Hata hivyo, kama vile ambavyo Uislamu walianzisha mkanganyiko unaotokana na wokovu, pia na isivyopendeza kuruhusu maombezi kwenye hukumu. Korani inafungua uwezekano wa maombezi kwa kusema, *"Sema: Uombezi wote ni wa Mwenyezi Mungu; ufalme wa mbingu na ardhi ni Wake, kisha mtarajeshwa Kwake"* (**Q. 39:44**; angalia pia **Q. 2:255; 10:3; 19:87**). Malaika waliambiwa waombe kwa ajili ya msamaha wa wale walioko duniani (**Q. 40:7; 42:5**). **Q. 43:86** Kinyume na "hakuna aya ya maombezi" kwa kusema, *"Wala hawana uwezo wa uombezi wale wanaowaomba badala Yake, ila anayeishuhudia haki, nao wanajua.."* Wachambuzi wengi wa Kiislamu huchukulia hili kama hali kwa Mohamedi kuwa na uwezo wa ziada wa kuombea (angalia Ali 2006: Q. 43:86n.4683). Kwa ujumla Uislamu, sura ya Mohamedi huchukuliwa kwenye uwiano sawa na Masihi na, wakati huo huo Uislamu kwa ujasiri wakisema kwamba wanamwabudu Allah pekee na kwamba Nabii wao alikuwa tu mjumbe mwaminifu, kwa nafasi yake kwenye ulimwengu wa Uislamu ni kama kumweka kuwa mpatanishi muhimu kati ya Allah na watu wake" (Gilchrist 1994: 121).

Wakati wanasisitiza nafasi ya Mohamedi kwenye maombezi, Hadithi inaasili umuhimu wa maombezi bila sheria. Mbali na kule kutokuweza kuwaombea hata familia yake mwenyewe vizuri, Mohamedi anajipambanua mwenyewe kama mwombezi mkuu: "Nitakuwa miongoni mwa wazao wakubwa wa Adamu katika ile siku ya ufufuo na nitakuwa mwombezi wa kwanza na ambaye maombezi yake yatakuwa ya kwanza kukubaliwa (na Allah)" (Muslim: 2278; angalia pia al-Bukhari: 7510; Abi Dawud 4673; Ibn Majah: vol. 5, book 37, no. 4308).

F. ***Matokeo ya dhambi na wokovu kulingana na Uislamu***

Kama ilivyo kwa Mtazamo wa Wakristo juu ya asili ya mwanadamu, dhambi, na wokovu kupitia mtu na sadaka ya Kristo ilivyo ya matokeo muhimu, hivyo mtazamo wa Kiislamu wa mwanadamu, dhambi, na njia ya wokovu vina umuhimu mkubwa. Mtafaruku wa ndani wa Uislamu unaweza kuwavuta Waislamu kwenye mwelekeo wa kutatanisha, kama ambavyo matokeo mawili hapo juu yalivyoonyesha.

[19] Hadithi hii siyo tu kwamba inaelezea tangazo la awali la milele la Allah lakini pia linafunua tabia yake ya kuzivuruga chaguzi zake mwenyewe, na asili yake ya kutokujali, na jinsi alivyo na ukabila. Mohamedi mwenyewe aliwamiliki na kuwauza idadi kubwa ya Waafrika kama watumwa (al-Bukhari: 2468, 5191, 6161, 7263, vol. 6, book 60, no. 435; Muslim: 1602, 2323a; Ibn Majah: vol. 4, book 24, no. 2869; an-Nasa'i: 3728; 4184, 4621; at-Tirmidhi: 1239, 1596).Hata hivyo Mohamedi aliwadhihaki waafrika kwa ajili ya sura zao: "Mjumbe wa Allah alisema, 'Ni lazima kuwasikiliza na kuwatii, watawala wenu hata kama ni Waethiopia (weusi) watumwa ambao *vichwa vyao vilionekana kama zabibu*'" (al-Bukhari: 7142, fafanuzi imeongezwa; Ibn Majah: vol. 4, book 24, no. 2860). Kwa hiyo inaaminika kwamba Mwafrika yeyote au mtu yeyote mrithi wa Afrika ni lazima awe Muislamu.

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

1. Uislamu hawana msingi ulio wazi wa kupambana na uovu na waweza kuendeshwa na matukio na kukata tamaa. Uislamu una mtazamo usio wazi kuhusiana na dhambi na wokovu. Wakati mtu akihofia mawazo ya mafundisho ya Kiislamu pamoja kwenye "anguko" la mwanadamu na fundisho la "dhambi ya asili," mafundisho ya msingi ya Kiislamu yanakataa mafundisho hayo yote mawili. Kwa kukataa anguko la mwanadamu, kwa hiyo Uislamu wanapaswa kuuona ulimwengu kama ambavyo Allah alikusudia uwe. Zaidi, mafundisho makuu ya Uislamu ni kwamba Allah ndiye mtayarishaji na mtawala wa moja kwa moja na mhusika wa kila kitu, ikiwa ni pamoja na uovu. Msisitizo huu wa tangazo la awali la Allah litapelekea kuendeshwa na matukio na kukata tamaa. *Mishkat* inasimulia kwamba Abu Abdullah, mmoja wa washiriki wa Mohamedi mwenyewe, alipunguza kilio alipokumbuka kwamba Mohamedi alisema, "Allah alimshika mtu mmoja kwa mkono wake wa kuume na mwingine kwa mkono wake mwingine, na kusema: 'huyu ni kwa ajili ya hili, na huyu ni kwa ajili ya hili, na Sijali.' Mimi sijui ni kwa mkono upi nilioshikiliwa kati ya miwili." (Al-Tabrizi 1939: 3:118, no. 455w) Karim anatolea maoni, "Wale walioko kwenye mkono wake wa kuume wataenda Paradiso na wale walioko kwenye mkono wake wa kushoto wataenda Jehanamu. Msimulizi aliogopa ni kwa mkono gani wa Allah aliangukia ambao kwa huo utaamua mwelekeo wake." (Karim 1939: 3:118n.1563) Hata kama Mohamedi hakuwa na uhakika wa mwelekeo wake wa umilele na washiriki wake mwenyewe walipunguza kilio kwa sababu ya mwelekeo wao usiotabirika, halitakuwa jambo la kushangaza ikiwa wengine wakiona kwamba kila jitihada wanazofanya hazina maana na kujiuzulu wenyewe kutoka kwenye mwelekeo wao.

Kwa maana ya kisaikolojia, kwa matamshi ya kiufahamu ya Korani na Hadithi, kuunganisha na maagizo kwamba usihoji chochote kwenye Korani na tishio la Jehanamu kwa wale watakaojihusisha na *bid'ah* (ugunduzi), kutachochea kutokutenda chochote. Kwa mfano, Mohamedi alisema, "Yeyote atakaye leta ugunduzi ambao Allah na mjumbe wake hawakupendezwa nao, atakuwa na (mzigo wa) dhambi sawasawa na ule wa miongoni mwa wale watu waliotenda dhambi, bila ya dhihaka kutokana na dhambi zao ndogo" (Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 210; angalia pia vol. 1, book 1, no. 14, 42, 45, 50). Matokeo ya kiutendaji ya hili yameelezwa kwa kifupi na Bernard Lewis kwenye kitabu chake kiitwacho *What Went Wrong?* Bila kujali ukuaji na ongezeko kubwa la Uislamu, "ulikuwa kwa uwazi mkubwa Mashariki ya Kati na hakika kwenye ulimwengu wote wa Uislamu kwamba mambo haya yanaendelea kuwa mabaya na yenye makosa zaidi. Ukilinganisha na changamoto zao za Milenia, Ukristo, Ulimwengu wa Uislamu umekuwa maskini, dhaifu na wajinga. Kwa maendeleo ya karne ya kumi na tisa na ishirini, kwa umuhimu na kwa hiyo utawala/umiliki wa kimagharibi uko wazi kwa wote kuona." (Lewis 2002: 151) Kama Sundiata alivyoeleza, mtazamo huu wa kiulimwengu "Ni wajibu wa Waislamu kukosa maamuzi ya kuimarisha hali zao; wanafikiri kwamba hali zao ziko halisi kama yalivyo mapenzi ya Allah na kwa hiyo kutokuwa na nguvu au ruhusa ya kuingilia mwelekeo ambao Allah ameuweka kwa ajili yao. Ufahamu wa Kiislamu unadhoofisha matamanio ya wanadamu kujifunza ni jinsi gani hali inavyofanya kazi na jinsi gani inaweza kufanywa itende kazi; inawakatisha tamaa Waislamu kujifunza juu ya watu wengine, mahali, na vitu." (Sundiata 2006: 214)

2. Waislamu wengi husukumwa na mihemko, hofu na Jihadi. Emerick anadai kwamba "Allah hututuza kulingana na kiwango cha matendo yetu mema. Ni aina ya ubepari wa kidini ambao matokeo yake ni kwamba yanaweza kufanya maisha ya kila mmoja kuwa bora." (Emerick 2004: 36) Wakati mtazamo wa mtu kupata wokovu unaweza kuwa wa kutia moyo kutenda matendo mema, ikumbukwe kwamba *tafsiri* ya Uislamu wa kile kinacholeta "matendo mema" hakitokani na ujuzi wowote wa kidunia kimaadili lakini ni kwa maamrisho maalum na makatazo ya Korani na Hadithi. Kwenye hili lipo tatizo, kwa Uislamu kutokumheshimu mtu yeyote kama rafiki au adui isipokuwa kwa misingi ya kidini" (al-Athari 2005: 58). **Q. 60:1** (Hilali-Khan) anasema, *"Enyi mlioamini, msiwashike adui Zangu na adui zenu kuwa marafiki; mnawapeleka (ujumbe wa) urafiki hali wamekwisha kataa haki iliyowafikieni, wakamfukuza Mtume na ninyi kwa sababu mnamwamini Mwenyezi Mungu, Mola wenu. Kama mnaondoka kufanya jihadi katika njia Yangu na kuitafuta radhi Yangu mnarafikiana nao kwa siri; nami Najua sana mnayoyaficha na mnayoyadhihirisha; na anayefanya hayo miongoni mwenu, basi amekwisha potea njia iliyo sawa"* (angalia pia **Q. 3:28, 118; 4:89, 144; 5:51; 9:23; 58:22**). Hivyo, Shaikh Abdullah bin Baz anaeleza, "Mwamini wa kweli huwapenda waamini wenzake na kuwachukulia kama marafiki, na kuwaonyesha chuki wasiowaamini na hawawachukulii kama marafiki" (bin Baz 2002: 266).

Kuihalifu amri hii kuna matokeo ya ndani. Tamimi anasema kwamba kitu kimoja ambacho "kinakataa *Tauhid*" [na hivyo kuwahakikishia kwenda Jehanamu kwakuwa *tauhid* ni fundisho la msingi la Kiislamu kwamba Allah ni mmoja] ni "kuwasaidia wasioamini na unafiki kwa kuwatukuza na

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kuwaheshimu. Hii ni pamoja na kuwatambua kwa vyeo vya *Saiyid* (sir), kuwapokea kwa salaam za heshima na kuwapenda." (At-Tamimi 2002: 238) Hili linahusisha hata familia ya mtu mwenyewe: *"Hutapata watu wanaomwamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho kuwapenda wale wanaompinza Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, lau kama ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao. Hao ndio Ameiandika mioyoni mwao imani na Akawasaidia kwa Roho itokayo Kwake: Na Atawaingiza katika Mabustani yapitayo mito chini yao, humo watakaa. Mwenyezi Mungu Amekuwa radhi nao, na wao wamekuwa radhi naye; hao ndio kundi la Mwenyezi Mungu. Sikilizeni! Hakika kundi la Mwenyezi Mungu ndio wanaofaulu."* (**Q. 58:22**). **Q. 48:29** (Hilali-Khan) anaenda zaidi kwa kusema, *"Mohamedi (SAW)ni Mjumbe wa Allah, na walio pamoja naye ni wenye imara mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao"* (angalia pia **Q. 5:54; 66:9**).**Q. 9:29** inaenda mbali zaidi kwamba, kuwaamrisha Uislamu *"Piganeni na wale wasiomwamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya mwisho wala hawaharimishi Alivyoviharimisha Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala hawashiki dini ya haki, miongoni mwa wale waliopewa Kitabu, mpaka watoe kodi kwa mikono yao wenyewe hali wakitii na wakubali kwamba wako chini ya utawala"* (angalia pia **Q. 2:191, 216; 4:89; 9:5, 123**).

Msingi wa Jihadi kwa Uislamu umeonyeshwa na Hilali na Khan; kwa kutolea maoni kwenye **Q. 2:190**, wanaeleza, "*Al-Jihad* (mapigano matakatifu) kwa kusudi la Allah (wakiwa kwenye idadi kubwa na silaha wamepewa umuhimu mkubwa kwenye Uislamu na ni moja ya nguzo zao). Kwa *Jihadi* Uislamu uliimarishwa. . . . kwa kuachwa *Jihadi* (Allah na atulinde na hilo) Uislamu uliangamizwa na Uislamu kuangukia kwenye nafasi ya udhaifu; heshima yao ilipotea, nchi yao ilitwaliwa, utawala na mamlaka yao viliisha. *Jihadi* ni ya kazi ya lazima kwa Uislamu na kwa kila Muislamu, na yeyote atakayejaribu kujiepusha na kazi hii, au ambaye haipo kwenye kina cha moyo wake na kutamani kuifanikisha kazi hii, hufa akiwa na hali ya kuwa kwenye nafasi ya unafiki." (Hilali na Khan 1998: 39n.1) Kwa kuhofia kwamba mtu kuifikiria amri hii kwamba haifanyi tena kazi au kuwa na uchaguzi wa kuitekeleza au la, maoni ya wakati huu kwenye **Q. 2:193** (*"Na wapigeni mpaka pasiwe mateso, na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu; na kama wakiacha, basi usiweko uadui ila kwa wadhalimu."*) inaeleza, "dhambi iliyo mbaya Zaidi ni kusalitiana (*Kufr*) na kuabudu miungu (*shirk*) ambavyo ni mwanzo wa uasi kwa Allah, Mwumbaji. Kulifuta hili, Uislamu wanapaswa kupigana hadi pale ambapo uwepo wake hautakuwepo tena Ulimwenguni, na dini pekee ni hii ya Allah." (Madani 2005: 1:235; angalia pia Darussalam 2002b: 316 ["*Jihadi* (kupigana na kung'ang'ana kwa kusudi la Allah) kwa utajiri wa mtu, na nguvu, kulingana na nguvu ya mtu huyo *ni lazima kwa Uislamu*," fafanuzi imeongezwa])

Amri hizi zimethibitishwa kwenye Hadithi. Mohamedi alisema, "Nimeamrishwa kupigana na watu, hadi pale watakaposhuhudia kwamba hakuna mungu mwingine isipokuwa Allah, na kuniamini mimi (kwamba) Mimi ni mjumbe (kutoka kwa Bwana) na vile vyote nilivyovileta" (Muslim: 21b; angalia pia Muslim: 22; al-Bukhari: 25). Amri hii haikuishia kwa Mohamedi tu lakini inawahusu Uislamu wote wa wakati wote. Kwenye Hadithi nyingine alisema, "Mtapigana Wayahudi na mtawaua hata pale jiwe litakaposema: Njoo hapa Muislamu, yupo Myahudi (aliyejificha mwenyewe karibu nami); mwue huyu." (Muslim: 2921a) Pia, "Nilimsikia mjumbe wa Allah (Amani iwe juu yake) akisema: Kuelekea mwisho wa nyakati patakuwa na watu ambao ni vijana kwa umri na kutoka kwa Uislamu kama mshale umfikiavyo mnyama aliyelengwa, na Imani yao haitapitia makoo yao. Popote utakapokutana nao waueni, kwa kuwa kuwaua kutamletea mwuaji tuzo siku ya ufufuo." (Abi Dawud: 4767) Kwa kweli, wakati kabila la Khazraj walipokuwa wakiapa kiapo cha uaminifu mbele ya Mohamedi, mtu alikiri uapo kwa kusema, "Kwa kiapo hiki cha uaminifu kwake unaahidi mwenyewe kwamba utapigana vita kinyume na wanadamu wote" (al-Tabari 1988: 134).

Korani inasema kwamba Allah huwakubali wale wapiganao na wale waliosalia nyumbani, na kuahidi tuzo kubwa kwa wapiganaji (**Q. 4:95**; angalia pia **Q. 61:4**). Kwa nyongeza, zawadi maalum inatolewa kwenye Korani na Hadithi kwa kushiriki kwenye Jihadi na hata kufia huko. **Q. 47:4-6** inasema, *"Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru wapigeni shingo mpaka mmewashinda, kisha wafungeni sana, tena waacheni kwa ihsani au kwa kujikomboa, hata vita vitue mizigo yake. Ndivyo hivyo; na kama Mwenyezi Mungu Angalitaka Angalijilipiza kisasi kwao, lakini Huwajaribu baadhi yenu kwa mikono ya watu wengine. Na wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu basi Hataviharibu kamwe vitendo vyao. Atawaongoza na kurekebisha mienendo yao. Na Atawaingiza katika bustani Aliyoipamba na kuitunza kwa ajili yao."* (angalia pia **Q. 9:88-89**) Kwenye Hadithi, "Mjumbe wa Allah alisema, 'Allah anamhakikishia ambaye atapigania jihadi kwa kusudi lake na hakuna cha kumfunga yeye kwenda isipokuwa Jihadi kwa kusudi lake, na kuliamini neno lake, kwamba atamkiri na kumwingiza Paradiso au kumrejesha na tuzo au nyara ambazo amezipata nyumbani kwake pale

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

alipoondokea.'" (al-Bukhari: 7457; angalia pia 36, 3123, 4046, 7463) Zaidi, "Yeyote apiganaye kwa ajili ya Allah, Mwenye nguvu na mwingi wa utukufu, kwa kipindi cha urefu kati ya vipindi viwili vya ngamia anyonyeshaye, Amehakikishiwa kuingia Paradiso." (an-Nasa'i: 3141)[20]

Uislamu pia wanao "mwisho wa kuhalalisha maana" mbinu ya kuongopea na kuhadaa dhidi ya kuwa mkweli. Kwa kweli, Uislamu umeendeleza fundisho la uongo liitwalo *taqiyya,* ambalo kwa uhalisia limezuiliwa miongoni mwa Uislamu wa Shi'ah (angalia Sookhdeo 2004: 89-92); kwa WaSunni linalofanana na hilo huitwa *muda'rat* ("Baadhi ya mafundisho ya Kiislamu" 2018: n.p. [Makala hii inajadili suala hili kwa kina kiasi fulani]). Fundisho la msingi kwenye Korani kwa baadhi ya mistari na hadithi nyingi. Kwenye maoni yake **Q. 3:28** (*"Waaminio wasiwafanye makafiri kuwa wapenzi badala ya waaminio; na atakayefanya hivyo, basi hatakuwa na cho chote kwa Mwenyezi Mungu, isipokuwa ya kwamba mjilinde nao kabisa; na Mwenyezi Mungu anawatahadharisheni na nafsi Yake; na marudio ni kwa Mwenyezi Mungu"*), Ibn Kathir analitafakari suala la Uislamu wanao uhofia usalama wao kwa wale wasio Uislamu: "Kwenye suala hili, waumini hawa huruhusiwa kuonyesha urafiki kwa wasioamini (wasio Uislamu) kwa nje tu, lakini kamwe siyo kwa ndani. Kwa mfano, Al-Bukhari imenukuu kwamba Abu Ad-Darda' alisema, 'Tunatabasamu kwenye nyuso za baadhi ya watu ingawaje mioyo yetu inawalaani.'" (Ibn Kathir, *Tafsir,* n.d.: Q. 3:28, maoni) *Sahih al-Bukhari* pia anatutaarifu kwamba mmoja wa washiriki wa karibu wa Mohamedi akisema, "Ninaweza kusema tu kumdanganya adui yangu" (al-Bukhari: 6930). Kwenye suala hili, Korani inamwelezea "adui" kama ifuatayo: *"Wasioamini (Uislamu) ni maadui wa wazi kwako"* (**Q. 4:101**; Tafsiri ya Hilali-Khan kwenye aya hii inasema, *"wasioamini(kwenye Uislamu) wakati wote ni maadui zako wa wazi"*.

Uongo na udanganyifu vinaruhusiwa kwa ajili ya *kuwaua* wasio Uislamu: "Nabii alisema, 'Ni nani aliye tayari kumwua Ka'b bin Ashraf (i.e. Myahudi).' Mohamedi bin Maslama alijibu, 'Ungependa mimi nimwue?' Nabii akakubali kwa kuthibitisha. Mohamedi bin Maslama alisema, 'Basi niruhusu kusema kile ninachokipenda.' Nabii akamjibu, 'Nakuruhusu.'" (al-Bukhari: 3032; angalia pia 4037; Muslim: 1801) Udanganyifu hata hivyo unaruhusiwa kwa ajili ya kujipatia utajiri: "Baada ya ushindi wa mji wa Khaybar na Uislamu, Nabii (Ma) walifikiwa na Hajaj Ibn 'Aalat na kuambiwa: 'Ewe Nabii wa Allah: Ninao kule Maka baadhi ya utajiri uzidio na baadhi ya ndugu, na ningependa warudi; Samahani kama nitakuharibia mwezi wako (kuepuka mateso)?' Nabii (Ma) wakamtaka radhi na kusema: 'Sema chochote utakacho kusema.'" (Abbas 1995-2014: Al-Taqiyya, Dissimulation Part 1, ref. 8) Abdul-Wahhab inatuarifu kwamba Ibn Mas'ud (mmoja wa washiriki wa karibu wa Mohamedi) alisema, "Kuapa kwa Allah wakati naongea uongo inapendeza Zaidi kuliko kuapa kwa mwingine yeyeote wakati nazungumza ukweli" (Abdul-Wahhab 2002: 142). Imani ya sita ya WaShi'ah, Ja'far as-Sadiq (699-765), hata hivyo inasema kwamba "Yule ambaye hana *taqiyyah,* hana dini." (Enayat 2005: 176) Vivyo hivyo, Hamid Enayat anahitimisha hivi "kuufanyia kazi (Uongo) [*taqiyya*] imekuwa sheria ya tabia ya uma popote palipo na msuguano kati ya Imani na usumbufu ." (Ibid.: 177)

Mfumo wa "Uadilifu wa Uislamu" na wokovu una misingi yake kwenye utii wa kutokuuliza swali kwa kujaribu kupingana na Korani na Mohamedi pia kuonyesha tofauti ya msingi wa Uadilifu kati ya Ukristo na Uislamu: Inapolazimika Mkristo kusema uongo, kudanganya, na kumwua asiye na hatia, hutenda yasiyotabirika/kubalika kutokana na Imani yao na huwa *sio waaminifu* kwa Kristo; Pale Waislamu wanaposema uongo, kudanganya, na kumwua mtu asiye na hatia hutenda yale ambayo yanakubalika na Imani yao na wanakuwa ni *watiifu* kwa Mohamedi na kwa Korani.[21] Mfumo huu wa

[20] Mtazamo wa Mohamedi mwenyewe juu ya jihadi umeelezwa kwa wazi kwenye hadithi: "Mjumbe wa Allah alisema, 'Kwake yeye ambaye uzima wangu uko mikononi mwake, Nitalipigania kusudi la Allah na hatimaye kulifia na kisha kufufuliwa tena (kuwa hai) na kulifia tena na kisha kuwa hai tena na kisha kulifia na kuwa hai tena na kisha kulifia na kisha (kuwa hai tena).'" (al-Bukhari: 7227; angalia pia 36, 2795, 2797, 2972, 7226. Kwa kina cha Kikorani kwa jihadi, angalia hapo chini kipengele **5.VIII.C.** ***Fundisho la kuondolewa lina madhara makubwa kwa kila anayedai kuwa Uislamu ni "dini ya amani."*** Mjadala ulio bora wa jihadi, historia yake, na theolojia ya Uislamu ya vita na amani, umefanywa na Patrick Sookhdeo, kwenye kitabu chake kiitwacho *Understanding Islamic Terrorism* (Pewsey, Wiltshire, UK: Isaac Publishing, 2004).

[21] Sundiata anachunguza kwamba "matendoo ya kutisha ya Jumuiya ya Uislamu na Ugaidi wa Uislamu unaweza kuangaliwa kuwa ni kile Mohamedi mwenyewe alichokisema, au alichokiagiza" (Sundiata 2006: 17). Kwa maneno mengine, "Wale wanaohukumu kuwa ukandamizaji,unafiki na vitendo vya vurugu hufanyika kwa Jina la Yesu wa Nazareti watamkuta Yesu huyo huyo kwenye upande wao kwa sababu bila kukubaliana alivikemea vitendo hivyo na Yeye mwenyewe alikandamizwa na kuuawa bila kufanya kosa lolote" (Ibid.: 18). Anakumbusha maoni ya Shayesteh, "Tunajua kwamba kile kiitwacho ulimwengu wa Ukristo kwa kiwango kikubwa wameshindwa wenyewe kujitoa kwa Yesu Kristo. Kwa hiyo, ni *kutokumwamin* Yesu Kristo kunakoeneza Uasherati miongoni mwa wale wanaoonekana wanaishi chini ya Jina la Ukristo. Kwa kuwa Injili ya Yesu Kristo, ipo aina moja tu ya Wakristo duniani, wale tu ambao wameokolewa

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

"uadilifu wa Kiislamu" kimsingi hutuongoza kwenye mapinduzi, uongo, na vurugu, kwa kuwa mambo haya yote kwa wazi na kwa kurudiwa yamesisitizwa kwenye Korani yote na Hadithi. Kama mwandishi Muislamu Abdel Rahman al-Rashed alivyoandika, "Ni ukweli usiopingika kwamba siyo Waislamu wote ni Magaidi, lakini ni ukweli unaofanana, na kwa ukweli mchungu ni kwamba, karibia magaidi wote ni Waislamu" (al-Rashed 2004: n.p.). Kwa kiwango cha kukaribia asilimia 75% ya zaidi ya matukio 12,500 ya mauaji ya kigaidi yaliyotekelezwa mwaka 2011 yalitekelezwa na Waislamu ("Muslim Statistics (Terrorism)" 2016: Worldwide) Tafiti mbalimbali duniani kote zinaonyesha kwamba Waislamu wanaosaidia vurugu na machafuko ya kigaidi siyo "kikundi kidogo cha wenye itikadi kali" ("Muslim Opinion Polls" 2002-2019; Shapiro 2014). Kwa mfano, kura ya hivi karibuni iliyofanywa na kituo cha Runinga cha Kiarabu cha Al Jazeeral, asilimia 81% ya waliojibu walikubali kwamba wanasaidiwa na "muungano wa ushindi wa jumuiya ya Kiislamu kule Iraq na Syria (ISIS)" (Schachtel 2015: n.p.). Hili linaongeza ukweli wa hali ya juu kwamba Uislamu wanaichukulia Imani yao kwa umakini, kwakuwa Mohamedi alisema, "Hakuna mwamini wa kweli mpaka pale tamanio lake litakapokuwa kutii kwa yale ambayo niliyaleta" (al-Nawawi, *40 Hadith*: 41), na kwamba linajumuisha vurugu na uongo.

3. <u>Hakuna uhakika wa wokovu kwenye Uislamu.</u> Mohamedi alisema, "Hayupo kati yenu ambaye hana makazi mawili: Makazi ya Paradiso na makazi ya Jehanamu. Kama akifa na akaingia Jehanamu, watu wa Paradiso watayarithi makazi yake." (Ibn Majah: vol. 5, book 37, no. 4341) Yeye pia alisema, "Jannah [Paradiso] ipo karibu na kila mmoja wenu kuliko soli ya viatu vyenu, na hivyo ni (Jehanamu) ya moto" (al-Nawawi, *Riyad*: book 1, no. 105). Akiwa na orodha ndefu ya mambo ya kufanya na yale yasiyo ya kufanya (yaliyokubaliwa na yaliyokatazwa) kwamba hakuna anayeweza kwa uhalisi kuzishika na kwa ukweli kwamba shirk itakuwa imefichwa kama siafu weusi kwenye mwamba mweusi wakati wa usiku, Hakuna Muislamu mwenye uhakika kama ataingia Paradiso au Jehanamu. Hakika, Athari anaeleza kwamba waamini wengi wa Kiislamu "wanafikiri kwamba mtu anapaswa kusema *insha' Allah (Allah akipenda)* anapojieleza mwenyewe kama Muumini, i.e., mtu anapaswa kusema, 'Mimi ni muumini, kama Allah atapenda.' Hawajielezi kwa uhakika kwamba wao ni waamini, kwa sababu ya nguvu ya hofu ya kumuogopa Allah, Imani yao kwenye mapenzi matukufu na maamrisho, na kusita kwao kujisifu wenyewe." (al-Athari 2005: 135) Kwa sababu "mioyo ipo kati ya vidole viwili vya vidole vya Allah [na] Huvibadilisha apendavyo yeye" (at-Tirmidhi: vol. 4, book 6, no. 2140), hata Abu Bakr, mshiriki wa karibu sana wa Mohamedi na Khalifa wa kwanza, "huuweka mkono wake wa kuume kwenye moyo wake na kurudia kwa sauti maombi ya Mjumbe wa Allah . . . : 'Ewe (Allah) unayeibadilisha mioyo! Uimarishe moyo wangu kwenye dini yako (ya Uislamu).' Ingawa alikuwa nayo hiyo imani, ambayo ilikuwa kuu sana kiasi cha kuwatosheleza wakaaji wote wa Ulimwengu, alikuwa akihofia kwamba moyo wake ungeweza kumkosesha. Hivyo, alikuwa akitamka, wakati akilia: 'Kwa hili kwamba nimekuwa mti uliopigwa!' Popote alipokumbushwa nafasi yake machoni pa Allah, angesema: 'Kwa Allah! Sijihakikishii na kujisikia salama kutokana na adhabu ya Allah, hata kam mguu wangu mmoja uko Paradiso.'" (Khalid 2005: 98-99)

Zaidi, bila kujali fundisho la msingi la Uislamu kwamba mtoto hana dhambi hata atakapofikia umri wa balehe, kulingana na hadithi, hata mtoto ambaye hajafikia umri wa kubalehe hana uhakika na wokovu wake "Mjumbe wa Allah aliitwa kuongoza sala ya mazishi ya mtoto wa Ansar. Nasema: Mjumbe wa Allah, ipo furaha kwa mtoto huyu ambaye ni ndege kwenye ndege za Paradiso kwa sababu hawatendi dhambi na hajafikia umri wa mtu kutenda dhambi. Alisema: 'A'isha, kwa safari yake, inaweza kuwa vinginevyo, kwa sababu Mungu aliwaumba kwa Paradiso wale ambao wanafaa kwa hilo wakati wakiwa bado kwenye viuno vya Baba zao na kuwaumba kwa ajili ya Jehanamu wale watakaokwenda Jehanamu. Aliwaumba wao kwa ajili ya Jehanamu wakiwa bado kwenye viuno vya Baba zao." (Muslim: 2662c; angalia pia Ibn Majah: vol. 1, book 1, no. 82) Vivyo hivyo, hata wale waislamu waliojitoa kabisa "wanaamini kwamba mwelekeo wa milele wa watu haujulikani na hakuna mtu ajuaye mwisho wake utakuwaje" (al-Athari 2005: 148). Sababu nyingine kwamba Uislamu hautoi uhakika wa wokovu ni kwa sababu unakataa uwezekano wa wafuasi wake kuyaishi maisha ya Kimungu hapa duniani. . . . Kinyume na Korani, wanaamini kwamba hauwezi kuokoka ukiwa kwenye maisha ya hapa duniani, lakini kwenye maisha baada ya kifo ingawa mwelekeo wa mtu baada ya kifo haueleweki." (Shayesteh 2004: 131, 202) Kwamba, kwa sababu hiyo, ni kinyume na Ukristo, ambao wokovu "hupokelewa duniani na hudumu milele" (Ibid.: 202).

---

kutoka kwenye utawala wa uasherati. Kwa hiyo, Uislamu hawapaswi kuchukulia Uasherati wa wale wajiitao jumuiya ya Kikristo kama ishara ya Imani ya Kikristo kuwa na mapungufu." (Shayesteh 2004: 204, fafanuzi imeongezwa)

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Mohamedi mwenyewe hakuwa na uhakika wa wokovu. Kwenye Korani, baada ya kusema kwamba hakuleta ujumbe mpya, Mohamedi alisema, "*wala Mimi sielewi kile kitakachofanyika kwangu au kwenu*" (**Q. 46:9**). Hadithi pia inashuhudia ukweli kwamba Mohamedi hakuwa na uhakika wa wokovu. Kwenye haditi moja, alitembelea kwenye nyumba ambayo mtu alikuwa amekufa. Mohamedi alisema, "Kama ilivyo kwake, mauti imekuja kwake na Mimi namtakia mema yote toka kwa Allah. Kwa Allah, ingawa Mimi ni Mjumbe wake, Wala Mimi sijui nini kitatokea kwangu mimi, wala kwenu." (al-Bukhari: 7018; angalia pia 1243, 3929)

Kwa kweli, Mohamedi alikuwa akiogopa sana kifo na adhabu ya Allah: "Aisha alisema kwamba Myahudi alikuja kwake na akazungumzia adhabu ya kaburi, akamwambia, 'Namwomba Allah akulinde na adhabu ya kaburi.' Baadaye Aisha alimwuliza Mjumbe wa Allah kuhusiana na adhabu ya kaburi. Alisema, 'Ndiyo, (ipo) adhabu kaburini.' Aisha aliongeza, 'Baada ya hiyo sitamwona tena Mjumbe wa Allah lakini kutafuta hifadhi kwa Allah kutokana na adhabu ya kaburi kwa kila maombi aliyokuwa akiyaomba'" (al-Bukhari: 1372) Mohamedi hakuwa salama na kuhofia adhabu ya Allah kwamba ingekuwa kubwa kiasi kwamba ilimsababishia usumbufu mkubwa kila upepo mkali ulipovuma, kupatwa kulipotokea (kwa jua au mwezi), au hata wingu lilipotanda angani tu—kwa sababu alifikiri matukio hayo ya asili yaliashiria kwamba siku ya hukumu imefika! "Popote upepo mkali ulipovuma, hofu ilionekana usoni mwa Nabii (akiogopa kwamba upepo ungeweza kuwa ishara ya hasira ya Allah)." (al-Bukhari: 1034) "Jua lilipopatwa Nabii aliinuka, akihofia kuwa inawezekana saa imefika (i.e. Siku ya hukumu). Alikuwa akienda msikitini na kufanya maombi kwa muda mrefu (Qiyam), akipiga magoti na kusujudu kwa kiwango ambacho sikuwahi kukiona kabisa kwake akifanya hivyo alisema, 'Ishara hizi ambazo Allah huzituma hazitokei kwa sababu ya maisha au kifo cha mtu, lakini Allah huwaogopesha wamwabuduo kwayo. Hivyo, unapoona chochote kama hicho, endelea kumkumbuka Allah, msihi na kumwomba msamaha.'" (al-Bukhari: 1059) "Aisha alisema, 'Kama Nabii angeona mawingu angani, angezunguka huku na kule akitetemeka, akitoka nje na kuingia ndani, na hata rangi ya uso wake ingebadilika, na kama kungenyesha, angejisikia kupumzika.' Hivyo Aisha aliielewa hali yake hiyo. Hivyo Nabii alisema, 'Sijui (ninaogopa), inaweza kuwa sawa na kile kilichotokea kwa baadhi ya watu wanaoonekana kwenye Korani tukufu kwenye Aya zifuatazo: - Basi walipoliona wingu likiyaelekea mabonde yao, wakasema: Wingu hili litatunyeshea mvua. Bali haya ni yale yale myaombayo kwa upesi: ni upepo ulio na adhabu iumizayo. (46.24)'" (al-Bukhari: 3206) Wakati wa kufa kwake, Mohamedi hakuwa na uhakika wa wokovu na alikuwa akimwita Allah amsamehe. Mkewe Aisha alisimulia, "Akiwa kwenye hali ya kufa nilimsikia mjumbe wa Allah akisema: 'Ewe Allah, nisamehe na unirehemu, na uniunganishe na Wafuasi wa hali ya juu'" (at-Tirmidhi: 3496; angalia pia al-Bukhari: 4440, 5674).

Kwakuwa hata Mohamedi hakuwa na uhakika wa waokovu, hakuna Muislamu mwenye uwezekano wa uhakika wa hatima yake ya milele. Kumbuka hili kulingana na **Q. 33:56** waamini na hata malaika wanapaswa kuomba kwa ajili ya Mohamedi. Hili linaacha swali: Kama Waislamu wanapaswa kumwombea Mohamedi, ni nani atakayeenda kuwaombea wao?

4. <u>Allah siyo Mtakatifu wala mwenye Haki.</u> Kama tulivyoona mwanzoni, Ukristo unao "mtazamo wa juu kuhusiana na dhambi (i.e., dhambi wakati wote na kimsingi ni kinyume na Mungu) kwa sababu Ukristo unao mtazamo wa juu wa utakatifu wa Mungu (i.e., Mungu ni mtakatifu mkamilifu kwa hiyo hawezi kukaa karibu na uwepo wa dhambi) na mtazamo wa hali ya juu wa ubinadamu (i.e., watu "wameumbwa kwa sura ya mungu" na dhambi iliifuta sura ile kwa sababu ni kinyume na mfanano wa Mungu); kwa sababu hiyo, Msamaha wa Mungu ulikuwa wa gharama. Kinyume chake, Uislamu una "mtazamo finyu" wa dhambi, ambao lazima unamaanisha kwamba Uislamu una mtazamo finyu wa utakatifu wa Allah. Hivyo, Korani inaashiria kwamba dhambi ya mwanadamu haina madhara yoyote kwa Mungu: *"Na anayejitahidi, basi bila shaka hujitahidi kwa ajili ya nafsi yake; kwa hakika Mwenyezi Mungu si mhitaji kwa walimwengu"* (**Q. 29:6**; angalia pia **Q. 14:8; 22:64; 35:15; 47:38**). Kwenye kutolea maoni aya hizi, Ali anaeleza, "Wakati tunapozungumzia kumtumikia Allah, siyo kwamba tunazungumzia faida yoyote kutoka kwake. Kwa kuwa hana uhitaji, na yuko huru kwa viumbe vyake vyote (*Cf.* 14:8). Kwa kufanana na mapenzi yake, tunatafuta mazuri yetu wenyewe, kama kwa kujiachilia kwenye uovu tunajiumiza wenyewe." (Ali 2006: Q. 29:6n.3428) Kutokujali moja kwa moja kwa Allah na kutokupata madhara kwa dhambi ya mwanadamu (au wokovu) inathibitishwa kwenye hadithi: "alisema kwa wale waliokuwa mkono wake wa kuume: Bila kujali waelekee Paradiso. Aliwaambia waliokuwa mkono wake wa kushoto: Bila kujali waelekee motoni." (Al-Tabrizi 1939: 3:117-18, no. 454w; angalia pia no. 455w) Kwa maneno mengine, dhambi zetu ni kinyume na nafsi zetu wenyewe lakini siyo dhambi kinyume na mapenzi ya Mungu (angalia **Q. 7:23; 39:53; 41:46; 47:38**).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

Aya hizi na mtazamo wa Uislamu wa dhambi na wokovu zinamaanisha kwamba Allah siyo mtakatifu na asiyehaki kwa angalau njia nne:

- Kwanza, kwakuwa Allah "hajali" kuhusiana na watu kuwa wenye haki au watenda dhambi, na dhambi haina madhara yoyote kwake kwenye tukio lolote, siyo mtakatifu kwasababu kimsingi dhambi haimaanishi chochote kwake na kwa hiyo hana haki ya kuwahukumu watu kwa matendo yao.
- Pili, kwa kiwango kwamba wokovu hupimwa kwa matendo mema ya mtu kutoka kwenye matendo mabaya ya mtu huyo, inaonyesha kwamba Allah siyo mtakatifu na hana haki kwa sababu hukubali matendo *ya muda na yasiyo makamilifu* (ambayo kwa asili yake hayambadilishi mtu mtenda dhambi kuwa mtu mtakatifu) kwa kutosheka na dhambi ambayo huiharibu nafsi ya mtu *kabisa*, kuleta madhara kwa wengine, nakuleta madhara kwa ulimwengu.
- Tatu, kwa tangazo lake la awali na kuingilia kwa matendo Allah ni sababu ya *moja kwa moja* ya dhambi ya mwanadamu, siyo mtakatifu kwa kuwasababishia watu kutenda dhambi na siyo mwenye haki kuwahukumu watu kwa dhambi alizoziamuru na kuzisababisha.
- Nne, kwa kuyaheshimu maamuzi ya Allah kuchagua kusamehe dhambi za watu bure na kwa wakati huo huo kuonekana kwake kwamba haki imetendeka (kama, kwa mfano, Kristo alikamilisha pale msalabani), "Kama Mungu angesamehe kwa kutumia Rehema zake tu, angeepuka madai ya Haki na kutokulaumiwa kwake. Kuepuka huko kungeashiria kutokukamilika kwake kuwa Mungu. Kwa hakika kitendo kama hicho kisingestahili kwa Utukufu wa Mungu." (Khan 1992: 23) Ghabril analiweka hili hivi: "Kwa kuwa ni ukweli [Allah] anaweza kufanya kama impendezavyo, bado hatapendezwa na kile kinachopingana na sifa yake ya asili na sheria zake tukufu. Fikiria kuwa Hakimu anamsamehe mwuaji wa ndugu yako baada ya uhalifu kuwa umeshathibitishwa, na akaendelea mbele Zaidi na kumsamehe. Utamchukulia kama mwenye haki? Hapana kabisa! Utamchukulia kuwa asiye na haki kwa sababu ameihalifu sheria." (Ghabril 2003: 24) Vivyo hivyo, kwa Allah "kusamehe tu" kiwango cha kusema kwamba hakuna tofauti kati ya mema na mabaya, haki au kutokuwa na haki. Kwa namna hiyo Allah pia amejifunua mwenyewe kuwa siyo mtakatifu kwa sababu labda sheria zake siyo takatifu kwa kuanzia au, kama ni takatifu, hazihitaji kukamilishwa hivyo siyo takatifu. Kwa Allah "kusamehe tu" pia kunamfanya yeye kuwa asiye na kina na mwenye kigeugeu hata kuliko mwanadamu, kwa kuwa mwanadamu anatambua kwamba kusamehe kunawakilisha tatizo kwa kubadilisha jicho lisiloona kuwa uovu au kumaanisha kwamba mtu anayesamehe ni lazima yeye kubeba gharama za mkosaji.

5. <u>Kwa sababu wokovu wa Kiislamu hauhusiani na asili ya msingi ya mwanadamu, Paradiso ya Kiislamu itakuwa haina maana kama ilivyo dunia.</u> Ingawa Waislamu pia wanatambua kwamba asili ya mwanadamu ni dhaifu sana, hakuna hata mpango mmoja wa Kiislamu wa wokovu unaolionyesha hili au kujifanya kuwapa watu moyo mpya, ufahamu, Roho au asili mpya. "Wanachokifanya ni kulazimisha sheria ya kidini [*sheria*] Kwa msukumo wa kisiasa huwezi kuwahakikishia jamii kuwa na maadili bora au hata ya mtu binafsi" (Shayesteh 2004: 202; see also Ghabril 2003: 24 ["siyo kwa kumwadhibu mwizi kwa kumfunga jela au kwa kukata mikono yake au kwa kumpiga mawe kahaba kutakakobadilisha hisia za mwizi wala za kahaba"]). Nehls na Eric wanaonyesha, "Waislamu hupitia maumivu makali kwa kuziangalia sheria ngumu kupita kiasi za Kiislamu (Sheria, Fiqh) kwa matumaini kwamba zitawaongoza kuhesabiwa haki Siku ya hukumu. Lakini hakuna sheria duniani inayomfanya mtu kuwa mwenyewe Haki. Sheria huamua kipi ni haki na kipi ni kosa, lakini haiwezi kumfanya mtu kuwa sahihi. Ni kiwango tu ambacho kwa hicho sheria hupitishwa." (Nehls and Eric 2010: 112)

Ghabril anajadili tatizo hili muhimu ndani ya Uislamu: "Mbingu au Paradiso, ambayo watu hutamani kupaingia, ni mahali safi ambapo ni wale tu ambao wametakaswa na waliofanywa wenye haki wanaoweza kupaingia. Hivyo yule ambaye anatenda dhambi moja anakosea na kuwa najisi. . . . Fikiria Muislamu ambaye amevalia joho jeupe na wakati akienda zake kwenye maombi tone la uchafu linaangukia joho lake au linamwangukia yeye mwenyewe. Hahesabiwi kuwa najisi? Kama hali ndiyo hiyo hapaswi kurudi nyumbani na kujitakasa mwenyewe ili aweze kuanza kuomba? Hii ni hali ya mwanadamu kumwelekea Mungu kwenye hali ya kuwa safi au kuwa najisi. Kwa hiyo haiwezekani kwa mwamini kuingia Paradiso kabla ya utakaso mkamilifu na upya wa moyo. Kwa kuwa kama angetakaswa dhambi zake na kusamehewa makosa yake, bado vimelea vya uovu vingebakia kwenye moyo wake, angebaki kuwa mwovu na asingestahili kuingia mbinguni." (Ghabril 2003: 24)[22] Matokeo

[22] Haya ni matokeo ya Hadithi moja ambayo inaanza kwa kusema, "Mjumbe wa Allah alisema, 'Enyi watu! Allah ni mtakatifu na, kwa hiyo, hukubali kile tu ambacho ni kitakatifu'" (al-Nawawi, *Riyad*: book 19, no. 44).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

ni kwamba bila kujali nadharia ya wokovu wa Kiislamu ambayo mtu huitumia, tabia za watu hazitabadilika na hakutakuwa na madai ya kufanyika hivyo. Hivyo, hawastahili kuingia mbinguni, na mbingu haiwastahili.

Hili siyo tu tatizo la kinadharia. Daniel Shayesteh anaonyesha kwamba kwenye Uislamu, "Tunajua kutokana na Korani kwamba Adamu na Hawa walifukuzwa kutoka kwenye bustani ya Edeni na Allah baada ya kutenda dhambi ya Kwanza. Allah asingeendelea kubeba mara ya pili dhambi yao kwenye Bustani ya Edeni na kuwafukuza kwenye uwepo wake. Hata hivyo, hali imebadilika sasa; Watu wanaweza kuingia Paradiso bila kujali unajisi wa mioyo yao." (Shayesteh 2003: 72) Mohamedi alilikiri hili wakati akijadili habari ya maombezi yake: "Nilipewa kuchagua baina ya kuingizwa Paradiso, na nilichagua maombezi, kwa sababu ni ya jumla na ya kutosheleza. Unafikiri ni kwa ajili ya umaarufu? Hapana, ni kwa ajili ya wenye dhambi wasio safi." (Ibn Majah: vol 5, book 37, no. 4311) Hali ni mbaya Zaidi hata kuliko hiyo: *Shetani anaweza kuingia Paradiso ya Kiislamu!* Kwenye maoni yake kwenye Korani, Ibn Kathir anaeleza, "Wanazuoni wengi husema kwamba Shetani kwa asili alikuwa amekatazwa kuingia Paradiso, lakini kuna wakati ambao inasemekana aliingia huko kwa siri. Kwa mfano, Tawrah alielezwa kwamba Ibilisi alijificha kwenye mdomo wa nyoka na aliingia Paradiso. Baadhi ya Wanazuoni walisema kwamba inawezekana kabisa kwamba Shetani aliwapotosha Adamu na Hawa wakati akitoka Paradiso. Baadhi ya wanazuoni husema kwamba aliwapotosha alipokuwa duniani, wakati wakingali bado mbinguni, kama ilivyoelezwa na Az-Zamakhshari." (Ibn Kathir, *Tafsir*, n.d.: Q. 2:36, maoni)

Kwa nyongeza, wakaaji wa Paradiso ya Kiislamu wako huru kujihusisha na shughuli ambazo kwa uhalisia zimekatazwa na kuonekana kuwa ni uovu duniani. Yahiya Emerick anakiri kwamba"karibia raha zote za dunia zimezuiliwa au zimekatazwa kwa Uislamu, hivyo tuzo yao ya kumtii Mungu kwenye maisha haya ni kuwa huru kuzishiriki kwenye ulimwengu ule ujao" (Emerick 2004: 38). Kwa mfano, Korani imewazuilia Uislamu kuoa Zaidi ya wanawake wanne (**Q. 4:3**). Hata hivyo, kule Paradiso Mohamedi alisema, "Hakuna hata mtu mmoja ambaye Allah atamwingiza Paradiso lakini Allah atamwozesha wanawake sabini na wawili, wawili kutoka kati ya wale walio kwenye kundi la warembo sana; angalia **Q. 44:54; 52:20; 55:72**] na sabini kutoka kwenye urithi wake kutoka kwa watu wa Jehanamu, wote watakuwa na nyuso za kuvutia na watakuwa na wanaume ambao kamwe hawatabadilika)" (Ibn Majah: vol. 5, book 37, no. 4337).[23] Sheria za Kiislamu zisizotamkika zinaonekana kwenye ukweli kwamba vitu vya karibu vitakavyo wapeleka watu Jehanamu bila shaka ni tuzo za Paradiso! **Q. 5:90** (Hilali-Khan) anasema, *"Enyi mlioamini! bila shaka vileo na kamari na masanamu (ya kuabudu) na mishale (ya ramli) ni uchafu wa kazi ya Shetani. Basi jiepusheni nayo, ili mpate kufaulul."* Kwenye Hadithi Mohamedi alisema, "Allah alikataza Kamari [Vileo], na kila Kamari ni kinyume cha Sheria" (an-Nasa'i: 5700; angalia pia al-Bukhari: 5579; Muslim: 2003b; Abi Dawud: 3685; Ibn Majah: vol. 4, book 30, no. 3390). Hata hivyo, kule Paradiso patakuwa na *"mito ya mvinyo(pombe),furaha kwa wale wanywao"* (**Q. 47:15**). Hata hivyo, "Yeyote anywaye kilevi duniani na hakutubu (kabla ya kufa), hataifaidi kwenye ulimwengu ule ujao" (al-Bukhari: 5575). Hivyo, Korani na Hadithi hazitoi mwelekeo wa uadilifu hata kidogo; ni sheria tu zisizo na mpangilio ambazo zaweza kubadilishwa wakati wowote kwa tamaa za Allah (au Mohamedi).[24] Hitimisho lisiloepukika ni hili kwamba "Paradiso ya Kiislamu" itafanana kabisa na dunia hii kama siyo kuwa itakuwa mbaya zaidi—iliyojaa wakaaji ambao wana asili ya dhambi kama walivyokuwa duniani, wakijihusisha na shughuli

[23] Siyo jambo la kushangaza kuona kwamba, hakuna ahadi yoyote kwa mwanamke yeyote ambaye ataweza kuingia Paradiso.

[24] Nyongeza ya kukatazwa kilevi, Mohamedi aliagiza, "Msivae Hariri na msinywe kwenye vyombo vya dhahbu wala vya fedha, na msile kwa kutumia vyombo vya aina hiyo (i.e., dhahabu na fedha), kwa kuwa hivyo ni vya kwao (wale wasioamini) kwenye ulimwengu huu" (Muslim: 2067g; angalia pia 2065b, c, 2067a; al-Bukhari: 5832, 5833, 5837; an-Nans-i: 5136, 5301; Abi Dawud 3723; Ibn Majah: vol. 4, book 30, no. 3414); hata hivyo kwenye Paradiso ya Kiislamu, wakaaji watakuwa *"humo watavikwa vikuku vya dhahabu, na lulu, na mavazi yao humo yatakuwa hariri"* (**Q. 35:33;** angalia pia **Q. 18:31; 22:23; 76:12, 21**); na *"Watatembezewa sahani za dhahabu na vikombe"* (**Q. 43:71;** angalia pia **Q. 76:15** [*"Na watatembezewa vyombo vya fedha na vikombe vitakavyokuwa vya kioo,"*]). Hadithi nyingine inasema, "Nilikuwa nimekaa pamoja na Nabii [SAW] wakati mwanamke alipomjia na kusema: 'Ewe Mjumbe wa Allah, bangili mbili za dhahabu.' Alisema: 'Bangili mbili za Moto.'" (an-Nasa'i: 5142; angalia pia Abi Dawud: 4236; at-Tirmidhi: 637); hata hivyo, Wakaaji wa Paradiso ya Kiislamu *"humo watavishwa bangili za dhahabu, na lulu, na mavazi yao humo yatakuwa hariri"* (**Q. 22:23;** angalia pia **Q. 35:33**). Mohamedi pia alisema, "Mwanamke yeyote atakayevaa mkufu wa dhahabu shingoni, Allah atamwekea kitu kama hicho cha moto shingoni mwake" (an-Nasa'i: 5139; angalia pia Abi Dawud: 4238); hata hivyo, Allah atawaruhusu baadhi ya watu kutoka Jehanamu "na watakuwa na mkufu wa (dhahabu), na baadaye atawaingiza Paradiso" (al-Bukhari: 7439).

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

ambazo zinaonekana kwa sasa kwamba ni machukizo kutoka kwa Shetani lakini kwamba baadaye zitaruhusiwa na kutiwa moyo kuzitenda.

IV. Dhambi na Wokovu: Hitimisho

Sultan Mohamedi Khan alianzisha jambo ambalo liligusa moyo wa kila dini: suala la dhambi na Wokovu. Ukristo na Uislamu unaleta mitazamo miwili inayokinzana kwenye kwenye suala hilo. Nafasi ya Ukristo kwa uwazi inaangazia ndani. Inatambua kwamba kimsingi dhambi ni uasi juu ya Mungu na kuvunja mahusiano na Mungu ambayo huathiri vitu vingine vyote. Ukristo unatupa uchambuzi wa kina wa asili ya mwanadamu na kutoa maelezo ya kuaminika ya kwanini mwanadamu ana tabia na asili ya dhambi. Kwa usahihi unatambua kwamba wanadamu hawawezi kujiokoa wenyewe kutoka kwenye dhambi ya asili haijalishi ni kiwango gani watakavyojaribu. Hivyo Ukristo unakiri kwamba kama watu wataokolewa na asili zao kugeuzwa, basi ni Mungu pekee anayeweza kutufanyia kile ambacho sisi wenyewe hututaweza kujifanyia.

Ukristo pia una mtazamo wa wazi na wa hali ya juu kumhusu Mungu: Mungu ni mtakatifu, mwenye rehema, na haki. Ukristo unatambua kwamba msamaha una gharama kubwa: ni sehemu ya aliyekosewa kuzibeba gharama na kulipa fidia ya yule aliyetenda dhambi. Kwa Mungu kuwa mwanadamu kupitia mwanadamu Yesu Kristo na kuzichukua dhambi za wanadamu juu yake mwenyewe kama mwakilishi pale msalabani, mtazamo wa Ukristo pekee unaweza kuleta uwiano wa kusuluhisha masuala hayo yote hapo juu. Kama Sultan Khan alivyosema, “Kama Kristo aliahidi Wokovu bila ya kuyatoa maisha yake, madai ya Rehema kwa hakika yangekuwa yamekamilishwa. Ili kutosheleza hitaji la haki pia, Kristo alilipa fidia, ambayo ilikuwa ni Damu yake ya Thamani. Kwa njia hiyo Mungu aliudhihirisha Upendo wake kwetu.” (Khan 1992: 26)

Hatimaye, Ukristo unawawezesha watu kuupokea wokovu na maisha mapya hapa duniani ambapo yanahitajika sana. Hili linawapa Wakristo Amani ambayo hutokana na uhakika wa wokovu wao. Huwapa pia Wakristo msukumo wa kipekee wa kuishi maisha ya haki. Kama Timothy Keller alivyosema, “Dini huongozwa na kanuni ‘Nina tii—kwa hiyo Ninakubaliwa na Mungu.’ Lakini kanuni iongozayo Injili ni hii ‘Ninakubaliwa na Mungu kupitia kile ambacho Kristo alikifanya—kwa hiyo Nina tii.’” (Keller 2008: 179-80) Mungu wa Biblia “hasamehi tu” Wakristo, huwaandaa Wakristo kwa vitendo kuishi kama watakiwavyo kwa kuwapa Wakristo moyo mpya, ufahamu wa Kristo, na Roho Mtakatifu akaaye ndani. Hivyo hubadilishwa kutokea ndani kuja nje, na mwendelezo wa kazi ya Mungu ndani yao ili kwamba*“wafananishwe na mfano wa Mwana wake”* (**Warumi 8:29**).

Uislamu, kwa upande mwingine, haueleweki kwenye masuala yote yahusuyo dhambi na Wokovu. Mafundisho yao ya kimsingi kwamba watu huzaliwa wakiwa safi na kiasili wamepewa kutenda mema siyo tathmini ya kweli ya asili ya mwanadamu. Uislamu hauwezi kuelezea ujumla wa dhambi ya mwanadamu. Vivyo hivyo, mamlaka nyingi za Kiislamu hupingana na mafundisho yao na kukiri kwamba wanadamu wote kimsingi ni wakosaji na watenda dhambi kiasili. Kote kwenye Hadithi na kwingineko, Uislamu wanakiri fundisho la Wakristo la “anguko” la mwanadamu na urithi wetu wa asili ya dhambi kutoka kwa Adamu na Hawa (i.e., “dhambi ya asili”).

Wakati Allah, kama Mungu kwenye Biblia, anaitwa “mtakatifu,” “mwenye Rehema,” na mwenye “haki,” mamlaka kuu ya Kiislamu huihusisha moja kwa moja dhambi ya mwanadamu na tangazo la awali la Allah na kwa vitendo kujihusisha na maisha ya wanadamu hivyo kuwasababisha watende dhambi. Zaidi, tofauti na Mungu wa Biblia wa Upendo, Hadithi inafunua kwamba Allah “hajali” ikiwa watu wataenda Paradiso au Jehanamu. Haya yote hutuelekeza kwenye mtazamo mkanganyiko wa jinsi watu wanavyookolewa. Baadhi ya wenye mamlaka wa Kiislamu huzungumzia kuhusu kuyapima matendo mema na mabaya ya watu kwenye mizani, wakati wengine wenye mamlaka wakisema kwamba Allah husamehe au kutokusamehe watu kwa sababu zake mwenyewe, bila kuhusisha matendo ya watu au kirahisi tu, kuuhusisha mwelekeo wa ndani wa watu na tangazo la awali la Allah.

Kwenye Uislamu suala la Wokovu wa mtu hauamuliwa mpaka baada ya kifo. Kwa hiyo, hakuna Muislamu—pamoja na Mohamedi mwenyewe—anayeweza kuwa na uhakika hata kidogo kwamba dhambi zake zitasamehewa na kwamba ataenda Paradiso badala ya Jehanamu. Madhara ni kwamba Allah hawabadilishi Uislamu “kutokea ndani kuja nje” kama Mungu wa Biblia ambaye hufanya ndani ya Wakristo kwa Roho wake. Zaidi, bila kujali ahadi ya maburudisho ya Paradiso, Paradiso ya Kiislamu itakuwa imejawa na makosa yote na uovu wa dunia hii kwa sababu watu wakaao Paradiso hawatakuwa na tofauti na “kuanguka” kwao au asili ya dhambi waliyo nayo sasa.

Wakati wote, Mkanganyiko na kutokujitosheleza, mtazamo usiobadilisha wa Uislamu kuhusiana na Wokovu huishia kwenye ukweli kwamba Uislamu una mafundisho pungufu kuhusiana na Mungu na mwanadamu. Kama John Stott alivyoliweka, “Kama tukimshusha kwenye kiwango chetu na sisi kujikweza kwenye kiwango chake, kimsingi hatutaona sababu ya Wokovu, tumwache (Mungu) mwenyewe kwa ajili ya

Hakimiliki © 2015-2019 na Jonathan Menn. Haki zote zimehifadhiwa.

kutimiza fidia ya hili. Wakati, kwa upande mwingine, tumeuona utukufu wa ajabu wa utakatifu wa Mungu, na tumehukumiwa sana na dhambi zetu kwa Roho mtakatifu kiasi kwamba tunatetemeka mbele za Mungu na kujitambua kwamba tukoje, tukijiita 'wenye dhambi tunaostahili Jehanamu', tena na pekee tena umuhimu wa msalaba unadhihirika wazi kwamba tunastaajabia kwamba hatukuuona kabla." (Stott 1986: 109) Theologia hiyo ina matokeo muhimu siyo tu kwa mwelekeo wa mtu baada ya maisha haya kuisha lakini pia kwa maisha ya mtu na kwa hali ya jamii kwa sasa. Kwa mtazamo wa haya yote,Utofauti kati ya Ukristo na Uislamu umeangaliwa kwa kina na kimsingi.

ORODHA YA VYANZO

Kumbukumbu kamili ya bibliografia kwa nukuu kwenye maandiko yameonyeshwa kwenye bibliografia ya *Ukristo na Uislamu: Mambo Muhimu* ambayo yapo kwenye Wavuti ya ECLEA website at http://www.eclea.net/courses.html#islam.

MWANDISHI

Jonathan Menn anaishi Appleton, WI, USA. Alipokea shahada yake ya B.A. kwa masomo ya sayansi ya siasa kutoka kwa Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison, na taaluma ya heshima, mnamo mwaka wa 1974, baadaye akajumuika na Phi Beta Kappa kwa kuwa na heshima ya kijamii. Tena akapata J.D. kutoka kwa Shule ya Uanasheria cha Cornell, magna cum laude, mnamo mwaka wa 1977, na akawekwa kwenye mamlaka ya Kisheria ya Coif haki za heshima ya jamii. Akaitumia miaka iliyofuata 28 akifanya kazi za uanasheria, kama wakili, wa huko Chicago na baadaye akashirikiana na Shirika la mawakili liitwalo Menn Law Firm kule Appleton, WI. Alikuwa muumini na mfuasi wa Yesu Kristo tangu mwaka wa 1982. Alifundisha masomo ya Biblia darasa la watu wazima kwa miaka kadhaa. Kukua kwa pendo lake kwenye Theolojia na Huduma vilimfanya aende akatafute Shahada ya Uzamili ya mambo ya Mungu au Master of Divinity kwenye chuo cha Trinity Evangelical Divinity School huko Deerfield, IL. Alipokea shahada yake ya M.Div. kutoka kwa TEDS, summa cum laude, mnamo Mei 2007. Na sasa yeye ni mkurugenzi wa Huduma ya Kuwawezesha Viongozi wa Kanisa Afrika Mashariki (Equipping Church Leaders East Africa. "ECLEA"): **www.eclea.com.** Unaweza kuwasiliana na Jonathan kupitia na tovuti hii, na barua pepe kwa anuani hii: **jonathanmenn@yahoo.com.**